# Kutoka Ugomvi hadi Ushirikiano

## Ushirika wa Walutheri na Wakatoliki katika Ukumbusho wa Matengenezo ya Kanisa Mwaka 2017

# Kutoka Ugomvi hadi Ushirikiano

Ushirika wa Walutheri na Wakatoliki katika Ukumbusho wa Matengenezo ya Kanisa Mwaka 2017

**Ubunifu na Mpangilio**: Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani
The Lutheran World Federation (LWF)

**Picha ya Kitabu:** Kai-Michael Gustmann

**Tafsiri:** Chuo cha Biblia na Theologia Mwika, Tanzania

**Uhakiki wa Tasfiri na Mpangilio:** LWF Ofisi ya Mawasiliano na Dawati la Afrika

**Mchapishaji**: Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (LWF)
Route de Ferney 150
P. O. Box 2100
1211 Geneva 2
Switzerland

**Imechapishwa:** Moshi Lutheran Printing Press, Tanzania

**Toleo la Kiswahili:** Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania,
Moshi, Tanzania (KKKT), 2022

ISBN 978-9976-5629-3-4

# Yaliyomo


5 **Neno la Shukrani**

7 **Dibaji**

9 **Utangulizi**

11 **Mlango wa I**
*Maadhimisho ya Matengenezo ya Kanisa katika Enzi ya Kiekumeni na ya Ki-Utandawazi*
- 11 Sifa za Kumbukumbu Zilizopita
- 12 Kumbukumbu ya Kwanza ya Kiekumeni
- 13 Kumbukumbu Katika Mazingira Mapya ya Utandawazi na Mazingira ya Kidunia (Secular Context)
- 14 Changamoto Mpya kwa Kumbukumbu ya Mwaka 2017

17 **Mlango wa II**
*Mitazamo Mipya Juu ya Martin Luther na Matengenezo*
- 17 Michango ya Utafiti kwa Nyakati za Katikati
- 18 Utafiti wa Kikatoliki wa Karne ya Ishirini Juu ya Luther
- 20 Mikakati ya Kiekumeni Ilivyoandaa Njia ya Kufikiwa kwa Mwafaka
- 23 Umuhimu wa Majadiliano ya Kiekumeni

25 **Mlango wa III**
*Muhtasari wa Kihistoria wa Matengenezo ya Kanisa la Kilutheri na Itikio la Kanisa Katoliki*
- 25 Nini Maana ya Matengenezo (Reformation) ?
- 27 Chanzo cha Matengenezo: Mabishano Juu ya Vyeti vya Msamaha
- 28 Luther Kushtakiwa
- 29 Kushindwa Kukutana
- 30 Hukumu ya Martin Luther
- 31 Mamlaka ya Maandiko Matakatifu
- 32 Luther Akiwa Worms
- 33 Mwanzo wa Vuguvugu la Matengenezo
- 34 Mahitaji ya Usimamizi
- 35 Kuleta Maandiko Matakatifu kwa Watu
- 37 Jitihada ya Kitheolojia ya Kukabiliana na Ugomvi wa Kimadhehebu

**47 Mlango wa IV**
*Mada Kuu za Theolojia ya Martin Luther Katika Mtazamo wa Majadiliano kati ya Walutheri na Kanisa la Rumi*
47 Umbile la Mlango wa IV
48 Urithi wa Martin Luther Kutoka Karne za Katikati
49 Theolojia ya Utawa na Theolojia ya Kisirisiri (Monastic and Mystical Theology)
50 Kuhesabiwa Haki
63 Ekaristi
71 Huduma [ya Kichungaji]
77 Majadiliano Kati ya Walutheri na Wakatoliki kuhusu Huduma
84 Maandiko Matakatifu na Mapokeo

**95 Mlango wa V**
*Wito wa Maadhimisho ya Pamoja*
95 Ubatizo: Msingi wa Umoja na Maadhimisho ya Pamoja

**103 Mlango wa VI**
*Maazimio Matano ya Pamoja*

**107 Vifupisho**

**109 Maazimio ya Pamoja**
Awamu ya Kwanza (1967–1972)
Awamu ya Pili (1973–1984)
Awamu ya Tatu (1986–1993)
Awamu ya Nne (1995–2006)

**111 Tume ya Walutheri – Wakatoliki Kuhusu Umoja**

# Neno la Shukrani

Historia ya Wakristo Walutheri na Wakatoliki inashuhudia ufa uliojengeka baina yao kwa muda mrefu tangu Matengenezo ya Kanisa, mwaka 1517.

Kwa kipindi cha miaka 500 kumekuwepo uhasama na uadui uliodumu baina ya pande hizi mbili na kusababisha majeraha kwa watu wengi na baadhi yao kupoteza maisha.

Tunamshukuru Mungu kwa jitihada ambazo zimechukuliwa na Kamati iliyojumuisha Walutheri na Wakatoliki kukaa pamoja na kuona jinsi ya kupunguza au kuondoa ufa huu uliodumu kwa muda mrefu.

Mchakato wa Mazungumzo ya kitheologia baina ya pande hizi mbili yamedumu kwa muda mrefu. Tunamshukuru Mungu kwa matokeo chanya ya mazungumzo haya ambayo yamezaa *Azimio la Pamoja la Fundisho la Kuhesabiwa Haki* la mwaka 1999 (*Joint Declaration on the Doctrine of Justification*).

Andiko hili, *Kutoka Ugomvi hadi Ushirikiano* ni tokeo la majadiliano hayo ya muda mrefu yaliyotawaliwa na utii wa agizo la Yesu Kristo "*Wote wawe na Umoja kama wewe Baba ulivyo na umoja."* (Yoh.17:21)

Naipongeza kamati ya kuandaa jambo hili na jinsi mchakato ulivyoendeshwa hadi kufikia tukio la Lund Sweden, mwaka 2016, ambapo katika kuadhimisha yubile ya miaka 500 ya matengenezo ya Kanisa, viongozi wakuu wa Kanisa Katoliki na wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (LWF) walishiriki ibada ya pamoja kuasisi enzi mpya ya ushirikiano na maridhiano na kutia sahihi andiko hili.

> *"Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya – Kristo Yesu*" (Fil. 1:6)

Ni jambo la furaha kuwa andiko hili ambalo lilitokea katika lugha mbalimbali, kwa sasa limechapishwa katika lugha ya Kiswahili. Naipongeza na kuwashukuru kamati iliyohusika kutafsiri andiko hili hadi kufikia hatua ya kuchapishwa kwa lugha ya Kiswahili.

Nimelisoma andiko na nimefarijika sana kuona kuwa jambo hili limekuja kwa wakati huu ambapo utandawazi unafanya dunia kuwa kijiji. Hivyo,

mambo ya kujenga umoja yanapopata nafasi yataenea kwa kasi tofauti na enzi zile za Matengenezo ya Kanisa.

Andiko hili ni fundisho sahihi la Kikristo linalokaza roho ya uekumene, ninatoa rai kwa Wakristo wote hasa wa madhehebu yanayotajwa huku mara kwa mara, yaani, Wakatoliki na Walutheri kusoma na kutafakari ujumbe uliopo katika andiko hili kuweza kutazama upya mahusiano baina ya madhehebu haya mawili.

Hii itasaidia waweze kutoka katika mitazamo ya kuoneana mashaka hadi kuaminiana, kutoka kulaumiana hadi kushirikiana, kutiana moyo, na kutoka matengano hadi umoja.

Ninazihimiza taasisi zetu zinazotoa elimu ya theologia kulifanya andiko hili kuwa sehemu muhimu ya madai ya kitaaluma ili kuweza kuhamasisha na kuhimiza moyo wa kiuekumene kwa kudumisha mahusiano mazuri.

> *"Wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma."* (Yoh.17:21)

Kwa utukufu wa Mungu.

Askofu Dr. Fredrick Onael Shoo
Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT)
Desemba 2021

# Dibaji

Mahangaiko ya Martin Luther kuhusu Mungu yalitoa mwelekeo wa maisha yake. Swali lake kuu lilikuwa, "Nitawezaje kumpata Mungu mwenye neema?" Swali hili lilimtesa kila siku. Baada ya mahangaiko haya aliweza kumpata huyo Mungu mwenye neema katika Injili ya Yesu Kristo. "Theolojia ya kweli na ufahamu kuhusu Mungu vipo katika Kristo aliyesulubiwa." (Maneno haya ni kutoka Malumbano ya *Heidelberg)*

Mwaka 2017, Wakristo Wakatoliki na Walutheri, kwa pamoja watarudisha mioyo na mawazo yao ikiwa ni wakati muafaka wa kuangalia mambo yaliyotokea miaka 500 iliyopita, kwa kuipa Injili ya Yesu Kristo umuhimu wa kwanza. Injili lazima iadhimishwe na kutangazwa kwa watu wa kizazi chetu, ili watu wa dunia hii waamini kwamba Mungu mwenyewe anajitoa kwao wanadamu na anatualika sisi katika ushirikiano naye na Kanisa lake. Katika mambo haya ndimo ulimo msingi wa furaha yetu katika umoja wetu wa imani.

Katika furaha hii pia kuna kujifahamu sisi wenyewe, kujitathmini sisi wenyewe, sio tu katika historia yetu, bali hata katika hali halisi ya sasa. Sisi Wakristo bila shaka hatukuwa waaminifu mara zote kufuata Injili; bali mara nyingi tulivutiwa na mawazo na tabia ya mazingira yetu ya dunia. Kwa kufanya hivi, tena na tena tulizuia Habari Njema ya neema ya Mungu.

Kwa pamoja, kama mtu mmoja mmoja na kama jumuiya ya waaminio, sisi sote na mara zote tunahitaji kutubu na kuanza kwa upya, tukitiwa moyo na kuongozwa na Roho Mtakatifu. "Pale Bwana wetu Yesu Kristo aliposema, 'Tubuni' alitaka maisha mazima ya waamini yawe ya toba." Hivyo ndivyo inavyosomeka hoja ya kwanza katika hoja 95 za Martin Luther zilizoanzisha matengenezo mwaka wa 1517.

Ingawa hoja hii sio dhahiri kwa mtu wa siku hizi, sisi Wakristo Walutheri na Wakatoliki tunapenda kuichukulia kwa uzito wake kwa njia ya kujikosoa sisi wenyewe kwanza, sio kukosoana. Mwongozo wetu ni mafundisho ya kuhesabiwa haki, ambayo yanaeleza ujumbe wa Injili na kwa hiyo "mara zote yanasaidia kuelekeza mafundisho na matendo yote ya makanisa yetu kuelekea Kristo" (*Azimio la Pamoja la Fundisho ya Kuhesabiwa Haki - Joint Declaration on the Doctrine of Justification*).

Umoja wa kweli wa kanisa unaweza kuwepo pale tu ambapo pana ukweli wa Injili ya Yesu Kristo. Matokeo ya karne ya kumi na sita juu ya kupigania ukweli huu ni kupotea kwa umoja huu katika Ukristo wa Magharibi. Hii ni aibu kubwa katika historia ya kanisa. Mwaka 2017, lazima tuungame wazi kwamba tumetenda dhambi mbele ya Kristo kwa kuharibu umoja wa kanisa. Mwaka huu wa maadhimisho hayo, tunakabiliwa na changamoto mbili:

- kusafisha na kuponya majeraha ya mambo mabaya yaliyotokea, na
- kutengeneza tena umoja wa Kikristo kufuata ukweli wa Injili ya Yesu Kristo (Efeso 4:4–6).

Maandiko yanayofuata yanaeleza namna ya "kutoka ugomvi hadi ushirikiano"—njia ambayo bado hatujafikia lengo lake. Hata hivyo, Kamati ya muungano wa Walutheri na Wakatoliki ilizingatia sana maneno ya Papa Yohana XXIII, ambaye alisema: "Mambo yanayotuunganisha ni mengi kuliko mambo haya ambayo yanayotutenganisha."

Tunawaalika Wakristo wote kusoma kwa umakini ripoti hii ya kamati yetu na kupima vizuri ili kwa pamoja tuweze kuimarisha ushirika wa Wakristo wote pamoja.

Karlheinz Diez
Msaidizi wa Askofu wa Fulda
(kwa niaba ya Wakatoliki )

Eero Huovinen
Askofu Mstaafu wa Helsinki
Mlutheri mwenyekiti msaidizi

# Utangulizi

1. Mwaka 2017, Wakristo Walutheri na Wakatoliki wataadhimisha pamoja Jubilee ya miaka 500 ya mwanzo wa Matengenezo ya Kanisa. Walutheri na Wakatoliki wa leo wanafurahia hali inayojitokeza kati yao ya kuzidi kuelewana, kushirikiana na kuheshimiana. Wamefikia hatua ya kukubali kwamba yapo mambo mengi yanayowaunganisha pamoja kuliko mambo yale yanayowatenganisha: juu ya yote ni ile imani ya pamoja katika Mungu wa utatu na ufunuo katika Yesu Kristo pamoja na utambuzi wa ukweli na usahihi wa mafundisho ya kuhesabiwa haki kwa imani.

2. Tayari ile Jubilee ya miaka 450 ya Ungamo la Augsburg iliyofanyika mwaka wa 1980 ilitoa nafasi kwa wote, Walutheri na Wakatoliki, kuwa na uelewa wa pamoja juu ya misingi sahihi ya imani kwa kurejea kwa Yesu Kristo ambaye ni kiini cha imani ya Kikristo.[1] Kwenye Jubilee ya miaka 500 ya kuzaliwa Martin Luther iliyofanyika mwaka wa 1983, mazungumzo ya kimataifa kati ya Wakatoliki na Walutheri walikubaliana baadhi ya madai ya Luther. Ripoti ya kamati iliundwa kuangalia mambo haya ilimwita Luther "Shahidi wa Yesu Kristo" na ilitangaza kuwa, "Wakristo, wawe Waprotestanti au Wakatoliki, wasimdharau Martin Luther na ujumbe wake."[2]

---

[1] Roman Catholic/Lutheran Joint Commission, "All Under One Christ: Statement on the Augsburg Confession 1980," katika Harding Meyer and Lucas Visher (eds), *Growth in Agreement I: Reports and Agreed Statements of Ecumenical Conversations on a World Level, 1972–1982* (Geneva: World Council of Churches, 1984), 241–47.

[2] Roman Catholic/Lutheran Joint Commission, "Martin Luther: Witness to Jesus Christ" I.1, katika Jeffrey Gros, FSC, Harding Meyer and William G. Rusch (eds), *Growth in Agreement II: Reports and Agreed Statements of Ecumenical Conversations on a World Level, 1982–1998* (Geneva: WCC Publications, 2000), 438.

3. Mwaka ujao wa 2017 unatoa changamoto kwa Wakatoliki na Walutheri kujadiliana kwa pamoja mambo na matokeo ya Matengenezo ya Kanisa yaliyofanyika Wittenberg. Matengenezo haya ambayo kiini chake ni Martin Luther na mawazo yake. Hivyo lazima Wakristo wapokee maono yake na kuona njia nzuri ya kuyatumia siku hizi. Mawazo ya Matengenezo ya Kanisa ya Martin Luther, hadi leo, ni changamoto ya kiroho na kitheolojia kwa pande zote mbili, kwa Wakatoliki na kwa Walutheri.

# Mlango wa I

## Maadhimisho ya Matengenezo ya Kanisa katika Enzi ya Kiekumeni na ya Ki-Utandawazi

4. Kila kumbukumbu ina mazingira yake. Siku hizi mazingira haya yanaunganisha changamoto tatu kuu, ambazo zinaleta fursa na wajibu: (1) Ni kumbukumbu ya kwanza kutokea wakati wa enzi ya ekumeni Kwa hiyo, kumbukumbu hii ya pamoja ni nafasi kuimarisha uhusiano kati ya Wakatoliki na Walutheri. (2) Ni kumbukumbu ya kwanza kutokea wakati wa utandawazi. Kwa hiyo, kumbukumbu hii lazima iunganishe uzoefu na mitazamo ya Wakristo kutoka Kusini na Kaskazini, Mashariki na Magharibi. (3) Ni kumbukumbu ya kwanza inayobidi ishughulike na haja ya uInjilisti mpya katika kipindi ambacho kina sifa ya kukua kwa pamoja, kuanzisha mienendo mipya ya kidini, na wakati ule ule, kuongezeka kwa mitazamo ya kiulimwengu (secularization) mahali pengi. Kwa hiyo, kumbukumbu hii ya pamoja inatoa fursa na uwajibikaji wa kuwa ushuhuda wa pamoja wa imani.

### Sifa za Kumbukumbu Zilizopita

5. Mapema kuliko ilivyotarajiwa, tarehe ya 31 Oktoba 1517 ilikuwa alama ya awali ya Matengenezo ya Kanisa ya Kiprotestanti. Hata leo, makanisa mengi ya Kilutheri yanakumbuka tarehe ya 31 Oktoba kila mwaka, matukio yaliyofahamika kama "Matengenezo ya Kanisa." Sherehe za Jubilee za karne kwa karne za Matengenezo ya Kanisa ziliendeshwa kifahari na kianasa. Kwenye matukio haya mitazamo ya kinyume na vikundi tofauti vya kimadhehebu ilionekana sana. Kwa Walutheri siku hizo za kumbukumbu zilikuwa ni nafasi ya kuelezana tena historia hii ya mwanzo wa tabia ya mfumo wao wa kiInjili wa kanisa, ili kuhalalisha upekee wao. Matendo haya yalilenga moja kwa moja kwenye kukosoa Kanisa la Katoliki. Kwa upande mwingine,

Wakatoliki walichukulia matukio haya ya kumbukumbu kama fursa ya kuwalaumu Walutheri kwa kujitenga kwao kusikokubalika kutoka Kanisa la kweli na kuikana Injili ya Kristo.

6. Tena ajenda za siasa na za siasa ya Kanisa zilitawala kumbukumbu za karne hizo zilizopita. Kwa mfano mwaka 1617, fursa ya Jubilee ya miaka 100 ilisaidia kuimarisha na kuamsha sura ya pamoja ya Matengenezo ya Kanisa la Walutheri na la Warifoma. Kwenye sherehe zao za pamoja Walutheri na Warifoma walionyesha ushirikiano wao kwa njia ya mabishano makali dhidi ya Kanisa Katoliki. Kwa pamoja walifanya sherehe iliyomweka Luther kuwa kama mkombozi wa kuondoa nira ya Kirumi. Baadaye sana, mwaka 1917, katikati ya vita kuu ya duniani ya kwanza, walimchora Luther kama shujaa wa taifa la Kijerumani.

## Kumbukumbu ya Kwanza ya Kiekumeni

7. Mwaka 2017 utatokeza kumbukumbu ya kwanza ya karne ya matengenezo ya kanisa tangu kuanzishwa kwa enzi ya kiekumeni. Pia itaweka alama ya miaka hamsini ya Mawasiliano ya Walutheri na Wakatoliki. Kama sehemu ya mwendo wa kiekumeni, kuomba pamoja, kuabudu pamoja, na kuhudumia jumuiya zao pamoja kumetajirisha Wakatoliki na Walutheri. Pia sasa wanakabili kwa pamoja changamoto za kisiasa, za kijamii na za kiuchumi. Maisha ya kiroho yanayoonekana katika ndoa kati ya madhehebu yalileta mitazamo na maswali mapya. Walutheri na Wakatoliki wameweza kueleza kwa upya mapokeo na utekelezaji wao wa kitheolojia, kutambua jinsi walivyoathiriana. Kwa hiyo, wana hamu ya kukumbuka mwaka 2017 kwa pamoja.

8. Mabadiliko haya yanahitaji mtazamo mpya. Haifai tena kurudia tu maelezo ya zamani juu ya kipindi cha matengenezo ya kanisa, ambayo yaliwakilisha mara nyingi mitazamo ya Kilutheri na Kikatoliki kwa upande mmoja tu, tena mara nyingi kwenye kubishana. Kumbukumbu za kihistoria mara zote zinachagua matukio ya kihistoria kutoka

miongoni mwa matukio mengi ya kihistoria na zinaunganisha haya kuwa habari nzima yenye maana. Kwa sababu maelezo haya mara nyingi yalikuwa kwenye mabishano, mara nyingi yalikoleza ugomvi huu kati ya madhehebu na mara nyingine hata yalizalisha uadui wa wazi.

9. Namna hii ya kukumbuka historia iliathiri sana uhusiano kati ya madhehebu. Kwa sababu hii kumbukumbu ya kiekumeni ya Matengenezo ya Kilutheri ni muhimu tena ni ngumu wakati ule ule. Hata leo, Wakatoliki wengi wakisikia neno "Matengenezo ya Kanisa", mara moja wanahusianisha na mgawanyiko wa Kanisa, wakati Walutheri wengi wanaposikia "Matengenezo ya Kanisa" wanahusianisha na Ugunduzi tena wa Injili, hakika ya imani na uhuru wa Mkristo. Hivyo itatubidi kuzingatia asili hizi mbili ili kuunganisha mitazamo hii miwili na kuiwezesha kufanya mawasiliano pamoja.

## Kumbukumbu Katika Mazingira Mapya ya Utandawazi na Mazingira ya Kidunia (Secular Context)

10. Katika karne iliyopita, Ukristo umezidi kuwa dini ya kimataifa. Leo wapo Wakristo wa madhehebu mbalimbali ulimwenguni pote; idadi ya Wakristo wa kusini kwa dunia inaongezeka, wakati idadi ya Wakristo huko kaskazini inapungua. Makanisa ya Kusini yanapata umuhimu sana miongoni mwa Wakristo duniani pote. Makanisa haya hayaoni kwa urahisi ugomvi wa kimadhehebu wa karne ya kumi na sita kama ni ugomvi wao. hata kama makanisa haya yanaunganishwa na makanisa ya Ulaya au Marekani kwa njia ya jumuiya mbalimbali za Kikristo na kushirikiana pamoja mafundisho ya imani. Kuhusiana na mwaka wa 2017, itakuwa muhimu sana kuheshimu michango, maswali na mitazamo ya makanisa haya ya Kusini.

11. Katika nchi ambazo Ukristo umekuwepo kwa muda mrefu, siku za karibuni watu wake wengi wameondoka makanisani au wengine wamesahau mapokeo yao ya kikanisa. Katika mazingira hayo, makanisa yalirithisha kizazi baada ya kizazi ufahamu wao walioupata baada ya kusoma Maandiko Matakatifu: Ufahamu juu ya

Mungu, juu ya binadamu, na juu ya dunia kama itikio la ufunuo wa Mungu kupitia Yesu Kristo; tena walirithisha hekima iliyotokana na mahusiano ya muda mrefu ya Wakristo na Mungu tena walirithisha mambo ya liturgia, nyimbo na sala, Elimu ya Kikristo, na huduma za diakonia. Kama wengi wamesahau mambo haya yote, mambo mengi yaliyotenganisha kanisa zamani, hayafahamiki kwa watu wa leo.

12. Ekumeni, hata hivyo haiwezi kujikita yenyewe katika mambo ya kimapokeo yaliyosahaulika. Lakini, kwa jinsi gani basi kama watakuwa wamesahau, watakumbuka historia ya matengenezo mwaka 2017? Tena, mambo gani ya mabishano ya kimadhehebu ya karne ya kumi na sita yanastahili kutunzwa? Baba na Mama zetu wa imani walikuwa na hakika kwamba kuna kitu muhimu ambacho kilistahili kupiganiwa, kitu kilicho muhimu kwa maisha ya kiroho. Kwa njia gani mapokeo haya ya wazazi yaliyosahauliwa yanaweza kukabidhiwa kwa kizazi kingine? Mambo haya yasibaki kuwa mambo ya kihistoria tu, bali yawe msaada katika maisha ya Kikristo. Vile vile ni kwa njia gani mapokeo haya yanaweza kupitishwa bila kuanzisha ugomvi mwingine miongoni mwa Wakristo wa kiri tofauti.

## Changamoto Mpya kwa Kumbukumbu ya Mwaka 2017

13. Kwa karne nyingi kanisa na utamaduni vilikuwa vitu vilivyoungana kabisa. Kwa kadri karne zilivyoendelea kupita, mambo mengi ya maisha ya kanisa yalikuwa sehemu ya utamaduni wa nchi hizo. Kuainisha hali ndivyo ilivyo kwenye jamii hizi mpaka leo, hata kama watu hawategemei kanisa tena. Maandalizi ya mwaka 2017 yanatakiwa kutambua mambo katika jamii yanayoasilishwa na tamaduni za kanisa, kuyachambua, ukiongozwa na hali mbalimbali za mapokeo yaliyopo katika utamaduni wa sasa. Hii itasaidia kueleza, na kuendesha mawasiliano kati ya kanisa na utamaduni katika mwanga wa mitazamo hii mbalimbali.

14. Kwa zaidi ya miaka mia moja iliyopita, Wapentekoste na Wafuasi wa vikundi vya uamsho (charismatic movements) wameenea duniani

kote. Vikundihivi vilikaza mambo ambayo yalifanya mivutano katika mapokeo ya kimadhehebu yasiwe ndio kipaumbele chao. Mfumo huu wa kipentekoste upo pia katika makanisa mengi ukitokea kama uamsho au ushirika unaovuka mipaka ya kidhehebu. Kwa hiyo mwendo huu unatufungulia fursa mpya za kiekumeni lakini pia wakati huo huo kuzalisha changamoto nyingine. Hizi zote zitakuwa na nafasi ya maana katika maadhimisho ya matengenezo ya Kanisa mwaka 2017.

15. Jubilee za Matengenezo ya Kanisa zilizopita zilitokea katika nchi ambazo matengenezo yalianzia, au angalau katika nchi ambazo sehemu kubwa ya wananchi wake walikuwa Wakristo. Leo Wakristo wanaishi katikati ya mazingira ya dini mbalimbali. Wingi huu wa dini unaleta changamoto mpya kwa ekumeni. Sio kusema ekumeni haina maana tena, bali ni kinyume chake. Kazi ya ekumeni ni ya muhimu na ya haraka zaidi, kwa sababu uadui miongoni mwa Wakristo unaharibu imani ya Kikristo. Jinsi Wakristo wanavyoshughulikia tofauti katikati yao, inaweza kufunua kitu juu ya imani yao kwa watu wa dini nyingine. Kwa vile jambo la namna ya kushughulikia ugomvi ndani ya Ukristo ni muhimu wakati wa maadhimisho ya mwanzo wa matengenezo, kipengele cha mabadiliko ya mazingira ya dini mbalimbali kinastahili kupewa uzito katika kutafakariwa mwaka 2017.

# Mlango wa II

## Mitazamo Mipya Juu ya Martin Luther na Matengenezo

16. Mambo yaliyotokea zamani hayawezi kubadilishwa, lakini, kadri muda unavyopita, kipi na jinsi gani cha zamani kinachokumbukwa huweza kubadilika. Kumbukumbu hufanya kale kuwa leo. Ingawa zamani yenyewe haifai kubadilishwa, uwepo wa zamani katika wakati wa sasa unafaa kubadilisha. Kwa mtazamo wa 2017, hoja sio kusimulia historia tofauti, lakini kusimulia hiyo historia tofauti.

17. Walutheri na Wakatoliki wana sababu nyingi za kusimulia tena historia yao kwa namna mpya. Wamepata nafasi ya kukaribiana kwa njia ya uhusiano wa ukoo, kwa njia ya huduma ya misioni ulimwenguni kwa upana, na pia kwa umoja katika kupinga udhalimu maeneo mengi. Mawasiliano haya ya kina yamebadilisha namna ya kutazamana, na kuibua hitaji kubwa la majadiliano ya kiekumeni na utafiti zaidi. Ekumeni imebadilisha maoni ya makanisa juu ya matengenezo: Watheolojia wa Kiekumeni wameamua kutosisitiza juu ya udhehebu kwa lengo la kukaribiana na wenzao wa upande mwingine. Ni afadhali watafute yanayowaunganisha pamoja katika tofauti zao, hata katikati ya upinzani, hivyo kuwekeza katika kuondoa tofauti zinazoyagawanya makanisa.

### Michango ya Utafiti kwa Nyakati za Katikati

18. Utafiti umechangia sana katika kubadilisha mtazamo wa kale kwa njia mbalimbali. Katika suala la Matengenezo ya Kanisa, mchango huu unajumuisha maelezo ya kanisa la Kiprotestanti na la Katoliki juu ya historia ya kanisa. Michango ambayo imeweza kusahihisha uelewa mbalimbali kimadhehebu juu ya historia, kwa kutumia mwongozo madhubuti kujipima katika misimamo mbalimbali. Kwa

upande wa Wakatoliki hii ni sawa hasa kwa utafiti wa kisasa juu ya Luther na matengenezo. Kwa upande wa Waprotestanti, inahusu hasa kwa msimamo juu ya Theolojia ya nyakati za katikati na mabadiliko na kupanuka kwa mtazamo juu ya nyakati za katikati. Kwenye muonekano wa kisasa juu ya kipindi cha Matengenezo, upo umakini mpya juu ya mambo mengi ambayo sio ya kitheolojia, — mambo ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Kwa Kutumia kielelezo cha ukiri, waliweza kufanya masahihisho muhimu katika mafundisho ya zamani juu ya historia.

19. Nyakati za mwisho za zama za katikati hazitazamiki tena kama za giza, kama ambavyo Waprotestanti walifafanua kila mara, wala sio za nuru tupu, kama Wakatoliki walivyoeleza katika mafundisho ya zamani. Nyakati hizi kwa sasa zinaonekana kama zilikuwa na upinzani mkubwa — uongofu wa nje dhidi ya upungufu mkubwa; mtazamo wa theolojia ya matendo mema tu kwa maana ya *do ut des* ("Ninakupa ili unipe") dhidi ya kuitegemea neema ya Mungu tu; kutojali wajibu wa kidini, hata madai ya kiofisi, dhidi ya matengenezo makali kama ilivyokuwa katika maadili ya jumuiya kadhaa za kitawa.

20. Kanisa halikuwa la mfumo wa mawazo ya aina moja, hata kidogo; *corpus christianum (mwili wa Kikristo)* ulibeba theolojia nyingi tofauti, mfumo wa maisha mbalimbali na mifumo mingi tofauti ya Kanisa. Wanahistoria wanasema kwamba karne ya kumi na tano ilikuwa ni karne ya uamsho wa pekee ndani ya kanisa. Ni Wakati huu idadi kubwa ya Wakristo wa kawaida walipata elimu nzuri. Hivyo walihitaji kusikiliza mahubiri mazuri zaidi na theolojia iliyoweza kuwasaidia kuishi maisha ya Kikristo. Luther alianzia katika mikondo hii ya theolojia na uamsho na kuvikuza zaidi.

## Utafiti wa Kikatoliki wa Karne ya Ishirini Juu ya Luther

21. Utafiti wa Kikatoliki juu ya Luther ulitokana na hamu ya Wakatoliki ya kufahamu zaidi historia ya matengenezo. Hamu hii iliibuka wakati wa nusu ya pili ya karne ya kumi na tisa. Watheolojia hawa

walifuata juhudi za Wakatoliki waliokaa katika milki ya Ujerumani iliyotawaliwa na Waprotestanti. Hawa walitaka kujiweka huru dhidi ya mafundisho ya Kiprotestanti, ambayo yalikaza upande mmoja tu, kupinga Rumi. Mafanikio katika utafiti wa Kikatoliki yalikuja kwa hoja, kwamba Luther aliushinda Ukatoliki fulani ndani yake, ambao haukuwa Ukatoliki kamili. Kutokana na mtazamo huu, maisha na mafundisho ya kanisa la nyakati za katikati yalitumika kama ufunguo wa kukana mambo ya msingi ya matengenezo; Kutindikiwa kwa ukatoliki kulifanya mabishano ya kidini ya Luther kushawishi wengi.

22. Kwa namna nyingine mpya, Luther alioneshwa kama mtu mwenye bidii kidini na kama mtu mwombaji mwaminifu. Utafiti makini na wa kina unaonesha kwamba vitabu vya Kikatoliki juu ya Luther, kwa karne nne zilizopita hadi leo, kwa kiasi kikubwa, vimeathiriwa na maelezo ya Yohana Cochaleus, mpinzani wa Luther na mshauri wa mtawala George wa Saxony. Cochaleus alimchukulia Luther kama mtawa aliyeasi katika imani, mharibifu wa Ukristo, mpotoshaji wa maadili, na mzushi. Mafanikio ya kipindi hiki cha kwanza cha kujishughulisha na tabia ya Luther, kwa utafiti wa kina lakini wenye huruma ndani yake, yalikuwa ni kujinasua kwa tafiti zilizofanywa na Wakatoliki toka mtizamo ulioelemea upande moja kuhusu Luther. Tafiti zenye busara za Watheolojia Wakatoliki wengine zilionesha, kwamba kutengana hakukusababishwa na madai ya msingi ya matengenezo ya kanisa, mfano fundisho la kuhesabiwa haki, bali tabia ya Luther ya kukosoa hali halisi ya kanisa la wakati ule iliyoasilishwa na mahangaiko yake.

23. Hatua nyingine ya utafiti wa Kikatoliki juu ya Luther ilikuwa kugundua mambo yanayofanana katika mifumo na miundo ya kitheolojia mbalimbali, hasa kwa njia ya kulinganisha, kwa utaratibu, kati ya Watheolojia wawili wa muhimu wa madhehebu haya mawili ambao ni Thomas Aquinas na Martin Luther. Kazi hii iliwaruhusu Watheolojia kuelewa theolojia ya Luther ndani ya mfumo wake. Wakati huo huo, utafiti wa Kikatoliki ulipima maana ya fundisho la kuhesabiwa haki ndani ya Ungamo la Augsburg. Hapa iliwezekana kuona mawazo ya matengenezo ya Luther katika mazingira mapana zaidi ya utunzi wa kiri za imani za Kilutheri. Matokeo yalikuwa ni mwonekano wa

Ungamo la Augsburg kama maelezo ya msingi ya matengenezo na utunzaji wa umoja wa kanisa.

## Mikakati ya Kiekumeni Ilivyoandaa Njia ya Kufikiwa kwa Mwafaka

24. Juhudi hizi zilielekea moja kwa moja kwenye mradi wa kiekumeni. Mradi huu ulianzishwa mwaka 1980 na Watheolojia Walutheri na Wakatoliki nchini Ujerumani kwenye tukio la jubilee ya miaka 450 ya uwasilishaji wa Ungamo la Augsburg. Hii pia ilikuwa nafasi kwa upande wa Wakatoliki kulitambua Ungamo la Augsburg. Mafanikio mapana ya baadaye ya kamati nyingine ya ekumeni ya Watheolojia wa Kiprotestanti na Kikatoliki, iliyoasilika katika utafiti huu wa Kikatoliki juu ya Luther, ilizaa andiko la: *Tuhuma za Kipindi cha Matengenezo: Bado zinatutenganisha? (The Condemnations of the Reformation Era: Do They Still Divide?)*[1]

25. Azimio la Pamoja la Fundisho la Kuhesabiwa Haki *(Joint Declaration on the Doctrine of Justification)*,[2] ambalo Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani Duniani na Kanisa la Katoliki walilisaini wote kwa pamoja mwaka 1999, lilijengwa juu ya misingi hii. Pia lilijengwa juu ya kazi ya majadiliano ya Marekani juu ya kuhesabiwa haki kwa Imani (*Justification by Faith)*,[3]. Ilithibitisha makubaliano juu ya ukweli wa msingi wa mafundisho ya kuhesabiwa haki baina ya Walutheri na Wakatoliki.

---

[1] Karl Lehmann and Wolfhart Pannenberg (eds), *Condemnations of the Reformation Era: Do They Still Divide?* tr. Margaret Kohl (Minneapolis, MN: Fortress, 1990).

[2] The Lutheran World Federation and the Roman Catholic Church, *Joint Declaration on the Doctrine of Justification* (Grand Rapids, Michigan/Cambridge, U. K.: William B. Eerdmans, 2000). Iliyochapishwa awali kama *Gemeinsame Erklärung zur Rechtfertigungslehre* (Frankfurt am Main: Verlag Otto Lembeck/ Paderborn: Bonifatius-Verlag, 1999).

[3] H. George Anderson, T. Austin Murphy, Joseph A. Burgess (eds), *Justification by Faith,* Lutherans and Catholics in Dialogue VII (Minneapolis, MN: Augsburg Publishing House, 1985).

### *Maendeleo Upande wa Wakatoliki*

26. Mtaguso wa Pili wa Vatikani, kama itikio kuhusu Maandiko Matakatifu, liturgia na uamsho wa mababa wa miongo iliyotangulia, ulishughulika na mada kama: kuheshimu Maandiko Matakatifu katika maisha ya Kanisa; kutambua tena ukuhani wa wote waliobatizwa; hitaji la kuendelea kutakasa na kutengeneza kanisa; uelewa wa uongozi katika kanisa kama huduma; umuhimu wa uhuru na wajibu wa binadamu; ikihusisha kutambua uhuru wa kidini.

27. Mtaguso huu pia ulithibitisha alama za utakaso na ukweli hata nje ya miundo ya Kanisa la Katoliki la Rumi. Ulisisitiza "alama na mali zilizowekwa wakfu, zinazojenga na kutoa maisha kwa kanisa lenyewe, zinaweza kuwepo nje ya mipaka ionekanayo ya Kanisa Katoliki,". Mtaguso ulizitaja alama hizo "Neno la Mungu lililoandikwa; maisha ya neema; imani; matumaini na matendo ya huruma; pamoja na vipawa vingine vya Roho Mtakatifu vya ndani, na pia alama zinazoonekana." (*UR* 1).[4] Vile vile Mtaguso huu ulizungumza juu ya "matendo mengi ya kiliturgia ya dini ya Kikristo" ambayo yanatumiwa na "ndugu" waliotenganishwa, na kusema, "haya bila shaka yanaweza kusababisha kweli maisha ya neema kwa njia mbalimbali ambazo zinatofautiana kulingana na hali ya kila kanisa au jumuia. Matendo haya ya kiliturgia ni muhimu kutazamwa kama yenye uwezo kwa kutuunganisha na jumuiya ya wokovu" (*UR* 3). Utambuzi huu ulienea sio tu kwa alama moja moja na matendo katika jumuiya hizi, bali pia katika "makanisa na jumuiya zilizogawanyika" zenyewe. "Kwa kuwa Roho wa Kristo hajaacha kutumia mambo haya kama njia ya wokovu" (*UR* 1.3). *(Maelezo ya wafasiri: Kwa msingi walikubali kwenye mtaguso huu kwamba wokovu unaweza kupatikana hata nje ya Kanisa la Katoliki.)*

28. Kwa mtazamo wa kufanywa upya kwa theolojia ya Kikatoliki, uliokuwa bayana katika Mtaguso wa Pili wa Vatikani, Wakatoliki wa

---

[4] *Unitatis Redintegratio = UR 3.*

leo wanaweza kuyakubali mahangaiko ya matengenezo ya Martin Luther na kuyathamini kwa uwazi zaidi kuliko ilivyoonekana zamani.

29. Uhusiano ambao ulijitokeza bila kufunuliwa na hoja za Luther ulipelekea kutathmini Ukatoliki wake kwa upya, ambao ulitokea katika mazingira ya kutambua kwamba, makusudi yake yalikuwa kutengeneza kanisa, sio kulitenganisha. Hii inaonekana katika maandiko ya Yohana Kadinali Willebrands na Papa Yohana Paulo II.[5]. Kwa sifa hizi mbili za msingi kuhusu utu na theolojia yake kulileta uelewa mpya wa kiekumeni kuhusu Luther kama shahidi wa Injili."

30. Papa Benedikti pia alitambua jinsi utu na theolojia ya Martin Luther vimeleta changamoto ya kiroho na kitheolojia kwa theolojia ya Kikatoliki ya wakati huu. Hili lilidhihirika mwaka 2011 wakati Papa alipotembelea nyumba ya Utawa ya Augustino huko Erfurt ambapo Luther aliishi kama mtawa kwa takriban miaka sita. Papa Benedikti alisema, "Jambo lililomsukuma [Luther] mara zote lilikuwa ni swali kumhusu Mungu, hisia hii na yenye kumsukuma sana ilitawala maisha yake yote. 'Nitawezaje kumfikia Mungu mwenye neema?' – swali hili lilimsumbua sana moyoni na lilijikita katika msingi wa kila utafiti wake wa kitheolojia na mahangaiko yake yote ya ndani. Kwake, theolojia haikuwakazi ya kitaaluma tu, bali ilikuwa mahangaiko juu ya njia yake ya uzima, ambayo ilimaanisha mahangaiko yake pamoja na Mungu. 'Nitampataje Mungu mwenye neema?' Ukweli kwamba, swali hili lilikuwa nguvu ya kumsukuma Luther maisha yake yote, ukweli huu haukuacha kuamsha hisia moyoni mwangu tena na tena. Kwani kwa kweli, nani anajali swali hili siku hizi?—hata miongoni mwa Wakristo? Swali hili juu ya Mungu lina maana gani katika maisha yetu? Katika mahubiri yetu? Watu wengi siku hizi, hata Wakristo, wanafikiri kwamba Mungu kimsingi hajali dhambi au maadili yetu."[6]

---

[5] Jan Willebrands, "Lecture to the 5th Assembly of the Lutheran World Federation, on July 15, 1970," katika *La Documentation Catholique* (6 September 1970), 766; John Paul II, "Letter to Cardinal Willebrands for the Fifth Centenary of the Birth of Martin Luther," Katika *Information Service,* no. 52 (1983/II), 83–84.

[6] Benedict XVI, "Address," Meeting with the Council of the Evangelical Church in Germany, September

### *Maendeleo Upande wa Walutheri*

31. Utafiti wa Kilutheri juu ya Luther na matengenezo pia umepiga hatua ya kimaendeleo. Uzoefu wa vita kuu mbili za dunia ulivunja fikra kuhusu mwendelezo wa historia. Pia uzoefu huu ulivunja uhusiano kati ya Ukristo na utamaduni wa kimagharibi. Wakati huo uamsho wa theolojia ya kuhubiri ulifungua njia mpya kutafakari juu ya Luther. Majadiliano na wataalamu wa historia ilisaidia kuunganisha mambo ya kihistoria na kijamii ndani ya maelezo juu ya matengenezo. Watheolojia wa Kilutheri walitambua mchanganyiko wa maoni ya kitheolojia na makusudi ya kisiasa sio kwa upande wa Wakatoliki tu, bali hata kwa upande wao. Majadiliano na Watheolojia wa Kikatoliki yalisaidia kuondoa misimamo ya kimadhehebu ya upande mmoja tu na kuanza kujikosoa binafsi juu ya mambo ya mapokeo yao.

## Umuhimu wa Majadiliano ya Kiekumeni

32. Washirika wa majadiliano haya, Wakatoliki na Walutheri, wamejikita katika mafundisho ya makanisa yao, ambayo kwa mitazamo yao, yanaeleza ukweli wa imani. Mafundisho ya makanisa haya mawili yanaonesha umoja mkubwa, lakini yanaweza kutofautiana, hata yanaweza kuwa kinyume katika ufunzi wao. Kwa ajili ya misimamo ya mafundisho ya madhehebu haya majadiliano yamewezekana. Kwa ajili ya tofauti ya misimamo majadiliano ni muhimu.

33. Majadiliano yanaonesha kwamba washiriki wanazungumza lugha tofauti na wana ufahamu wa tofauti ya maana ya maneno; Wanatofautisha tofauti na wanatumia mbinu tofauti za kutafakari. Hata hivyo, kitu kinachoonekana kuwa kinyume katika maelezo, labda sio kinyume katika maana yake. Ili kufahamu kikamilifu uhusiano wa makala za mafundisho, lazima maandiko yafafanuliwe katika

---

23, 2011, katika **www.vatican.va/holy_father/benedict_xvi/speeches/2011/september/documents/hf_ben-xvi_spe_20110923_evangelical-church-erfurt_en.html**; tafsiri imebadilishwa.

mwanga wa mazingira ya historia ambapo yanaasilika. Tukifanya hivyo, tunaweza kutambua ni wapi kuna tofauti, hata kupishana, au ni wapi hakuna.

34. Majadiliano ya kiekumeni unamaanisha kuongoka kutoka misimamo ya fikra inayoasilika katika kusisitiza tofauti kati ya madhehebu. Badala yake, wajumbe wa majadiliano ya kiekumeni wanatafuta kwanza mambo yaanayowaunganisha. Baadaye wanaanza kutathmini umuhimu wa tofauti zao. Si kwamba wanapuuza au kukwepa tofauti hizi, kwa sababu majadilino ya Kiekumeni ni utafiti wa pamoja wa ukweli wa imani ya Kikristo.

# Mlango wa III

## Muhtasari wa Kihistoria wa Matengenezo ya Kanisa la Kilutheri na Itikio la Kanisa Katoliki

35. Leo tunaweza kusimulia historia ya matengenezo ya Kilutheri kwa pamoja. Pamoja na kwamba Wakatoliki na Walutheri wangali wana maoni tofauti, lakini kutokana na majadiliano ya ekumeni, wameweza kushinda msimamo wa kitamaduni wa kutazamana kama maadui, Waprotestanti wakipinga Wakatoliki na Wakatoliki wakipinga Waprotestanti. Badala yake wameweza kwa pamoja kutafuta njia ya kukumbuka mambo yaliyopita. Mlango huu haueleze historia nzima ya matengenezo pamoja na mambo makuu ya kitheolojia ambayo yalileta kuhitilafiana kwa pande hizi mbili. Bali mlango huu unaelezea kwa ufupi juu ya hali muhimu ya kihistoria na mambo muhimu ya kitheolojia ya matengenezo ya karne ya kumi na sita.

### Nini Maana ya Matengenezo (Reformation) ?

36. Zamani sana, neno la Kilatini la *reformatio* lilitumika kwa maana ya kubadilisha hali mbaya iliyopo kwa kurudisha tena hali nzuri na bora ya wakati uliopita. Katika zama za kati (middle ages), dhana ya *reformatio* mara nyingi ilitumika kwenye mazingira ya matengenezo kwenye nyumba za utawa. Jumuiya za watawa zilianzisha matengenezo ili kulinda nidhamu ya maisha ya kidini. Kwa mfano, katika karne ya kumi, vuguvugu la matengenezo makubwa sana, lilianza katika nyumba ya utawa ya Cluny.

37. Mwishoni mwa zama za kati, umuhimu wa dhana ya matengenezo ulianza kutumika katika kanisa nzima. Katika Mikutano Mikuu ya Kanisa na katika karibu kila kikao cha Dola Takatifu ya Kirumi walishughulika na *reformatio (matengenezo).* Mkutano Mkuu wa Constance (1414–1418) uliona ni lazima kufanya matengenezo

ya kanisa "kwa viongozi na waumini".[1] Andiko la matengenezo lililosambazwa likiwa na kichwa, "Reformacion keyser Sigmunds", lilikaza umuhimu wa matengenezo kwenye sheria na karibu kila sehemu ya maisha. Mwishoni wa karne ya kumi na tano wazo la matengenezo lilienea hadi serikalini na katika vyuo vikuu.[2]

38. Luther mwenyewe ni mara chache alitumia dhana ya "matengenezo." Katika "maelezo yake ya Hoja tisini na tano", Luther alisema, "Kanisa linahitaji matengenezo ambayo sio kazi ya mtu, kama Papa, au watu wengi, kama makadinali, kama tulivyoziona kazi zao (za pande zote mbili) kwenye mikutano mikuu iliyopita, bali ni kazi ya dunia nzima. Ni kazi ya Mungu mwenyewe. Zaidi ya yote, Mungu, aliyeumba muda, ndiye anayefahamu wakati kwa matengenezo haya."[3] Mara nyingine Luther alitumia neno "matengenezo" ili aeleze uboreshaji wa maagizo au utaratibu, kwa mfano wa vyuo vikuu. Katika maandiko yake ya kimatengenezo "Address to the Christian Nobility" ya 1520, alisisitiza kuwepo kwa "mkutano wa haki na uhuru" ili kutoa nafasi ya kujadiliana mapendekezo ya matengenezo.[4]

39. Neno "Matengenezo" lilikuja kutumika kwa maana finyu likizungumzia matukio ya kihistoria, hasa katika kipindi cha miaka ya 1517 hadi 1555, tangu kusambazwa kwa "hoja 95" za Martin Luther hadi wakati wa kupatikana kwa amani ya Augsburg. Mabishano ya kitheolojia na kikanisa,

---

[1] Council of Constance, session 3, 26 March 1415.

[2] Ona The Lutheran World Federation and Pontifical Council for Promoting Christian Unity, *The Apostolicity of the Church: Study Document of the Lutheran–Roman Catholic Commission on Unity* (Minneapolis, MN: Lutheran University Press, 2006), 92, n.8. [= *ApC*].

[3] Martin Luther, "Explanations of the Ninety-Five Theses," tr. Carl W. Folkemer, katika Helmut T. Lehmann and Jaroslav Pelikan (eds), *Luther's Works,* American Edition, 55 vols, (Philadelphia and St. Louis, 1955–1986), 31:250. (=*LW*); *WA* 1, 62, 27–31.

[4] Luther, "To the Christian Nobility of the German Nation concerning the Reform of the Christian Estate," Tr. Charles M. Jacobs, Rev. James Atkinson, katika *LW* 44:127; *WA* 6, 407, 1.

ambayo yalianzishwa na Theolojia ya Luther, haraka yalichanganyika na mambo ya siasa, mambo ya uchumi, na mambo ya utamaduni, kwa sababu ya hali halisi ya wakati ule. Hivyo kinachomaanishwa na neno "Matengenezo" kinajumuisha mengi kuliko yale Luther mwenyewe aliyofundisha na aliyokusudia. Dhana ya "Matengenezo" kama kiwakilishi cha kipindi fulani katika historia ilitoka kwa Leopold von Ranke ambaye katika karne ya kumi na tisa alieneza kwa watu desturi ya kuzungumza juu ya "kipindi cha matengenezo."

## Chanzo cha Matengenezo: Mabishano Juu ya Vyeti vya Msamaha

40. Tarehe 31. Oktoba 1517, Luther alipeleka kwa Askofu mkuu Albrecht wa Mainz barua ikiwa na kiambatanisho cha "hoja 95" zilizokuwa na kichwa cha habari, "Mabishano juu ya manufaa na nguvu ya vyeti vya msamaha." Katika barua hii Luther alionesha mashaka yake makubwa juu ya matokeo ya mahubiri na matumizi ya vyeti vya msamaha uliosimamiwa na Askofu Mkuu huyu. Luther alimsihi sana kufanya mabadiliko. Siku ile ile, aliandika barua nyingine kwa Askofu wake wa Dayosisi, Hieronymus wa Brandenburg. Luther alipotuma hoja zake kwa wenzake wachache na huenda pia alizibandika katika mlango wa kanisa la mji wa Wittenberg, alitaka kuanzisha mjadala. Mjadala huu uwe wa wasomi juu ya maswali tata ambayo yalikuwa hayajapatiwa ufumbuzi juu ya nadharia na matumizi ya vyeti vya msamaha.

41. Vyeti vya Msamaha vilichukua nafasi muhimu sana katika maisha ya wokovu wa wakati ule. Cheti kimoja kilikuwa na uwezo wa kutoa msamaha wa adhabu kwa mwenye dhambi kwani hatia yake ilikuwa imefutwa kwa njia ya cheti hiki. Wakristo waliweza kupokea cheti hiki wakitimiza masharti fulani yaliyowekwa —kama vile maombi, matendo ya huruma, na kutoa sadaka - Mambo yaliyotekelezwa kwa njia ya tendo la kanisa, ambalo Wakristo waliamini liligawa hazina ya malipo ya matendo mema ya Kristo na Watakatifu kwa waliohitaji msamaha.

42. Kwa maoni ya Luther, utoaji wa vyeti vya msamaha uliharibu maisha ya kiroho ya Mkristo. Aliuliza kama ni kweli vyeti hivi vingeweza kuwapa uhuru wakosaji kutoka adhabu iliyotolewa na Mungu; tena aliuliza kama adhabu zozote zilizowekwa na mapadri, zingeweza kuhamishiwa katika toharani (purgatory); vile vile aliuliza kama makusudi ya kumponya na kumtakasa mtu yaliyokusudiwa na adhabu hizi yangemfanya kupendelea kuteswa badala ya kukombolewa kutoka hayo; zaidi tena aliuliza kama pesa iliyonunua vyeti vya msamaha si bora ingetolewa kuwa msaada kwa maskini. Luther pia alionesha mashaka yake kama kweli ilikuwepo hazina ya kanisa ya matendo mema, ambayo Papa aliweza kuitumia kutolea vyeti vya msamaha.

## Luther Kushtakiwa

43. "Hoja tisini na tano" za Luther zilienezwa haraka sana katika eneo la Ujerumani na zilisababisha mtafaruku mkubwa na pia kuharibu vibaya kampeni za kuuza vyeti vya msamaha. Mara moja ilivumishwa kwamba Luther angeshtakiwa kwa ajili ya uzushi. Ilipofika Desemba 1517, Askofu Mkuu wa Mainz alikuwa tayari amezituma Rumi hizo "hoja tisini na tano" pamoja na maandiko mengine, ili kupima theolojia ya Luther.

44. Luther alishangazwa na mwitikio kwa hoja zake, kwani hakutegemea lile kuwa jambo la kujadiliwa na kila mtu bali jambo la kuamsha majadiliano makali kati ya wasomi. Alikuwa na wasiwasi kwamba hoja zake zingeweza kueleweka vibaya kama zingelisomwa na watu wasiokuwa na taaluma hii. Kwa hiyo, mwishoni mwa Machi 1518, alichapisha hotuba katika lugha ya wenyeji (Kijerumani), "Juu ya Vyeti vya Msamaha na Neema" ("Sermo von Ablass und Gnade"). Kilikuwa kijitabu kilichosomwa sana na watu wengi na kilimfanya Luther afahamike mahali pote Ujerumani. Luther alisisitiza tena na tena kwamba, nje ya hoja nne za kwanza, hoja hizi sio msimamo na maoni yake, bali ni kauli zilizoandikwa kwa majadiliano.

45. Viongozi wa Kanisa kule Rumi walikuwa na wasiwasi kwamba mafundisho ya Luther yangedhoofisha kanuni ya kanisa na mamlaka ya Papa. Hivyo, Luther aliitwa kufika Rumi ili ajibu mbele ya mahakama ya Vatikani kuhusu theolojia yake. Lakini, kufuatia ombi la mkuu wa mkoa wa kifalme wa Saxony, Friedrich mwenye Hekima, mashtaka yalihamishiwa Ujerumani, kwenye mkutano mkuu wa milki katika Augsburg. Kadinali Cajetan alipewa amri ya kumhoji Luther. Amri ya Papa iliagiza kwamba Luther abatilishe au, kama ingetokea atakataa, yule Kadinali alikuwa na mamlaka ya kumpiga marufuku Luther mara moja au kumkamata na kumpeleka Rumi. Baada ya mkutano, Cajetan aliandika hati ya mashtaka kwa mamlaka (ya mafundisho) ya Kanisa, na Papa aliitangaza muda mfupi baada ya mahojiano ya Augsburg bila kujibu hata kidogo hoja za Luther.[5]

46. Hisia kinzani za msingi zilitawala mchakato wote ulioishia kumtenga Luther na kanisa. Luther alitoa maswali kwa majadiliano na alipendekeza hoja. Yeye na wananchi, waliokuwa wameelimishwa juu ya msimamo wake na maendeleo ya mambo haya, kupitia vipeperushi na machapisho, walitegemea kuona majadiliano ya hoja. Luther alikuwa ameahidiwa kupata mashtaka ya haki. Hata hivyo, ingawa alihakikishiwa kwamba angesikilizwa, tena na tena alipata ujumbe tu, kwamba ama afute theolojia yake au angetangazwa kuwa mwasi.

47. Tarehe 13 Oktoba, 1518, kwenye taarifa maalum ya kupinga (*protestatio)*, Luther alidai kwamba anakubaliana na Kanisa takatifu la Kirumi. Na hangeweza kukana maoni yake pasipo kushawishiwa kwamba alikuwa amekosea. Tarehe 22 Oktoba, tena alisisitiza kwamba aliwaza na kufundisha kulingana na mafundisho ya Kanisa la Kirumi.

## Kushindwa Kukutana

48. Kabla hajakutana na Luther, Kadinali Cajetan alikuwa amesoma kwa makini sana maandiko ya Luther, ambaye alikuwa profesa

[5] Leo X, *Cum postquam*, 9 November 1518, DH 1448, cf. 1467 na 2641.

wa Wittenberg. Pia alikuwa ameandika makala juu yake. Lakini Cajetan alitafsiri maandiko ya Luther kwa kutumia ulimwengu wake mwenyewe wa kuwaza kiasi kwamba alimwelewa vibaya Luther, hasa kwenye suala la uhakika wa imani, hata alipo wasilisha kwa usahihi kila kitu kuhusu msimamo wa Luther. Kwa upande wake, Luther hakuwa na uzoefu na theolojia ya Kadinali huyu na katika kuhojiana kulikuwa na nafasi ndogo ya majadiliano na hili lilimfanya Luther kukana. Luther hakupata nafasi ya kuufahamu msimamo wa Kadinali. Hili ni sikitiko kubwa kwamba Watheolojia wawili wa pekee wa karne ya kumi na sita walikutana kwenye mashtaka ya uzushi.

49. Katika miaka iliyofuata, Theolojia ya Luther iliendelea haraka na kuleta mada mpya za mabishano. Huyu mtheolojia aliyeshtakiwa alifanya kazi ya kutetea msimamo wake na kuwapata watu wanaounga mkono katika mgogoro kati yake na hao, ambao walikuwa tayari kumhukumu kuwa mzushi. Maandiko mengi yalitolewa, yaliyomkubali na kumpinga Luther. Lakini yalikuwapo majadiliano ya mara moja tu, mwaka 1519, kule Leipzig kati ya Andreas Bodenstein wa Karlstadt na Luther kwa upande moja, na Johannes Eck, kwa upande mwingine.

## Hukumu ya Martin Luther

50. Wakati ule ule kule Rumi, mchakato dhidi ya Luther uliendelea. Mwishoni, Papa Leo X aliamua kuchukua hatua. Ili aweze kutimiza wajibu wa ofisi yake ya kiuchungaji, Papa Leo X aliona ilimbidi kutetea "*mafundisho sahihi"* kuwapinga "wanaopindisha na kughushi Maandiko matakatifu" mpaka "yasiwe Injili ya Kristo tena."[6] Kwa hiyo Papa alitoa azimio (bull) *Exsurge Domine* (15 Juni 1520), ambalo lilihukumu sentensi arobaini na moja zilizochukuliwa kutoka maandiko mbalimbali ya Luther. Ingawa sentensi hizi zote zipo katika

[6] Peter Fabisch and Erwin Iserloh (eds), *Exsurge Domine* in *Dokumente zur Causa Lutheri (1517-1521)*, vol. 2 (Münster: Aschendorffsche, 1991), 366; *Exsurge Domine*, DH 1467-1472, pia katika **www.ewtn.com/library/papaldoc/l10exdom.htm.**

maandiko ya Luther na zimenukuliwa kwa usahihi, zimenyofolewa kutoka mazingira ya kifungu husika. *Exsurge Domine* linaeleza sentensi hizi kuwa "uasi au za chukizo, au uongo, au zenye kuumiza masikio ya waaminio waaminifu, au kuwa hatari kwa wasiowaza kwa kina, au zenye kupindua Ukweli wa kikatoliki,"[7] bila kuelezea sentensi ipi ina ubaya upi. Mwishoni mwa azimio hili, Papa alionesha kukata tamaa juu ya hali halisi kwamba Luther alishindwa kutoa itikio lolote kwa majadiliano. Ingawa, alibaki kwenye matumaini kwamba Luther atafanya mageuzi moyoni na kuacha makosa yake. Papa Leo alimpa Luther siku sitini ama kufuta "makosa" yake au kukabili kutengwa na kanisa.

51. Eck na Aleander, ambao walichapisha *Exsurge Domine* kule Ujerumani walitoa wito wa maandiko ya Luther kuchomwa moto. Katika kuitikia jambo hili, tarehe 10 Desemba 1520, Watheolojia wachache wa Wittenberg walichoma vitabu mbalimbali, ambavyo baadaye vingeweza kujulikana kama vitabu vya sheria ya kanisa. Sambamba na hivyo vilichomwa pia vitabu vya wapinzani wa Luther, na Luther alichoma amri ya papa katika moto ule. Kwa hiyo ilikuwa wazi, kwamba Luther hakuwa tayari kufuta maoni yake. Luther alitengwa na Kanisa kwa njia ya amri ya Papa *Decet Romanum Pontificem* tarehe 3 Januari, 1521.

## Mamlaka ya Maandiko Matakatifu

52. Ugomvi juu ya vyeti vya msamaha uligeuka kuwa ugomvi juu ya mamlaka. Kwa Luther, uongozi wa Kanisa la Rumi ulikuwa umepoteza mamlaka yake kwa njia ya kung'ang'ania mamlaka yake badala ya kujadiliana kibiblia. Mwanzoni mwa ugomvi huu, Theolojia yenye nguvu katika msingi wa Maandiko Matakatifu, Mababa wa Kanisa, na mapokeo ya kanuni vilikuwa na umoja kwa Luther. Ugomvi ulipoendelea, umoja huu ulivunjika wakati Luther akihitimisha,

---

[7] Ibid., 368.

kwamba kwa namna kanuni zilivyowakilishwa na wenye madaraka wa Rumi, zinapingana na Biblia. Kwa Upande wa Kanisa Katoliki, hawakupinga sana kwamba Biblia ina mamlaka ya juu kabisa, (msimamo huu wamekubali), lakini walihangaika kuelewa tafsiri sahihi ya Maandiko (Biblia)

53. Luther akiwa hajaona msingi wa Biblia katika kauli za viongozi wa Kanisa la Rumi, au hata alipoona wanapinga ujumbe wa Biblia, alianza kumtazama Papa kama Mpinga Kristo. Madai haya bila shaka yanatisha. Kwa madai haya Luther alipenda kusema, kwamba Papa hakumruhusu Kristo kusema ambayo alipenda kusema, na pia kwamba Papa alijiweka juu ya Biblia badala ya kujiweka chini ya mamlaka ya Biblia. Papa alidai kwamba ofisi yake ilianzishwa *iure divino* ("kwa haki ya kimungu"), wakati Luther hakuweza kuona ushahidi wa kibiblia kwa madai haya.

## Luther Akiwa Worms

54. Kufuatana na sheria za milki Takatifu ya Kirumi katika Ujerumani, mtu ambaye alitengwa na kanisa vile vile alipoteza haki ya kibinadamu (imperial ban). Hata hivyo, wajumbe wa mkutano wa kanisa la Worms walidai, kwamba mamlaka, ambayo inajitegemea, imhoji Luther. Kwa hiyo, Luther aliitwa kufika Worms. Wakati alipoitwa, tayari alikuwa amehesabiwa kuwa ni mzushi. Hata hivyo Kaisari alimwahidi Luther, kumpa usafiri salama mpaka mji ule. Luther alikwenda kwenye mkutano huo akitegemea kuwepo kwa majadiliano kwenye mkutano. Badala yake alipofika aliulizwa moja kwa moja, bila nafasi ya kujieleza, kama ni yeye alikuwa ameandika vitabu vilivyokuwa mezani mbele yake, na pia kama yuko tayari kufuta maoni yake.

55. Luther alijibu swali hilo kwa maneno haya ambayo yalifahamika sana: "Isipokuwa nimeridhishwa na ushuhuda wa Maandiko Matakatifu au na hoja ya kweli (kwa sababu simwamini ama Papa au maamuzi ya mikutano peke yake, kwani tunajua kwamba wamekosea mara nyingi na pia wanapingana wenyewe), nimefungwa na Maandiko

Matakatifu niliyonukuu, na dhamiri yangu imefungwa na maneno ya Mungu. Siwezi na sifuti kitu chochote, kwani sio salama wala sio sahihi kupingana na dhamiri yangu. Mungu anisaidie. Amina."[8]

56. Katika kuitikia, Mtawala Charles V alitoa hotuba ya pekee kuonesha makusudi yake. Huyu mtawala alitaja kwamba yeye ni mrithi katika mstari mrefu wa watawala, ambao wote walijiona kuwa na wajibu wa kutetea imani ya Kikatoliki "kwa ukombozi wa nafsi za binadamu" na aliona yeye pia alikuwa na wajibu ule ule. Mtawala alitoa hoja yake kwamba mtawa mmoja alikosea wakati maoni yake yalipopingana na mafundisho yote ya Ukristo wa miaka elfu iliopita.[9]

57. Mkutano mkuu wa Worms ulimwona Luther kuwa mhalifu ambaye lazima akamatwe hata auawe na uliwaagiza Viongozi kukandamiza "uasi wa Luther" kwa njia yoyote. Kwa sababu hoja za Luther ziliwaridhisha wana wa wafalme (princes) na watu wengi wa mijini, hawakutekeleza amri hii.

## Mwanzo wa Vuguvugu la Matengenezo

58. Ufahamu wa Luther juu ya Injili uliendelea kuwaridhisha baadhi ya mapadre, watawa na wahubiri, na idadi yao iliongezeka kila siku. Hao walijitahidi kuingiza ufahamu huu katika mahubiri yao. Alama za mabadiliko zilianza kuonekana kama vile wakati wa Meza ya Bwana. Wakristo wa kawaida waliweza kupokea mkate na divai, sio mkate tu. Tena Mapadre na watawa wachache walifunga ndoa.

[8] Luther, "Luther at the Diet of Worms," tr. Roger A. Hornsby, in *LW* 32:112–3. Kwa "Words" badala ya Word, ona *WA* 8, 838, 7; kwa kuondolewa kwa "I Cannot do Otherwise, Here I stand" (cf. *WA* 8, 838, 9), ona 113, n. 2: "Maneno haya yametolewa katika Kijerumani katika maandishi ya Kilatini ambayo tafsiri hii inategemea," lakini "kuna uthibitisho mzuri" kwamba Luther hakuyasema.

[9] Fritz Reuter (ed.), *Der Reichstag zu Worms von 1521: Reichspolitik und Luthersache,* vol. 2 (Köln and Wien: Böhlau, 1981), 226–29; tazama pia *LW* 32, 114–15, n. 9.

Waliacha sheria mbalimbali za kufunga. Na mara kwa mara waliacha kuheshimu picha takatifu au masalio ya watakatifu.

59. Luther hakuwa na makusudi ya kuanzisha kanisa jipya, lakini alikuwa na hamu kubwa ya kufanya matengenezo ya kanisa. Aliendelea kuongeza nguvu yake kujaribu kuchangia kwa kupata matengenezo ya utekelezaji na kanuni, ambazo zilionekana kutegemea mamlaka ya kibinadamu tu, na sio kufaa au kufuata mafundisho ya Maandiko Matakatifu. Katika andiko lake "To the German Nobility" (1520), Luther alitetea ukuhani wa wote waliobatizwa. Kwa hiyo alidai Wakristo wa kawaida wapate nafasi ya kushiriki kwenye matengenezo ya Kanisa. Wakristo wa kawaida walishiriki nafasi muhimu katika Matengenezo, wakiwa ama ni wana wa wafalme, hakimu, au watu wa kawaida.

## Mahitaji ya Usimamizi

60. Kwa vile haukuwepo mpango maalum wala usimamizi wa utekelezaji wa matengenezo, hali ya utekelezaji ilitofautiana kati ya mji na mji na kijiji na kijiji. Ilionekana kuna haja ya kupanga tume rasmi za kutembelea kanisa. Kwa sababu hii ilihitaji kupata ruhusa kutoka kwa watawala na mahakimu, watu walioshiriki matengenezo walimwomba mwana mfalme na mtawala wa Saxony kuunda na kuruhusu kamati ya tume mwaka 1527. Kazi ya tume hii sio tu kupima mahubiri, ibada na maisha ya wachungaji, bali pia kuhakikisha kwamba wanapata riziki yao ya kutosha.

61. Tume hii ilianzisha kitu kama serikali ya kanisa. Wasimamizi walipewa kazi ya kuwasimamia wachungaji wa eneo fulani na kusimamia mafundisho yao na mwenendo wa maisha yao. Tume pia ilipima utaratibu wa ibada na ilisimamia umoja wa taratibu hizi. Mwaka 1528, kijitabu cha maelekezo kwa wachungaji kilitolewa kuelezea matatizo yote muhimu ya kiimani na utendaji wa kila siku. Kijitabu hiki kilikuwa mchango muhimu katika historia ya ukiri wa imani ya Kilutheri.

## Kuleta Maandiko Matakatifu kwa Watu

62. Luther, pamoja na wenzake katika chuo cha Wittenberg, walitafsiri Biblia katika Kijerumani, ili watu wengi zaidi waweze kusoma wenyewe na, kwa matumizi mengine, washiriki katika utambuzi wa kiroho na kitheolojia katika maisha yao ndani ya kanisa. Kwa ajili ya sababu hii, wafuasi Walutheri wa Matengenezo walianzisha shule kwa wavulana na wasichana na walijitahidi kwa nguvu kuwashawishi wazazi wawapeleke watoto wao kusoma katika shule hizo.

### *Katekisimo na Nyimbo*

63. Ili kuboresha hali duni ya imani ya Kikristo miongoni mwa wachungaji na Wakristo wa kawaida, Luther aliandika Katekisimo ndogo kwa wasomaji wa kawaida na Katekisimo kubwa kwa wachungaji na Wakristo wa kawaida wenye elimu kubwa. Katekisimo hizi zilieleza Amri Kumi, Sala ya Bwana, na Kiri za imani. Tena zilikuwa na maelezo juu ya Ubatizo mtakatifu na Chakula cha Bwana. Katekisimo ndogo ilikuwa na ushawishi wa pekee kubadilisha elimu za watu. Hii ilisaidia sana kuongeza elimu juu ya imani ya watu wa kawaida.

64. Katekisimo hizi zilikusudia kuwasaidia watu kuishi maisha ya Kikristo na kuwawezesha kuwa na uwezo wa utambuzi kitheolojia na kiroho. Katekisimo hizi zinaelezea kwa mifano, kwamba kwa washiriki wa matengenezo, imani sio kumwamini Kristo tu na ahadi yake, lakini pia lazima kukubali yaliyomo katika imani ambayo waamini wanaweza na lazima wajifunze.

65. Ili kuwawezesha Wakristo wa kawaida washiriki kwenye ibada, wafuasi wa matengenezo walitunga nyimbo na walitoa vitabu vya nyimbo hizo. Vitabu hivi vilisaidia maisha ya kiroho ya Kilutheri kusonga mbele sana na zikaja kuwa ni urithi wa thamani sana kwa kanisa zima.

### *Upatikanaji wa Wachungaji wa Sharika*

66. Sasa wakati sharika za Kilutheri zilikuwa na Maandiko Matakatifu katika lugha ya wenyeji, tena Katekisimo, nyimbo, utaratibu wa kanisa na taratibu za ibada. Bado changamoto kubwa ilibakia, yaani namna ya kuandaa wachungaji wa kutumika katika sharika. Kwenye miaka ya kwanza ya matengenezo mapadre na watawa wengi waligeuka kuwa wachungaji wa Kilutheri. Kwa hiyo wachungaji wa kutosha walipatikana. Lakini mbinu hii ya kupata wachungaji hatimaye ilionekana kuwa na upungufu.

67. Ni ajabu kwamba wafuasi wa matengenezo walisubiri mpaka mwaka 1535 kabla hawajapanga ubarikio wa wachungaji wao wenyewe katika Wittenberg. Katika Ungamo la Augsburg (1530), wafuasi wa matengenezo walitangaza kwamba wako tayari kuwatii Maaskofu kama Maaskofu wenyewe wangewaruhusu kuhubiri Injili kufuata imani ya matengenezo. Kwa sababu mambo haya hayakufanikiwa, iliwabidi wachague kati ya njia ya kubaki kwenye mapokeo ya Maaskofu kuwabariki wachungaji, na kwa njia hii kuacha kuhubiri kimatengenezo, au - kubaki na mahubiri ya kimatengenezo, lakini kujitegemea kwenye kubariki wachungaji kwa msaada wa wachungaji wengine. Wafuasi wa matengenezo walichagua njia ya pili, wakirejea mapokeo ya ufahamu wa Nyaraka za Kichungaji kurejea maelezo ya Hieronymus (Jerome) wa Kanisa la mwanzo.

68. Wana jumuiya wa kitivo cha kitheolojia cha Wittenberg, wakifanya kwa niaba ya kanisa, walipima elimu ya imani na maisha ya watahiniwa. Kisha ubarikio ulikuwa ukifanyika Wittenberg badala ya kufanyikia katika sharika za watahiniwa, kwani wachungaji walibarikiwa kutumikia kanisa zima. Vyeti vya ubarikio vilikaza kukubaliana na mafundisho ya kanisa Katoliki. Kanuni ya utekelezaji wa ubarikio ilikuwa kumwekea mikono na kuomba kwa Roho Mtakatifu.

## Jitihada ya Kitheolojia ya Kukabiliana na Ugomvi wa Kimadhehebu

69. Ungamo la Augsburg (1530) lilijitahidi kutatua ugomvi wa kidini uliotokana na matengenezo ya Kilutheri. Sehemu yake ya kwanza (vipengele 1–21) inawakilisha mafundisho ya Kilutheri yenye kukubaliana na kanuni za "kanisa Katoliki".[10] Sehemu yake ya pili inashughulika na mabadiliko ambayo wafuasi wa matengenezo walianzisha ili kurekebisha mambo fulani ambayo utekelezaji wake ulionekana kuwa unatumiwa vibaya (vipengele 22–28). Pia sehemu hii inatoa sababu za kubadilisha hali hiyo. Mwishoni mwa sehemu ya kwanza inasema, "Huu ni kama muhtasari wa mafundisho yetu. Kama inavyoonekana, hatuna jambo lolote linalopingana na Biblia au na Kanisa la Kirumi, kulingana na waandishi wake. Kutokana na haya, wale wanaowahukumu watu wetu kuwa ni wazushi, hao wanahukumu vikali mno."[11]

70. Ungamo la Augsburg ni ushuhuda wa nguvu wa kuonesha ushupavu wa wafuasi wa matengenezo wa Kilutheri kutunza umoja wa kanisa na kubaki pamoja kwenye kanisa lile moja na linaloonekana. Kwa njia ya kuonesha bayana kwamba tofauti sio kubwa na muhimu kuliko mambo ya pamoja, ungamo hili linafanana na kile ambacho leo tungekiita "makubaliano yanayoainisha tofauti" (differentiating consensus).

71. Mara moja Watheolojia wachache wa Katoliki waliona haja kuitikia ungamo hili la Augsburg. Kwa haraka walitunga andiko lililoitwa Confutatio, ili kukanusha Ungamo la Augsburg. Confutatio hili lilifuata kwa karibu sana maandiko na hoja za Ungamo. Kwa sehemu Confutatio liliweza kukubaliana na Ungamo la Augsburg juu

[10] "The Augsburg Confession," Andiko la Kilatini, katika Robert Kolb and Timothy J. Wengert (eds), *The Book of Concord: The Confessions of the Evangelical Lutheran Church* (Minneapolis, MN: Fortress, 2000), 59.

[11] CONCORDIA, Kitabu Kidogo cha Umoja wa Imani, Mafundisho na Ukiri wa Kilutheri, Fasihi Bora ya Urithi wa Imani ya Kilutheri 3, KKKT/ELCT 2000, uk. 51

ya mafundisho mbalimbali ya msingi ya Kikristo, kama kanuni ya utatu, Kristo, na Ubatizo. Lakini Confutatio lilikataa baadhi ya mafundisho ya Kilutheri juu ya mafundisho ya kanisa na sakramenti, kwa kuzingatia maneno ya Biblia na ya maandiko ya mababa wa kanisa. Kwa sababu Walutheri hawakuweza kushawishiwa na hoja za Confutatio, mawasiliano rasmi yalianzishwa mwisho wa mwezi wa Agosti mwaka 1530, ili kupatana juu ya tofauti za mawazo kati ya Ungamo na Confutatio. Lakini mawasiliano haya hayakufanikiwa kutatua matatizo ya kikanisa na kisakramenti yaliyobaki.

72. Jaribio jingine la kumaliza ugomvi huu wa kidini lilikuwa ni lile la kitu kilichoitwa *Religionsgespräche (mawasiliano ya dini)* au Colloquies (majadiliano ili kubainisha ukweli) (Speyer/Hagenau [1540], Worms [1540-1], Regensburg [1541–1546]). Mtawala au ndugu yake, Mfalme Ferdinand, aliitisha mazungumzo, ambayo yalifanyika chini ya uongozi wa mwakilishi wa mtawala mwenyewe. Lengo lilikuwa kuwashawishi Walutheri kurudi katika misimamo ya wapinzani wao. Njama, fitina na shinikizo za kisiasa zilichukua sehemu muhimu kati ya mawasiliano haya.

73. Wapatanishi walifanikiwa kuandika maandiko ya pekee juu ya kanuni ya kuhesabiwa haki katika kitabu cha Regensburg (*Regensburger Buch,* 1541). Lakini ugomvi juu ya kanuni ya Chakula cha Bwana ulionekana kuwa usioweza kutatuliwa. Mwishoni, pande zote mbili, upande wa Rumi na upande wa Luther, walikataa matokeo yote. Hii ilikuwa alama ya kushindikana kwa majadiliano haya.

### *Vita vya Kidini na Amani ya Augsburg*

74. Vita ya Smalcald (1546–1547) ya mtawala Charles V dhidi ya maeneo ya Kilutheri ilikusudia kuwashinda wana wa wafalme na kuwalazimisha kubatilisha mabadiliko yote. Mwanzoni huyu mtawala alifanikiwa. Alishinda vita hii. (20 Juli 1547). Majeshi yake yalifika Wittenberg baada ya muda mfupi, ambapo mtawala aliwazuia maaskari kufukua maiti ya Luther na kuichoma.

75. Kwenye Mkutano Mkuu wa Augsburg (1547–1548), mtawala aliingiza jambo lililoitwa 'Augsburger Interim' juu ya Walutheri. Hii ilikuwa hati ambayo ilileta ugomvi usiokoma katika maeneo ya Kilutheri. Hati hii ilieleza kwamba kuhesabiwa haki kwa sehemu kubwa ni juu ya neema inayoamsha upendo. Ilikaza wajibu wa kujiweka chini ya Maaskofu na Papa. Lakini hata hivyo iliruhusu kufunga ndoa kwa mapadre na kupokea Chakula cha Bwana kwa kupata mkate na divai.

76. Mwaka 1552, baada ya njama ya wana wa wafalme, vita mpya ilianza dhidi ya mfalme mkuu ambapo ilimlazimisha kukimbia kutoka Austria. Hii ilipelekea kupata mkataba wa amani kati ya Wana wa Wafalme wa Kilutheri na Mfalme Ferdinand. Kwa hiyo, jaribio la kuangamiza "uasi wa Kilutheri" kwa njia ya kijeshi mwishoni lilishindwa.

77. Vita ilikwisha na amani ya Augsburg ilipatikana mwaka 1555. Mkataba huu ilikuwa jaribio la kutafuta njia kwa watu wa imani ya dini tofauti kuishi pamoja kwenye nchi moja. Maeneo na miji ambayo yalizingatia Ungamo la Augsburg pia maeneo ya Kikatoliki yalitambuliwa katika milki ya Kijerumani, lakini sio watu wa imani nyingine kama Wareformed (Wa-Calvinisti) au waliobatiza mara mbili (Anabaptists). Wana wa wafalme (Princes; *maelezo ya wafasiri: walikuwa na nguvu kama chief*) na mahakimu walikuwa na haki kuamua dini ya wananchi wao. Kama mwana wa mfalme angebadilisha dini yake, iliwabidi wananchi, walioishi katika eneo lake, wabadilishe pia dini zao, ila katika maeneo ambapo maaskofu walikuwa wana wa wafalme (*geistliche Fürstentümer – mikoa ya kiroho*). Wananchi walikuwa na haki kuhama kama hawakukubaliana na dini ya mwana mfalme.

## *Mkutano Mkuu wa Trent*

78. Mkutano Mkuu wa Trent (1545–1563), uliitishwa baada ya kizazi kimoja cha matengenezo ya Luther. Ulianza kabla ya vita ya Smalcald (1546–1547) na ulimalizika baada ya amani ya Augsburg (1555). Amri ya Papa inayojulikana kama *Laetare Jerusalem* (19 Novemba 1544) iliweka maagizo matatu ya shughuli kwenye ajenda ya mkutano: Kuponya ufa wa kimadhehebu; kurekebisha kanisa; na kuunda

amani, ili kuimarisha ulinzi dhidi ya wana wa Ottomani (*maelezo ya mfasiri: Ni Waturuki)*.

79. Mkutano Mkuu uliamua, kwa kila kipindi cha mkutano huu kuwepo na mafundisho fulani kuhusu elimu ya imani, ili kuimarisha imani ya kanisa. Tena kuwepo na mafundisho kuhusu nidhamu, ili kusaidia kurekebisha kanisa. Kwa sehemu kubwa mafundisho ya elimu ya imani hayakuleta picha ya mafundisho yote ya kitheolojia juu ya imani. Badala yake walisisitiza yale mafundisho ambayo yalipingwa na Walutheri (Wana-Matengenezo) kwa namna ambayo iliweka mkazo katika maeneo ambayo (Wakatoliki na Walutheri) waliotofautiana.

**Fundisho la Kwanza: Maandiko Matakatifu na Mapokeo**

80. Mkutano Mkuu, tarehe 8 Aprili 1546, katika kutaka kutunza "usafi wa Injili baada ya kuondoa makosa yote," ulipitisha amri yake juu ya vyanzo vya ufunuo wa Mungu. Bila kutaja bayana, katika amri hii ulikataa kanuni ya *sola scriptura (Neno tu)* kwa njia ya kukataa maandiko kutenganishwa na mapokeo. (*Maelezo ya wafasiri: Maana yake, walisema, ufunuo wa Mungu hautokei kutoka Biblia tu, bali pia unatokea kutoka maandiko ya mababa wa Kanisa.)* Mkutano mkuu uliazimia kwamba Injili, "chanzo cha ukweli wote wa ukombozi na mafundisho ya maadili," imetunzwa "katika vitabu vilivyoandikwa na katika mapokeo ambayo hayakuandikwa,". Lakini ulikiri hivyo bila kueleza namna ya uhusiano wa Biblia na mapokeo. Aidha, ulifundisha kwamba mapokeo ya mitume yanayohusu imani na maadili "yametunzwa katika kanisa Kikatoliki kwenye mfululizo usiovunjika katika kanisa katoliki." Inabidi maandiko na mapokeo yapokelewe "katika tabia ya uchaji wa Mungu na heshima."[12]

81. Azimio hili lilitoa orodha ya vitabu kikanuni vya Agano la Kale na Agano Jipya.[13] Mkutano mkuu ulisisitiza kwamba haiwezekani

[12] Council of Trent, Fourth Session, 8 April 1546, Decree Concerning the Canonical Scriptures.

[13] Ibid.

kufafanua Maandiko Matakatifu kinyume cha mafundisho ya kanisa wala kinyume cha "mafundisho ya kauli moja ya Mababa" wa Kanisa. Hatimaye, Mkutano mkuu ulitangaza kwamba toleo la zamani la Kilatini la Biblia (Vulgata) ni matini (text) "halisi" kwa matumizi katika kanisa.[14]

**Fundisho la Pili: Kuhesabiwa Haki**

82. Kuhusu kuhesabiwa haki, Mkutano mkuu huu ulikataa waziwazi misimamo yote miwili: Msimamo wa kwanza ni kanuni ya kipelagio ya kuhesabiwa haki kwa njia ya matendo mema; Msimamo wa pili ni kanuni ya kuhesabiwa haki kwa imani tu (*sola fide*); Badala yake walieleza kuwa kimsingi imani ni ukubali wa mafundisho yaliyofunuliwa. Mkutano mkuu ulithibitisha msingi wa kuhusika kwa Kristo katika kuhesabiwa haki kwa njia ya kuhakikisha kwamba binadamu wameunganishwa ndani ya Kristo. Kwa msingi neema ya Kristo ni lazima katika mchakato mzima wa wokovu. Hata hivyo mchakato huu hauondoi tabia ya mwanadamu kuhusu neema au kuhusika kwa dhamiri huru. Ulitangaza, kwamba nafsi ya kuhesabiwa haki sio ondoleo la dhambi tu, lakini pia ni "kuweka nafsi ya mtu kuwa takatifu na mpya" kwa njia ya upendo upitao kupita akili.[15] Kimsingi kuhesabiwa haki ni "haki ya Mungu, sio haki ambayo inamfanya Mungu kuwa mwenye haki, lakini haki hii ambayo anatufanyia kuwa wenye haki." Na makusudi ya kuwahesabia binadamu haki ni "sifa kuu ya Mungu na Kristo na uzima wa milele."[16] Walithibitisha kwenye mkutano mkuu huu, kwamba imani ni "mwanzo, msingi na mizizi" ya kuhesabiwa haki.[17] Neema ya kuhesabiwa haki inaweza kupotezwa kwa dhambi ya mauti, na wala sio kwa kupoteza imani tu, ingawa

[14] Ibid., Decree Concerning the Edition and Use of the Sacred Books.

[15] Council of Trent, Sixth Session, 13, January 1547, sura ya VII.

[16] Ibid.

[17] Ibid., sura ya VIII.

inaweza kupatikana tena kwa njia ya sakramenti ya toba.[18] Mkutano mkuu ulithibitisha kwamba uzima wa milele ni neema, sio tuzo tu.[19]

### Fundisho la Tatu: Sakramenti

83. Kwenye kikao cha saba, Mkutano mkuu huu ulieleza kwamba sakramenti ni njia za kawaida ambapo "haki zote za kweli ama huanza au, kama zimekwisha kupokelewa zinapata nguvu, au ikiwa zimepotea, zinarejezwa tena."[20] Mkutano mkuu huu ulitangaza kwamba Kristo alianzisha sakramenti saba na mkutano ulizielezea kama alama zenye kufanya kazi, ambazo zinasababisha neema kwenye utekelezaji huo (*ex opere operato)* na sio kwa sababu ya imani ya mpokeaji.

84. Majadiliano juu ya kushirikiana Chakula cha Bwana katika kupokea mkate na divai yalionesha mafundisho ya kusema kwenye kila sura peke yake (kama ni mkate au kama ni divai) unapokea Kristo kamili pasipo kugawanyika. [21] Baada ya kuhitimisha mkutano huu (16 Aprili 1565), Papa aliruhusu kikombe cha divai kupokelewa na Wakristo wa kawaida, wakizingatia masharti fulani kwa majimbo ya Kanisa mbalimbali ya Ujerumani tena kwa maeneo ya urithi wa Habsburg.

85. Katika kujibu ukosoaji wa Wafuasi wa matengenezo kuhusu misa kuwa na sifa ya dhabihu, Mkutano mkuu ulisisitiza kwamba misa ni dhabihu ya kufidia makosa, ambayo inaifanya dhabihu ya msalaba kuwa tendo la sasa. Tena Mkutano mkuu ulifundisha kwamba, katika misa kuhani anatoa vyombo vya kidhabihu kama msalabani, lakini kwa namna nyingine. Kwa hiyo misa sio marudio ya dhabihu

[18] Ibid., sura ya XIV-XV.

[19] Ibid., sura ya XVI.

[20] Council of Trent, Seventh Session, 3 March 1547, Foreword.

[21] Council of Trent, Twenty-first Session, 16 July 1562, Sura ya III, can. 2.

ya pekee na kamili ya Kalvari. Pia Mkutano mkuu ulieleza kwamba misa inaweza kutolewa kuheshimu watakatifu na pia kwa waaminio, ambao ni hai au waliokufa.[22]

86. Kanuni kuhusu kuwekwa wakfu ilifafanua sifa za kisakramenti za wakfu na uwezo wa uongozi (kikanisa) uliojengwa katika maagizo ya Mungu.[23]

**Fundisho la Nne: Matengenezo ya kiuchungaji**

87. Mkutano mkuu huu pia ulianzisha mpango wa uboreshaji wa huduma ya kiuchungaji. Lengo la mpango huu lilikuwa kupata mahubiri yenye kufanya kazi zaidi kwa njia ya kuunda vyuo mbalimbali ili mapadri waelimishwe vizuri na kuwadai wahubiri kila Jumapili na kila sikukuu. Iliwabidi Maaskofu na Wachungaji wakae katika Dayosisi au sharika zao. Mkutano mkuu ulifuta matumizi mabaya mbalimbali kwenye mambo ya mamlaka ya kisheria, ubarikio, uangalizi, maslahi, na vyeti vya msamaha. Wakati huo huo ulipanua mamlaka ya askofu. Maaskofu waliwezeshwa kutembelea parokia tena kusimamia kazi ya kiuchungaji ya vituo vya Watawa vilivyoruhusiwa na mambo mbalimbali. Ulifadhili mikutano ya sinodi ya majimbo na ya Dayosisi. Ili kuimarisha mawasiliano juu ya imani, Mkutano mkuu huu uliwatia moyo waandishi waliojitokeza kutunga Katekisimo, kama zile za Petro wa Canisius. Tena ulianzisha maandalizi ya kuandika Katekisimo ya Kirumi.

**Matokeo**

88. Ingawa Mkutano mkuu wa Trent ulikuwa itikio kwa kiasi kikubwa kuhusu Matengenezo ya Kiprotestanti, haukuhukumu mtu mmoja mmoja au jumuiya lakini misimamo ya kanuni fulani. Kwa sababu kanuni za Mkutano mkuu kwa kiasi kikubwa zilikuwa itikio kwa

[22] Council of Trent, Twenty-second Session, 17 September 1562, Sura ya II, can. 3.

[23] Council of Trent, Twenty-third Session, 15 July 1563, Sura za III na IV.

mambo ambayo walifikiri ni makosa ya Waprotestanti, mkutano mkuu huu ulitengeneza mazingira ya mabishano kati ya Waprotestanti na Wakatoliki ambayo yalielekea kueleza Ukatoliki zaidi dhidi ya Uprotestanti. Kwenye msimamo huu ilikuwa kama kioo cha Maandiko ya Ukiri wa Kilutheri, ambayo yalieleza msimamo wa Kilutheri kwa njia ya kuonesha upinzani tu. Maamuzi ya Mkutano mkuu wa Trent yaliweka msingi kwa kuendeleza utambulisho wa Kikatoliki mpaka Mtaguso wa Pili wa Vatikani.

89. Mwishoni mwa kusanyiko la tatu la Mkutano mkuu wa Trent, ilibidi ikubalike kwamba umoja wa kanisa la magharibi ulikuwa umevunjika. Katika maeneo ya Kilutheri miundo mipya ya Kanisa ilikuwa imetokea. Amani ya Augsburg ya 1555 mwanzoni ilileta uhusiano imara wa kisiasa, lakini haikuweza kuzuia ugomvi mkubwa wa Ulaya katika karne ya kumi na saba, Vita ya Miaka Thelathini (1618–1648). Kuanzishwa kwa mataifa ulimwenguni yenye mipaka madhubuti ya kimadhehebu kulibaki kuwa mzigo, uliorithiwa kutoka kipindi cha matengenezo.

### *Mtaguso wa Pili wa Vatikani*

90. Wakati Mkutano mkuu wa Trent ulitawala kwa kiasi kikubwa uhusiano wa Wakatoliki na Walutheri kwa karne kadhaa, lazima tuone urithi wake kupitia mtazamo wa maamuzi ya Mtaguso wa Pili wa Vatikani (1962–1965). Mtaguso huu uliwezesha Kanisa la Katoliki kujiunga na ekumeni na kuacha mazingira mabaya ya mabishano ya kipindi kilichofuata matengenezo. Kanuni ya mafundisho kuhusu Kanisa (*Lumen Gentium*), Kanuni ya ekumeni (*Unitatis Redintegratio*), Tangazo juu ya uhuru wa dini (*Dignitate Humanae*), na Katiba ya Kanuni juu ya Ufunuo wa kimungu (*Dei Verbum*) ni maandiko ya msingi kwa ekumeni ya Kikatoliki. Mtaguso wa Pili (Vatikani II), hali ukithibitisha kwamba Kanisa la Kristo linaishi katika Kanisa la Katoliki, pia ulikiri kuwa, “alama nyingi za utakaso na za ukweli zinaonekana nje ya muundo wake wa Katoliki unauonekana. Alama hizi, kama vipawa vya Kanisa la Kristo vinachochea umoja wa Kikatoliki” (*LG* 8). Mtaguso huu uliheshimu sana mambo ambayo

Wakatoliki wanashirikiana na Wakristo wengine kama kiri za imani, Ubatizo, na Maandiko matakatifu. Katika mwanga wa theolojia ya Ushirikiano kimakanisa, walikaza kwamba Wakatoliki wanakaa katika ushirikiano wa kweli, hata kama sio kamili, pamoja na wote wanaomkiri Yesu Kristo na wamebatizwa (*UR* 2).

# Mlango wa IV

## Mada Kuu za Theolojia ya Martin Luther Katika Mtazamo wa Majadiliano kati ya Walutheri na Kanisa la Rumi

91. Tangu karne ya kumi na sita, misimamo mikuu ya Martin Luther pamoja na Theolojia ya Kilutheri ni jambo ambalo limeleta mvutano kati ya Walutheri na Wakatoliki. Majadiliano ya kiekumeni na tafiti za kitaaluma zimechambua malumbano haya na kujaribu kuyatatua kwa kuainisha misamiati mbalimbali, sura mbalimbali za mitizamo na haja (concerns) mbalimbali ambazo sio lazima zikinzane.

92. Katika sura hii, Walutheri na Wakatoliki kwa pamoja wanawasilisha baadhi ya fikra kuu za kitheolojia alizoziratibisha Luther. Haya maelezo ya pamoja hayamaanishi kuwa Wakatoliki wanakubaliana na kila alichokisema Martin Luther kama kilivyowasilishwa hapa. Hitaji endelevu la majadiliano ya kiekumeni na maridhiano bado vinahitajika. Hata hivyo, tumefikia hatua katika safari ya kiekumeni inayotusaidia kuwa na andiko hili la pamoja.

93. Ni muhimu kutofautisha kati ya theolojia ya Luther na theolojia ya Kilutheri, zaidi sana kati ya theolojia ya Luther na fundisho la makanisa ya Kilutheri kama linavyoelezwa katika maandiko ya kiri zao. Fundisho hili ni rejeo la majadiliano ya kiekumeni. Lakini ni sahihi hapa kujikita zaidi kwenye theolojia ya Luther kwa ajili ya maadhimisho yake ya 31 Oktoba 1517.

### Umbile la Mlango wa IV

94. Sura hii inasimamia mada nne tu katika Theolojia ya Luther: Kuhesabiwa haki, Ekaristi, Huduma na Maandiko na Mapokeo. Kwa sababu ya umuhimu wa mada hizo katika maisha ya Kanisa, na

kwa sababu ya mvutano iliyotokea kwa karne kadhaa, zimejadiliwa kwa kina katika majadiliano ya Walutheri na Wakatoliki. Maelezo yanayofuata ni matokeo ya majadiliano haya.

95. Majadiliano ya kila mada yaliendelea katika hatua tatu. Mtazamo wa Luther kwa kila mojawapo ya hizo mada nne uliwasilishwa kwanza, na kufuatiwa na maelezo kwa kifupi ya Wakatoliki kuhusiana na mada husika. Ndipo jumuisho likionesha jinsi theolojia ya Luther imewekwa katika mtafaruku na fundisho la Kikatoliki katika majadiliano ya kiekumeni. Sura hii itaainisha yale yaliyoafikiwa na kuweka wazi tofauti zilizobakia.

96. Mada muhimu kwa ajili ya majadiliano ya mbeleni ni jinsi gani tunaweza kukaribiana zaidi katika mambo yote ambapo bado tuna mikazo tofauti hususan kuzingatia fundisho la Kanisa.

97. Ni muhimu kukumbuka kuwa sio maazimio yote ya majadiliano kati ya Walutheri na Wakatoliki inabeba uzito sawa wa maridhiano, wala sio yote imepokelewa katika hali sawa na Walutheri na Wakatoliki. Upeo wa juu wa mamlaka umeegemea kwenye *Azimio la Pamoja la Fundisho la Kuhesabiwa Haki* (*Joint Declaration on the Doctrine of Justification*) lililotiwa sahihi na wawakilishi wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (LWF) na Kanisa la Kikatoliki huko Augsburg, Ujerumani, tarehe 31 Oktoba 1999 na kukubaliwa na Fungamano la Makanisa ya Kimethodisti Duniani mwaka 2006. Bodi za udhamini zimepokea taarifa ya majadiliano ya tume nyingine za kimataifa na kitaifa. Lakini hizi taarifa zinatofautiana katika umuhimu wake katika theolojia na maisha ya jumuiya za Kilutheri na Kikatoliki. Kwa sasa viongozi wa Makanisa wanashirikiana wajibu unaoendelea kwa kuthamini na kupokea kukamilika kwa majadilino ya kiekumeni.

## Urithi wa Martin Luther Kutoka Karne za Katikati

98. Martin Luther alijikita katika mitazamo ya mwishoni ya miaka ya kati. Luther angeliweza kwa wakati fulani kukubaliana nayo, kupingana

nayo kwa mbali au kuwa kwenye mchakato wa kwenda mbele zaidi ya theolojia ya kipindi hiki. Mwaka 1505, Luther alikuwa mtawa wa nyumba ya watawa ya Augustino iliyopo Erfurt, na mwaka 1512, alikuwa profesa wa theolojia huko Wittenberg. Katika nafasi hii, Luther katika kazi yake ya theolojia aliweka kipaumbele kwenye mafafanuzi ya vifungu vya Biblia. Mkazo huu juu ya Maandiko Matakatifu ulikubaliana na taratibu za yale waliotegemewa watawa kufanya katika nyumba ya Augustino. Taratibu hii ni kujifunza na kutafakari Biblia, si tu kwa faida binafsi, bali pia kwa faida ya kiroho kwa ajili ya wengine. Maandiko ya Mababa wa kanisa, hususan maandiko ya Augustino, yalitoa mchango mkubwa katika kuendeleza na kukamilisha sura ya mwisho ya theolojia ya Luther. "Theolojia yetu na Mtakatifu Augustino zinasonga mbele vizuri"[1], aliandika mwaka 1517. Pia katika Malumbano ya Heidelberg 1518 anarejea "Mtakatifu Augustino kuwa mfafanuzi mwaminifu kupita wote"[2] wa mtume Paulo. Hivyo inaonekana Luther alijikita kwenye mizizi ya mapokeo ya Mababa wa Kanisa,.

## Theolojia ya Utawa na Theolojia ya Kisirisiri (Monastic and Mystical Theology)

99. Wakati Luther alikuwa na mtizamo wa ukosoaji dhidi ya theolojia ya Waskolastika, kama mtawa wa ki-Augustino kwa miaka ishirini, aliishi, aliwaza, na kufanya theolojia katika mapokeo ya theolojia ya watawa. Mmoja kati ya washawishi wakuu wa theolojia ya utawa alikuwa Bernard wa Clairvaux, ambaye Luther alimheshimu sana. Njia ya Luther ya kufafanua "Maandiko Matakatifu" kama mahali pa kukutana kati ya Mungu na mwanadamu, inaonyesha dhahiri kuwiana na njia ya Bernard ya kufafanua "Maandiko Matakatifu".

[1] Luther, "Letter to John Lang, Wittenberg, May 18, 1517," tr. Gottfried Krodel, katika *LW* 48:44; *WAB* 1; 99, 8.

[2] Luther, 'Heidelberg Disputation," tr. Harold J. Grimm, katika *LW* 31:39; *WA* 1; 353, 14.

100. Luther alikuwa pia amejikita kwa kina katika mapokeo ya kimafumbo (mystical tradition) mwishoni mwa enzi za kati. Alipata msaada katika mahubiri ya Kijerumani ya John Tauler (†1361) na kwa njia ya kuyasoma mahubiri haya Luther alijihisi ameeleweka. Aidha, Luther mwenyewe alichapisha andiko la mafumbo, lililoitwa *Theolojia deutsch* (German Theology, 1518), ambalo lilikuwa limeandikwa na mwandishi asiyejulikana. Andiko hili lilienea na kujulikana sana kwa njia ya Luther kukichapisha kitabu hiki.

101. Kwa maisha yake yote, Luther alijisikia kuwa mwenye shukrani nyingi kwa John wa Staupitz, aliyekuwa msimamizi wa nyumba ya utawa. Theolojia ya Staupitz, ambayo kiini chake ni Kristo, ilimfariji Luther katika mahangaiko yake. Staupitz alikuwa mwakilishi wa *nuptial mysticism*, yaani kujiona kama Bibi Arusi wa Yesu Kristo. Mara kwa mara Luther alikiri ushawishi wa msaada kutoka kwa Staupitz, Luther akisema, "Staupitz alianzisha fundisho hili"[3] na akimsifu "kuwa Baba yake katika fundisho hili, na amenizaa katika Kristo"[4]. Katika miaka ya mwisho ya nyakati za kati, Theolojia iliundwa kwa ajili ya walei. Theolojia hii (*Frömmigskeitstheologie*) iliakisi maisha ya Kikristo katika hali halisi na ilikusudiwa kukaza utakatifu. Luther alihamasika na theolojia hii kuandika makala za aina yake kwa walei. Alichagua mada zao nyingi na kuzipa mkazo wake mwenyewe.

## Kuhesabiwa Haki

### *Ufahamu wa Luther Kuhusu Kuhesabiwa Haki*

102. Luther alipata mojawapo ya ufahamu wa msingi wa matengenezo kwa kutafakari sakramenti ya kitubio hususan kulingana na Matayo

[3] *WA* TR 1; 245, 12.

[4] Luther, "Letter to Elector John Frederick, March 25, 1545," iliyonukuliwa katika Heiko Obermann, *Luther: Man between God and the Devil,* tr. Eileen Walliser-Schwarzbart (New Haven & London: Yale University Press, 1989), 152; *WAB* 11, 67, 7f; *WAB* 11, 67, 7f.

16:19. Katika taaluma yake mwishoni mwa karne za katikati alijifunza kuamini, kuwa Mungu atamsamehe yule ambaye atajutia dhambi zake na kutenda tendo la kumpenda Mungu kuliko vitu vingine vyote. Kwa tendo hili Mungu ataitikia kwa kumpa mtu neema na msamaha wake kama zawadi kwa upya (*facienti quod in se est dues non denegat gratiam* [5]*), kufuata agano (pactum*), lake. Kwa hiyo kuhani angetangaza tu kuwa Mungu amesamehe dhambi tayari. Luther alihitimisha kuwa Matayo 16 inasema kinyume, kuwa kuhani anamtangazia haki mwenye dhambi atubuye, na kwa tendo hili kwa niaba ya Mungu, mwenye dhambi anahesabiwa haki.

## Neno la Mungu Kama Ahadi

103. Luther alielewa maneno ya Mungu kama maneno yanayoumba kile yanachokisema na kuwa na tabia ya ahadi (promissio). Aina hii ya neno la ahadi linasemwa mahali fulani na kwa muda maalum na mtu maalum, na kuelekezwa kwa mtu maalum. Ahadi ya kimungu huelekezwa kwa imani ya mtu. Matokeo yake imani hushika kile kinachoahidiwa kama kilivyoahidiwa kwa muumini binafsi. Luther alisisitiza kuwa imani hii ndio pekee inayofaa kuitikia neno la ahadi ya Mungu. Mwanadamu anaitwa kutojitazama mwenyewe ila kutazama ahadi ya Mungu na kuiamini kikamilifu. Kwa kuwa imani inatuweka katika msingi wa ahadi za Kristo, inampa mwamini hakika timilifu ya wokovu. Kutokuwa na imani katika neno hili, kutamfanya Mungu mwongo au mmoja wa wale ambao neno lao huwezi kulitegemea. Kwa mtazamo wa Luther kutokuwa na imani ni dhambi kubwa kuliko zote mbele ya Mungu.

104. Zaidi ya kuhusisha uhusiano kati ya Mungu na mwenye dhambi katika sakramenti ya kitubio, uhusiano wa ahadi na kusadiki pia hujenga uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu katika kuhubiri Neno. Mungu anapenda kuhusika na wanadamu kwa kuwapa neno la ahadi. Sakramenti pia ni neno la ahadi linaloonesha nia ya Mungu wa kuwaokoa wanadamu. Kwa upande mwingine wanadamu

[5] "Mungu hatamnyima neema yake yule afanyaye yale yaliyo ndani yake."

wanapaswa kuhusiana na Mungu kwa kuzitegemea tu ahadi zake. Imani hutegemea kabisa ahadi za Mungu; haiwezi kuumba kitu ambacho mwanadamu ataweka tegemeo lake kwake.

105. Hata hivyo, kutegemea ahadi za Mungu sio jambo la maamuzi ya kibinadamu, ila Roho Mtakatifu ndiye anayefunua ahadi hizi kama za kutegemewa na kujenga imani ndani ya mtu. Ahadi za kimungu na imani ya mwanadamu zinawekwa pamoja. Vipengele vyote viwili vinapaswa kusisitizwa kwa pamoja, ahadi kama ilivyo na imani ya mhusika. Kulingana na Luther, Mungu hafunui tu ukweli wake kama taarifa ambayo lazima akili ya kawaida ikubaliane nao, ufunuo wa Mungu una makusudi ya wokovu unaoelekezwa kwa imani na ukombozi wa muumini ambaye anapokea ahadi za Mungu anazotoa, kwa "ajili yako" kama maneno ya Mungu kwa ajili yangu (pro me) au kwa ajili yetu (pro nobis).

106. Jitihada pekee za Mungu zinaanzisha uhusiano wa wokovu kwa mwanadamu, ambapo wokovu unatokea kwa neema. Zawadi ya neema inaweza tu kupokelewa, na kwa kuwa zawadi hii tunaipokea kupitia ahadi ya kimungu, haiwezekani kupokelewa isipokuwa kwa njia ya imani na sio kwa matendo. Wokovu unatokea kwa neema pekee. Hata hivyo, Luther wakati wote alikaza kuwa mwanadamu mwenye kuhesabiwa haki atatenda matendo mema kwa msaada wa Roho Mtakatifu.

### Kwa Njia ya Kristo tu

107. Upendo wa Mungu kwa wanadamu umeasilika, na umejikita na kujengeka ndani ya Kristo Yesu. Hivyo, kwa neema pekee, inaelezwa wakati wote kwa njia ya Kristo pekee. Hapa Luther anaeleza uhusiano binafsi wa mwanadamu na Kristo kwa kutumia mfano wa ndoa ya kiroho. Nafsi ndiye bibi arusi, na Kristo ndiye bwana arusi, imani ni pete ya arusi. Kulingana na sheria za ndoa, mali ya bwana arusi (haki) inakuwa ni mali ya bibi arusi, na mali ya bibi arusi (dhambi) inakuwa mali ya bwana arusi. Mabadilishano haya ya furaha ni kusamehewa dhambi na kupokea wokovu.

108. Taswira inaonesha kuwa jambo la nje, ambalo ni haki ya Kristo, inakuwa jambo la ndani. Hilo linakuwa mali ya moyoni, lakini katika ushirika na Kristo kwa kutegemea ahadi zake, na wala si katika hali ya kutengana na Kristo. Luther anakaza kuwa, haki yetu moja kwa moja ni ya nje kwa sababu ni mali ya Kristo. Hata hivyo inakuwa mali yetu moja kwa moja kwa njia ya imani katika Kristo. Pale ambapo pande hizi mbili zitasisitizwa kwa usawa, ndipo ukweli wa wokovu utaeleweka vizuri. Luther anasema, kiuhalisia Yesu yupo kwa njia ya imani [6]. Kristo yupo kwa ajili yetu (*pro nobis*) na ndani yetu (*in nobis*) na sisi tu ndani ya Kristo (*in Christo*).

### Umuhimu wa Sheria

109. Luther vilevile alitambua hali ya mwanadamu, kuhusiana na sheria katika maana ya kitheolojia au kiroho, kwa mtazamo wa yale Mungu anayodai kutoka kwetu. Yesu anaeleza mapenzi ya Mungu kwa kusema, Utampenda Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote na kwa akili zako zote (Mt 22:37). Hii ina maana amri za Mungu zinakamilika tu kwa kujitoa kabisa kwa Mungu. Hii haihusishi tu nia na matendo ya nje yanayoambatana nayo, bali pia vipengele vyote vya nafsi na moyo wa mwanadamu kama vile hamu, shauku, jitihada za mwanadamu, yaani vipengele na mwenendo wa nafsi ambavyo ama havitawaliwi kabisa na (haviko chini ya) mapenzi (nia) ya mtu au ambavyo vinatawaliwa kwa njia isio ya moja kwa moja kupitia matendo mema.

110. Katika mambo ya kisheria na maadili, kuna kanuni ya kale, ambayo ni wazi kihisia, kwamba hapana mtu analazimika kufanya chochote kuzidi uwezo wake (*ultra posse nemo obligatur*). Hivyo, katika enzi za miaka ya kati, Watheolojia wengi walishawishika kuamini kuwa amri hii ya kumpenda Mungu lazima ijikite ndani ya hiari ya mtu. Kulingana na ufahamu huu, amri ya kumpenda Mungu hailazimu mienendo yote ya nafsi, kuelekezwa na kutolewa maalum kwa

---

[6] *WA* 40/II; 229, 15.

Mungu. Badala yake, ingetosha kwamba hiari ya mtu itampenda Mungu kuliko vitu vyote. (*diligere deum super omnia*).

111. Luther alisema, hata hivyo, kuna tofauti ya uelewa kati ya sheria kimaadili na uelewa wa sheria kisheria, kwa upande mmoja, na uelewa wake kitheolojia, kwa upande mwingine. Mungu hajahusisha amri zake katika hali ya mwanadamu aliyeanguka katika dhambi. Badala yake kwa mtizamo wa kitheolojia, amri ya kumpenda Mungu inaonesha hali na uovu wa mwanadamu. Kama Luther alivyoandika katika andiko la mabishano kinyume cha theolojia ya Waskolastika: "Uelewa kiroho ni kuwa mtu si kwamba haui, hafanyi uovu, hakasiriki au kuwaka tamaa asipokuwa na hasira au tamaa mbaya tu."[7]. Katika uelewa huu, sheria ya Mungu kimsingi haitimizwi kwa matendo ya nje tu au kwa nia ya kuacha matendo ya tamaa bali sheria itatimiziwa kwa kujitoa kwa moyo wote wa mwanadamu mzima kwa mapenzi ya Mungu.

### Kushiriki Katika Haki ya Kristo

112. Msimamo wa Luther, kwamba Mungu anamtaka mtu kujitoa kwa moyo wake wote kutimiza sheria zake, unaeleza, kwa nini Luther alikaza kwa nguvu kwamba tunategemea haki ya Kristo tu. Kristo ndiye mtu pekee aliyetimiza mapenzi ya Mungu kwa ukamilifu. Wanadamu wengine wote wanaweza tu kutenda haki kwa mtizamo wa kitheolojia, ikiwa wanashiriki kwenye haki ya Kristo. Kwa hiyo haki yetu ni kitu cha nje, kwa vile ni haki ya *Kristo*. Lakini lazima iwe haki *yetu*, ambayo ni ya ndani, kwa imani katika ahadi ya Kristo. Ni kwa namna tu ya kushiriki kule kujitoa kwa Yesu kwa Mungu kwa moyo wote, sisi tunaweza kuwa kwenye haki kikamilifu.

113. Kwa kuwa Injili inatuahidi, hapa ni Kristo na Roho wake, ushiriki wetu katika haki ya Kristo hauwezekani bila kuwa chini ya uwezo wa

[7] Luther, "Disputation against Scholastic Theology (1517)", tr. Harold J. Grimm, *LW* 31:13; *WA* 1, 227, 17–18.

Roho Mtakatifu anayetuhuisha. Hivyo, kuwa na haki na kuhuishwa ni pande mbili ambazo zipo pamoja na hatuwezi kuzitenganisha. Luther hakukosoa Watheolojia wenzake kama Gabriel Biel kwa mkazo wake mkali kuhusu nguvu ya neema katika kuleta mabadiliko, kinyume chake alipinga kuwa hawakusisitiza inavyotakikana nguvu ya neema kama msingi wa mabadiliko ya kweli ndani ya muumini.

**Sheria na Injili**

114. Kulingana na Luther, kuhuishwa huku hakutafikia utimilifu tukiwa hai. Kwa hiyo, muundo mwingine wa kuelezea wokovu wa mwanadamu ulikuwa muhimu kwa Luther. Muundo huu ulitokea kwa Mtume Paulo. Katika Warumi 4:3, Paulo anarejea kwa Abrahamu katika Mwanzo 15:6: "(Abrahamu) akamwamini BWANA, naye akamhesabia jambo hili kuwa haki." na anahitimisha: "Lakini kwa mtu asiyefanya kazi, bali anamwamini yeye ambaye amhesabia haki, asiyekuwa mtauwa, imani yake mtu huyo imehesabiwa kuwa haki." (Rumi 4:5)

115. Kifungu hiki kutoka Warumi kinahusisha mawazo ya kimahakama kwa mtu aliyepo katika chumba cha mahakama aliyetangaziwa haki. Ikiwa Mungu anamtangazia mtu fulani kuwa haki, hili linabadili hali yake na kujenga hali mpya. Hukumu ya Mungu haibaki nje ya mwanadamu. Luther mara nyingi alitumia mfano wa Paulo kwa lengo la kusisitiza kuwa mtu katika utimilifu wake amekubaliwa na Mungu na ameokolewa kwa ujumla. Hata hivyo mchakato wa kuhuishwa ndani kwa aliyehesabiwa haki kufikia hali ya kujitoa kikamilifu kwa Mungu, hauwezi kufikia utimilifu katika maisha ya hapa duniani.

116. Sisi kama waumini ambao tupo katika mchakato wa kuhuishwa na Roho Mtakatifu, bado hatujatimiza kwa ukamilifu amri ya Mungu ya kumpenda Mungu kwa moyo wote na hatujaweza kutimiza madai yote ya Mungu. Hivyo sheria inatushtaki na kutubainisha kama wenye dhambi. Kwa mtazamo wa sheria, kitheolojia tunaamini kuwa bado tu wenye dhambi. Lakini kwa kuzingatia Injili, ambayo inatuahidi ipo haki ya Kristo, tuna haki ya kuhesabiwa haki kwa sababu tunaamini katika ahadi za Injili. Huu ndio uelewa wa Luther wa muumini wa

Kikristo ambaye kwa wakati huo huo ni mwenye dhambi na wakati huo huo ni mwenye kuhesabiwa haki. (*simul iustus et peccator*).

117. Hii haina utata kwani lazima kubainisha mahusiano aina mbili ya muumini kwa Neno la Mungu: Uhusiano na Neno la Mungu kama sheria ya Mungu inayomhukumu mwenye dhambi; Na Uhusiano na Neno la Mungu kama Injili ya Mungu kwa kuwa Kristo anatukomboa. Kwa kuzingatia uhusiano wa kwanza sisi ni wenye dhambi, lakini kwa kuzingatia uhusiano wa pili sisi ni watakatifu waliohesabiwa haki. Uhusiano huu wa pili ni uhusiano wa kudumu unaopita mwingine. Hii ina maana kuwa Kristo anatuhusisha katika mchakato endelevu wa kuhuishwa kwa kadri tunavyotegemea katika ahadi zake kuwa tumeokolewa milele.

118. Hii ndiyo maana Luther alikaza kwa nguvu zote uhuru wa Mkristo. Uhuru wa kukubaliwa na Mungu kwa neema tu na kwa imani tu katika ahadi za Kristo, uhuru kutoka kushitakiwa na sheria kwa njia ya msamaha wa dhambi, na uhuru wa kutumikia jirani kwa hiari bila kutafuta malipo. Mtu aliyehesabiwa haki hata hivyo anategemewa kutimiza amri za Mungu na atafanya hivyo kwa kuhamasishwa na Roho Mtakatifu. Kama Luther anavyotamka katika Katekisimo ndogo yatupasa kumwogopa Mungu na kumpenda, hivyo tu…, baadaye maelezo ya amri kumi yanafuata [8].

## *Maelezo ya Kanisa Katoliki Kuhusu Kuhesabiwa Haki*

119. Hata katika karne ya kumi na sita, kulikuwepo na makubaliano ya msingi kati ya Walutheri na Wakatoliki kuhusu umuhimu wa neema ya Mungu na udhaifu wa mwanadamu kupata wokovu kwa nguvu zake mwenyewe. Mkutano mkuu wa Trent ulifundisha dhahiri kwamba mwenye dhambi hawezi kuhesabiwa haki ama kwa njia ya sheria au kwa jitihada za mwanadamu. Ulipinga yeyote anayedai mwanadamu anaweza kuhesabiwa haki mbele za Mungu kwa ajili ya kazi zake

[8] Luther, “The Small Catechism,” Katika *BC*, 351-54.

alizotenda au kwa nguvu zake za asili, au kwa mafundisho ya sheria, au bila neema ya Mungu kupitia Yesu Kristo [9]

120. Hata hivyo Wakatoliki, wameona baadhi ya misimamo ya Luther ni ya kutaabisha. Baadhi ya lugha aliyotumia Luther ilisababisha Wakatoliki kutilia mashaka kama Luther alipinga uwajibikaji wa mtu binafsi kwa matendo yake. Hii ndiyo maana mkutano mkuu wa Trent ulisisitiza uwajibikaji binafsi wa mtu na uwezo wa kushirikiana na neema ya Mungu. Wakatoliki walisisitiza kwamba aliyehesabiwa haki lazima ahusike katika kufunuliwa kwa neema kwenye maisha yake. Hivyo kwa aliyehesabiwa haki, jitihada za mwanadamu huchangia kukua zaidi katika neema na ushirika na Mungu.

121. Aidha, kulingana na maandiko ya Wakatoliki, fundisho la Luther kuhusu shutumu za kimahakama (*forensic imputation*) ilionekana kupinga nguvu ya kibunifu ya neema ya Mungu kushinda dhambi na kumbadilisha aliyehesabiwa haki. Wakatoliki hawakutaka kusisitiza juu ya msamaha wa dhambi tu, bali pia kutakaswa kwa mwenye dhambi. Hivyo katika utakaso Mkristo anapokea haki ya Mungu ambapo Mungu anatufanya kuwa wenye haki.

## *Majadiliano ya Kilutheri - Kikatoliki Juu ya Kuhesabiwa Haki*

122. Luther na Wanamatengenezo wengine walitambua fundisho la kuhesabiwa haki kwa wenye dhambi kama fundisho la kwanza na la msingi [10], tena kama mwongozo na mwamuzi juu ya sehemu zote za fundisho la Kikristo[11]. Hii ndiyo sababu, mgawanyiko katika hoja hii ulikuwa mkali. Na kazi ya kushinda mgawanyiko huu ilikuwa jambo lililopewa kipaumbele katika mahusiano ya Wakatoliki na Walutheri. Katika nusu ya pili ya karne ya ishirini mzozo huu ulikuwa mada

[9] Council of Trent, Sixth Session, 13 January 1547, can. 1

[10] Luther, “Smalcald Articles,” katika *BC*, 301.

[11] *WA* 39/1, 205, 2–3.

ya uchunguzi wa kina baina ya wanatheolojia binafsi na pia katika majadiliano mbalimbali ya kitaifa na ya kimataifa.

123. Muhtasari wa matokeo ya uchunguzi na majadiliano haya unapatikana ndani ya *Azimio la Pamoja la Fundisho la Kuhesabiwa Haki (Joint Declaration on the Doctrine of Justification JDDJ)*, na mwaka 1999 lilipokelewa rasmi na kanisa la Katoliki na Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani. Maelezo yafuatayo yamejikita katika azimio hili, ambalo linaonesha mapatano yanayoundwa na maazimio ya pamoja yaliyo sambamba na mikazo tofauti toka kila upande, kwa madai kuwa tofauti hizi hazibatilishi mifanano (maeneo ya mfanano) ya pande hizi mbili. Kwa hiyo ni maafikiano yasioondoa tofauti, bali kwa wazi yanahusisha tofauti hizo.

## Kwa Neema tu

124. Wakatoliki na Walutheri kwa pamoja wanakiri: "Kwa neema tu, katika imani katika kazi ya wokovu ya Kristo na wala si kwa sababu ya matendo yetu yeyote tunakubalika na Mungu na kupokea Roho Mtakatifu, anayehuisha mioyo yetu akituwezesha na kutuita kwenye matendo mema" (JDDJ 15). Kifungu "kwa neema tu" kimeelezewa zaidi katika njia hii: "Ujumbe wa kuhesabiwa haki [...] unatuambia sisi, kama wenye dhambi, maisha yetu mapya ni kutokana tu na msamaha na rehema inayotuhuisha, ambayo Mungu anatupa kama zawadi na tunapokea kwa imani, na hatuwezi kustahili kwa namna yeyote ile" (JDDJ 17).[12]

125. Ni katika mhimili huu ambapo mipaka na heshima ya uhuru wa mwanadamu vyaweza kuainishwa. Kifungu "kwa neema tu", kwa mtazamo wa mwenendo wa mwanadamu kuelekea wokovu, kinatafsiriwa katika njia hii: "Tunakiri pamoja, kwamba watu wote hutegemea kabisa neema inayotoka kwa Mungu pekee kwa wokovu

[12] The Lutheran World Federation and the Roman Catholic Church, *Joint Declaration on the Doctrine of Justification* (Grand Rapids, MI., Cambridge: Eerdmans, 2000) [=*JDDJ*].

wao. Uhuru walio nao kuhusiana na watu na vitu vya dunia hii sio uhuru kuhusiana na wokovu" (JDDJ 19).

126. Wakati Walutheri wanakaza kuwa mtu anaweza kuhesabiwa haki, wanamaanisha, hata hivyo, kuna "kuondoa uwezekano wowote wa mtu kuchangia kwenye kuhesabiwa haki binafsi. Lakini hawakatai kwamba waumini wanahusishwa moja kwa moja binafsi katika imani yao, ambayo inaasilishwa na neno la Mungu" (JDDJ 21).

127. Wakati Wakatoliki wanazungumza juu ya maandalizi ya neema kwa maana ya "ushirikiano", wanamaanisha "kuhusika binafsi" kwa mwanadamu ambako "ni tokeo la neema, na wala si tendo linalochipua ndani ya uwezo wa mwanadamu" (JDDJ 20). Hivyo Wakatoliki hawakani maelezo ya pamoja, kwamba wenye dhambi "hawana uwezo wa kumgeukia Mungu kwa uwezo wao, kutafuta ukombozi kukidhi kuhesabiwa haki mbele za Mungu, au kufikia wokovu kwa nguvu zao wenyewe. Kuhesabiwa haki kunatokea kwa neema ya Mungu pekee tu" (JDDJ 19).

128. Kwa kuwa imani inajulikana sio tu kama ufahamu unaokubali kwa akili tu, lakini pia kama tegemeo la moyo lililojikita lenyewe katika Neno la Mungu, tunaweza kusema kwa pamoja, "Kuhesabiwa haki kunatokea kwa neema tu; (JDDJ 15 na16), kwa imani tu; Mtu anahesabiwa haki bila matendo (Rum 3:28, cf.JDDJ 25)"; (JDDJ, Annex 2C). [13]

129. Kile kilichotenganishwa mara kwa mara na kuhusishwa na (ukiri) upande mmoja au mwingine, lakini sio kwa wote wawili, sasa kimetambuliwa katika mshikamano halisi pamoja: "Wakati watu huja kwa imani kushiriki katika Kristo, Mungu haendelei kuwahukumu katika dhambi, bali kwa njia ya Roho Mtakatifu huwasilisha ndani yao upendo hai. Vipengele hivi viwili vya utendaji wa neema ya Mungu havipaswi kutenganishwa" (JDDJ 22).

---

[13] Ibid., JDDJ

**Imani na Matendo Mema**

130. Ni muhimu kwamba Walutheri na Wakatoliki wana mtizamo wa aina mmoja kuhusu mwonekano wa uhusiano wa matendo na imani: Waumini "wanaweka tumaini lao katika ahadi ya neema ya Mungu kwa imani inayowahesabika haki, ambayo inahusisha tumaini katika Mungu na kumpenda. Aina hii ya imani ni hai katika upendo; hivyo Mkristo hawezi na hapaswi kubaki bila matendo" (JDDJ 25). Kwa hiyo, Walutheri pia hukiri nguvu ya Neema ya Mungu itendayo kazi ambayo hugusa maeneo yote ya mwanadamu na kumwongoza kwenye maisha yenye tumaini na upendo" (JDDJ 26). "Kuhesabiwa haki kwa imani tu" na "kuhuishwa", lazima vitofautishwe lakini visitenganishwe.

131. Wakati huo huo, "Kwa mwenye kuhesabiwa haki, lolote linalotangulia au kufuata kipawa cha imani, sio msingi wa kuhesabiwa haki wala stahili yake." (JDDJ 25) Ndio maana msukumo ambao Wakatoliki wanayoipa neema inayotuhesabia haki hautegemewi kuwa sifa isiohusika na Mungu. Au ambayo anayeimiliki angeweza kujitetea kwayo mbele ya Mungu." (JDDJ 27). Badala yake, mtazamo huu unachukulia kwamba ndani ya uhusiano mpya na Mungu mwenye kuhesabiwa haki, anafanywa kiumbe kipya na kuwa mwana wa Mungu, ambaye anaishi katika ushirika mpya na Kristo. Ushirika huu mpya binafsi na Mungu unaasilika kabisa kutoka neema ya Mungu pekee na hubakia wakati wote tegemezi kwa kazi ya wokovu na kazi iliyoasilishwa na neema ya Mungu. Mungu huyu, anayebaki na kweli yake mwenyewe, ili binadamu aweze kumtegemea. " (JDDJ 27).

132. Kuhusu swali la matendo mema, Wakatoliki na Walutheri kwa pamoja wanatamka: "Tuna kiri pia kwamba amri za Mungu zinashikilia thamani yake kwa yule ambaye amehesabiwa haki (JDDJ 31).Yesu Kristo mwenyewe, pia hata maandiko ya mitume, huhimiza "Wakristo kuwa na matendo ya upendo yanayotokana na kuhesabiwa haki kama matunda yake." (JDDJ 37). Ili uwajibikaji kwa amri usieleweke vibaya, imesemwa: "Wakati Wakatoliki wanasisitiza, kwamba wenye haki wanapaswa kuzingatia amri za Mungu, hawapingi kwamba

kupitia Yesu Kristo, Mungu kwa rehema amewaahidi watoto wake kuwapa neema ya uzima wa milele" (JDDJ 33).

133. Wote wawili, Walutheri na Wakatoliki, wanaweza kutambua thamani ya matendo mema katika mtazamo wa kuimarisha ushirika na Kristo (rejea JDDJ 38 kuendelea), hata kama Walutheri hukaza kuwa kuhesabiwa haki, kama kukubalika na Mungu na kushiriki kwenye haki ya Kristo, kwa wakati wote ni timilifu. Dhana kinzani ya matendo mema inaelezewa kuwa, "Wakati Wakatoliki hukubali hali ya ustahili kwa ajili ya kazi njema, wanataka kusema kwamba, kulingana na ushahidi wa kibiblia, thawabu mbinguni imeahidiwa kwa haya matendo mema. Kusudi lao ni kusisitiza wajibu wa watu kwa yale wanayoyatenda, na wala sio kupinga sifa ya matendo kama vipawa, au kupinga kuwa kuhesabiwa haki hubaki kuwa zawadi ya neema ambayo hatustahili." (JDDJ 38).

134. Kwa yale mengi yaliyojadiliwa kuhusu suala la ushirikiano wa wanadamu, nukuu kutoka maungamo ya Kilutheri imetumika katika nyongeza kwenye *Azimio la Pamoja la Fundisho la Kuhesabiwa Haki (JDDJ)*, kama msimamo wa pamoja katika upekee wa hali ya juu: "Neema ya Mungu itendayo kazi, haitengi matendo ya mwanadamu, Mungu huasilisha yote, utayari na mafanikio, kwa hiyo, tunaitwa kukazana (rejea Filipi 2:12 kuendelea). 'Mara tu Roho Mtakatifu aanzishapo kazi yake ya kutufanya kiumbe kipya na kutuhuisha kwa njia ya Neno na Sakramenti takatifu, ni hakika kuwa tunaweza na ni lazima tushirikiane kwa uweza wa Roho Mtakatifu…'"[14]

## Mwenye Haki na Mdhambi kwa Wakati Mmoja (Simul iustus et peccator)

135. Katika mjadala juu ya tofauti katika kusema kuwa Mkristo ni "mwenye dhambi na mwenye haki kwa wakati mmoja", ilionekana kuwa pande zote hazina uelewa timilifu wa kuhusu maneno dhambi,

[14] *JDDJ*, Annex 2C, akinukuu "The Formula of Concord, Solid Declaration," II. 64f., katika *BC*, 556.

tamaa, na kuhesabiwa haki. Ni muhimu kutokuweka msisitizo kwenye muundo tu, lakini na kwenye yaliyomo kwa lengo la kufikia muafaka. Kufuata Warumi 6:12 na 2 Wakorintho 5:17, Wakatoliki na Walutheri wanakubaliana kuwa kwa Wakristo dhambi lazima na inapaswa isitawale. Zaidi hukaza kulingana na 1Yohana 1:8-10 kuwa Wakristo sio bila dhambi. Wanasema juu ya utata kwa Mungu ndani ya tamaa ya ubinafsi ya Adamu wa kale pia katika waliohesabiwa haki, kunakofanya mapambano ya kudumu katika maisha kinyume chake kuwa ya lazima (JDDJ 28)

136. Uelekeo huu hauendani na kusudi la asili la Mungu kumuumbia binadamu utu, na inapingana kwa wazi na Mungu (JDDJ 30), kama Wakatoliki wanavyosema. Kwa kuwa kwa upande wao, dhambi ina tabia ya tendo. Wakatoliki hapa hawasemi habari ya dhambi, wakati Walutheri huona katika mwelekeo huu wa upinzani kukataa kujitoa binafsi kikamilifu kwa Mungu na hivyo kuita hali hii dhambi. Lakini wote wawili (Wakatoliki na Walutheri) wanasisitiza, kwamba hii tabia ya kupingana haimtengi aliyehesabiwa haki na Mungu.

137. Chini ya fikra za mfumo wake wa kitheolojia na baada ya kujifunza maandiko ya Luther, Kadinali Cajetan alijumlisha mawazo ya Luther kwa kusema, kulingana na ufahamu wa Luther kuhusiana na hakika ya imani ilimaanisha kuanzisha kanisa jipya. Majadiliano kati ya Wakatoliki na Walutheri umeainisha mitizamo ya aina tofauti ya Cajetan na Luther ambayo iliasilisha kutokuelewana kwao. Leo, inawezekana kusema, Wakatoliki wanaweza kushiriki mawazo ya Wanamatengenezo ya Kanisa kuweka msingi wa imani katika ukweli halisi wa ahadi ya Kristo, kutokuangalia uzoefu wetu, na kutumaini katika Neno la msamaha wa Kristo pekee. (Mt 16:19, 18:18) (JDDJ 36).

138. Walutheri na Wakatoliki wameshutumiana na kalaumiana kila mmoja kwenye mafundisho katika maungamo yao. Kwa hiyo, maridhiano ya tofauti zao kama yalivyowasilishwa kwenye *azimio la pamoja la fundisho la kuhesabiwa,* lina pande mbili, upande mmoja, azimio linadai kuwa mapingamizi ya Wakatoliki na mafundisho ya Walutheri kama yalivyoainishwa hayahusishi katika maungamo mengine. Kwa

upande wa pili, azimio linalokubaliana na maridhiano katika kweli za msingi wa fundisho la kuhesabiwa haki; “Uelewa wa fundisho la kuhesabiwa haki lilivyowekwa bayana katika azimio linaoonesha kwamba maridhiano yamefikiwa kati ya pande mbili Walutheri na Wakatoliki, katika ukweli wa kimsingi wa fundisho la kuhesabiwa haki”. (JDDJ 40).

139. Katika mwanga wa maridhiano haya tofauti zilizobakia kuhusiana na lugha, mafafanuzi ya kitheolojia, na msisitizo katika ufahamu wa kuhesabiwa haki zinakubalika. Kwa hiyo maelezo ya Walutheri na Wakatoliki kuhusu kuhesabiwa haki katika tofauti zao ni wazi kwa kila mmoja na haziharibu mwafaka unaohusu kweli za msingi (JDDJ 40). Hivyo mashutumu ya kimafundisho ya karne ya kumi na sita, yanayohusiana na fundisho la kuhesabiwa haki, yanaonekana katika mwanga mpya: Mafundisho ya makanisa ya Kilutheri yaliyowasilishwa katika azimio hili la pamoja hayaingii katika mashutumu ya mkutano wa Trent. Mashutumu katika Maungamo ya Kilutheri hayahusishi fundisho la Kanisa la Kirumi ambalo limejadiliwa katika azimio la pamoja la kuhesabiwa haki. (JDDJ 41). Huu ni mwitikio wa hali ya juu kuhusiana na mtafaruku juu ya fundisho hili uliodumu kwa karibu nusu milenia.

## Ekaristi

### *Ufahamu wa Luther Juu ya Chakula cha Bwana*

140. Kwa Walutheri na Wakatoliki Chakula cha Bwana ni kipawa cha pekee ambapo Wakristo wanapata ustawi na faraja kwa ajili yao, pale na ndipo Kanisa wakati wote ni jipya linakusanya kwa upya na kujengwa. Kwa hiyo malumbano kuhusu Sakramenti hii yanaleta maumivu.

141. Luther alielewa Sakramenti ya Chakula cha Bwana kama agano, (*testamentum*), ahadi ya yule anayekaribia kufa, kama inayothibitishwa kutoka toleo la Kilatini la maneno ya kusimika. Mwanzoni Luther

alichukulia ahadi ya Kristo (testamentum) kama ahadi ya neema na msamaha wa dhambi lakini, katika mdahalo na Huldrych Zwingli, alisisitiza imani yake, kwamba Yesu Kristo anajitoa mwenyewe, mwili wake na damu yake, ambavyo kweli vipo. Imani haimfanyi Kristo awepo, ni Kristo anayejitoa mwenyewe mwili na damu yake, kwa washiriki, bila kujali wanaamini au la. Hivyo, upinzani wa Luther kwa fundisho la kisasa sio kwamba alikataa uwepo halisi wa Yesu Kristo, ila alihusika na jinsi ya kuelewa badiliko linalotokea katika Chakula cha Bwana.

### Uwepo Halisi wa Kristo

142. Mkutano wa nne wa Lateran (1215) ulitumia kitenzi *transubstantiare,* neno ambalo linatofautisha kati ya kiini na mbadiliko wa umbo [15]. Ingawa kwa Luther huu ulikuwa ni uwezekano wa maelezo yanayoelekea kile kinachotokea katika Chakula cha Bwana, hakuona jinsi maelezo haya ya kifilosofia yangeweza kuwa ya lazima kwa Wakristo wote. Kwa kila hali, Luther mwenyewe alisisitiza kwa nguvu uwepo halisi wa Kristo katika sakramenti.

143. Uelewa wa Luther ulikuwa mwili na damu ya Kristo kuwepo ndani na katika mkate na mvinyo. Kuna mabadilishano ya hali (sifa, tabia - communication idiomatum) kati ya mwili na damu ya Kristo na mkate na mvinyo. Hali hii inasababisha muungano wa kisakramenti kati ya mkate na mwili wa Kristo na mvinyo na damu ya Kristo. Aina hii mpya ya muungano, unaoasilishwa kwa ushirikiano wa hali (tabia), unafanana na muungano wa asili ya Mungu na asili ya Mwanadamu katika Yesu Kristo. Luther vilevile alifananisha uhusiano wa Sakramenti na uhusiano wa chuma na moto katika tanuru la chuma.

144. Kama tokeo lake la uelewa wa asili ya maneno ya kuanzishwa Chakula cha Bwana, (Nyweni nyote katika hiki, Mt. 26:27) Luther alipinga kitendo cha kuwazuia walei kushiriki, Sakramenti katika (kwa) aina

[15] The Fourth Lateran General Council, Symbol of Lateran (1215), *DH* 802.

zote mbili, mkate na mvinyo. Hakusema kuwa walei watashiriki nusu ya mwili wa Kristo, lakini alitamka (alithibitisha) kuwa watampokea Kristo katika ukamilifu wake katika aina zote mbili. Hata hivyo, Luther alipinga kuwa Kanisa lilikuwa na uwezo wa kuondoa damu ya Kristo kwa walei kwa kuwa maneno ya kuanzisha Chakula cha Bwana yapo wazi katika hili. Wakatoliki katika hili wanawakumbusha Walutheri kuwa sababu za kiuchungaji ndizo chimbuko la kufanya zoezi hili la kushiriki kwa kutumia aina moja (yaani mkate) ya mwili wa Kristo kwa walei.

145. Luther alielewa Chakula cha Bwana pia kama tukio la ushirika, chakula halisi, ambapo (vitu/vifaa) vilivyobarikiwa vinakusudiwa kutumika na wala sio kuhifadhiwa baada ya kushiriki. Luther alihimiza matumizi ya vyote vilivyoandaliwa kwa ajili ya Chakula cha Bwana, ili suala la muda wa uwepo wa Kristo (katika sakramenti hii) lisijitokeze kabisa. [16]

## Kafara ya Ekaristi

146. Pingamizi kubwa la Luther kwa fundisho la Wakatoliki kuhusu ekaristi lilielekezwa dhidi ya ufahamu wa misa kama kafara. Theolojia ya ekaristi kama kumbukumbu halisi (anamnesis, Realgedächtnis), ambapo kafara itoshayo ya Kristo ya mara moja kwa wakati wote (Heb. 9:1-10:18) inajihudhurisha kuwepo yenyewe kwa washiriki waaminifu, haikueleweka kikamilifu katika zama za mwisho za enzi ya miaka ya kati. Hivyo, wengi walichukulia kushiriki misa kuwa aina nyingine ya kafara kama nyongeza ya kafara ya Kristo. Kulingana na nadharia iliyochipua kutoka *Duns Scotus*, wingi wa misa ulidhaniwa kuasilisha wingi wa neema na kuleta neema hii kwa watu binafsi, ndio maana enzi za Luther, kwa mfano, maelfu

[16] Luther alikuwa amemwagiza Mchungaji wa Kilutheri Simon Wolferinus asichanganye mabaki ya elementi zilizowekwa wakfu na zile zisizowekwa wakfu. Lutheri alimwambia "tufanye tunavyofanya hapa [yaani, kule Wittenberg], yaani, kula na kunywa mabaki ya Sakramenti pamoja na wanaoshiriki ili isiwe lazima kuibua maswali ya kashfa na hatari kuhusu lini hatua ya Sakramenti inaisha" (*Luthers Werke—Weimarer Ausgabe, Briefweschel,* X: 348f.).

ya misa binafsi yalikuwa yakifanyika kila mwaka katika kanisa la ngome kuu la Wittenberg.

147. Luther alisisitiza kuwa, kulingana na maneno ya kuanzisha Chakula cha Bwana, Yesu Kristo anajitoa mwenyewe katika Chakula cha Bwana kwa wote wanaompokea, na ya kwamba, kama kipawa, Yesu Kristo anaweza tu kupokelewa kwa imani na sio kutolewa. Kama Kristo alitolewa kwa Mungu, maana ya ndani na uelekeo wa ekaristi itakuwa imegeuzwa. Katika mtazamo wa Luther, kuelewa ekaristi kama toleo la kafara ingemaanisha kuwa Ekaristi ni kazi nzuri (matendo mema) tufanyayo na kuyatoa kwa Mungu. Lakini alihoji kuwa kwa kadri ambavyo hatuwezi kubatizwa mahali pa mtu mwingine, vivyo hivyo hatuwezi kushiriki ekaristi kwa niaba ya na kwa manufaa ya mtu mwingine. Badala ya kupokea kipawa cha pekee ambacho ndicho Kristo anayejitoa kwetu, tutakuwa tunajaribu kutoa kitu kwa Mungu na hivyo kubadilisha kipawa cha Mungu kuwa matendo mema.

148. Hata hivyo, Luther aliweza kuona dalili za kafara katika misa, kafara ya shukrani na sifa. Ni sadaka halisi ambapo kwa kutoa shukrani, mtu anakiri ya kuwa yupo katika uhitaji wa kipawa na kwa jinsi hiyo hali yake itabadilika tu kwa kupokea kipawa. Kwa hiyo, kupokea kwa kweli katika imani kunahusisha upande wa utendaji ambao haupaswi kupuuzwa.

### *Mashaka ya Wakatoliki Kuhusiana na Ekaristi*

149. Kwa upande wa Wakatoliki, hali ya Luther kuipinga dhana ya kubadilika mkate na mvinyo kuwa mwili na damu kweli ya Bwana Yesu, inaamsha mashaka endapo fundisho la uwepo wa Kristo katika Chakula cha Bwana lilikuwa limethibitika kikamilifu katika theolojia yake. Ingawa mkutano wa Trent ulitamka, kwamba hatutaweza kueleza kwa maneno hali ya uwepo wa Kristo na kutofautisha fundisho la kubadilika kwa vitu au vifaa vile kutoka katika maelezo ya kitaalamu, hata hivyo ulikubali, “Kanisa takatifu Katoliki wameita

badiliko hili "*transsubstantiation*".[17] Dhana hii ilionekana, katika mtazamo wa Wakatoliki, kuwa hakikisho la kweli la kudumisha uwepo halisi wa Yesu Kristo katika mkate na mvinyo na kuthibitisha uwepo halisi wa Yesu Kristo kwa kila kipengele kinachounda Chakula cha Bwana, yaani mkate na mvinyo. Wakati Wakatoliki wanasisitiza vitu vilivyoumbwa kubadilika vyenyewe, wanatamani kudhihirisha uwezo wa uumbaji wa Mungu, ambao unatoa uumbaji mpya katikati ya uumbaji wa zamani.

150. Wakati mkutano wa Trent ulitetea zoezi la kusujudia sakramenti iliyokwisha barikiwa, ilichukua kama hatua ya awali kuwa kusudi la msingi la ekaristi ni ushirika wa waaminio. Yesu Kristo alianzisha ekaristi itumike kama chakula cha kiroho. [18]

151. Kama tokeo la kupoteza uadilifu wa dhana ya kukumbuka, Wakatoliki walikabiliana na ugumu kukosa vithibitisho vya kutosha kueleza uelewa wa ekaristi kama dhabihu. Wakikabiliwa na mapokeo ya nyakati za mababa, Wakatoliki hawakutaka kuacha utambulisho wao wa kuona ekaristi kama kafara halisi hata wakati walipokuwa wanakazana kukubali utambulisho wa hii kafara ya ekaristi pamoja na kafara pekee ya Yesu Kristo. Kuhuishwa kwa theolojia ya sakramenti na liturgia kama ilivyoainishwa katika Mtaguso wa Pili wa Vatikani ulipaswa kuhimiza dhana ya ukumbusho (anamnesis) (SC 47:LG 3)

152. Katika majadiliano ya kiekumeni, Walutheri na Wakatoliki wanaweza wote kunufaika kutoka maono ya mwenendo wa kiliturgia na mitazamo mipya ya kitheolojia. Katika kujadili wazo la *anamnesis*, wote wameongozwa katika uelewa mzuri ya uelewa wa jinsi sakramenti ya Ekaristi kama ukumbusho inavyotokeza uwepo halisi wa tukio la wokovu, na hasa kafara ya Kristo. Wakatoliki wanaweza kuheshimu aina mbalimbali za uwepo wa Kristo katika liturgia ya ekaristi. Kwa mfano, uwepo wake katika Neno na katikati ya kusanyiko

[17] Council of Trent, Thirteenth Session, 11 October 1551, Sura ya IV.

[18] Ibid., Sura ya II.

(SC 7). Katika mwanga wa hakika ya fumbo la ekaristi, Wakatoliki wamejifunza kutathimini maelezo tofauti ya imani katika uwepo halisi wa Yesu Kristo katika sakramenti. Walutheri wamenufaika na ufahamu mpya wa sababu ya kujihusisha kwa heshima na mkate na mvinyo uliobarikiwa baada ya adhimisho.

## *Majadiliano ya Walutheri na Wakatoliki Kuhusu Chakula cha Bwana*

153. Hoja ya uwepo halisi wa Yesu Kristo katika Chakula cha Bwana sio suala la kupingana kati ya Walutheri na Wakatoliki. Majadiliano kati ya pande hizi mbili kuhusu ekaristi, ulifikia maelezo kuwa: Mapokeo ya Walutheri unathibitisha utamaduni wa Wakatoliki kwamba chakula cha Bwana kikishabarikiwa hakibaki tu kuwa mkate na mvinyo wa kawaida bali kwa uweza wa neno liumbalo zinatolewa kama mwili na damu ya Kristo. Kwa mantiki hii Walutheri wanaweza kwa wakati mwingine kusema kama ilivyo mapokeo ya Kiyunani ya badiliko (Eucharist 51). [19] Walutheri na Wakatoliki, kwa pamoja wanakataa uwepo wa kiasili ya Yesu na wanakataa ufahamu wa sakramenti kama ukumbusho au ishara tu” (Eucharist 16).[20]

### Ufahamu wa Pamoja Kuhusu Uwepo Halisi wa Kristo

154. Walutheri na Wakatoliki wanaweza kwa pamoja kuafikiana juu ya uwepo halisi wa Yesu Kristo katika chakula cha Bwana: Katika sakramenti ya chakula cha Bwana Yesu Kristo Mungu kweli na mwanadamu kweli, yupo katika utimilifu na ukamilifu wote katika mwili na damu yake, chini ya ishara ya mkate na mvinyo. (Eucharist 16).Azimio hili la pamoja linaafiki vipengele vyote muhimu vya imani katika chakula cha Bwana kuhusu uwepo halisi wa Yesu Kristo bila kutumia dhana ya msamiati wa badiliko la asili (transubstantiation). Kwa hiyo Wakatoliki na Walutheri wanafahamu, kwamba: Bwana

[19] Cf. “Apology of the Augsburg Confession” X, katika *BC* 184–85.

[20] Growth in Agreement I, 190–214.

aliyetukuka yupo katika chakula cha Bwana katika mwili na damu alivyovitoa pamoja na Uungu wake na Ubinadamu wake kupitia Neno la ahadi katika kipaji cha mkate na mvinyo ndani ya uweza wa Roho Mtakatifu vinavyopokelewa kupitia usharika. [21]

155. Swali la uwepo halisi wa Kristo na ufahamu wake kitheolojia vimeunganishwa na swali la muda wa uwepo wake Kristo pamoja na swali la kutukuza (adoration) uwepo wa Kristo katika sakramenti baada ya kushiriki. Tofauti kuhusiana na muda wa uwepo wa Kristo katika sakramenti imejitokeza pia katika matumizi ya liturgia. Walutheri na Wakatoliki kwa pamoja wanakiri kwamba uwepo wa Kristo unaelekezwa kwenye imani ya kupokea ekaristi, kwamba si tu imefungwa na wakati wa kupokea, na haitegemei imani ya mpokeaji, licha ya kuwa imani na Ekaristi vyaweza kuwa na uhusiano wa karibu (Eucharist 52).

156. Andiko la Ekaristi liliwaomba Walutheri kuona jinsi ya kutunza mkate na mvinyo vinavyobaki baada ya kushiriki. Aidha, andiko liliwatahadharisha Wakatoliki kutambua kwamba zoezi la kutukuza ekaristi halipingani na uelewa wa pamoja wa sifa/tabia ya ekaristi kama chakula (Eucharist 55). [22]

## Maridhiano Katika Ufahamu wa Kafara ya Ekaristi

157. Kwa kuzingatia yale ambayo yalikuwa ya msingi kwa Wana matengenezo, kafara ya ekaristi, majadiliano kati ya Walutheri na Wakatoliki unaelezwa kama kanuni ya msingi kuwa: Walutheri na Wakatoliki kwa pamoja wanatambua kwamba katika chakula cha Bwana, Yesu Kristo yupo kama msulubiwa ambaye alikufa kwa ajili ya

[21] Council of Trent, op. cit. (rejea 23), akinukuu Condemnations of the Reformation Era.

[22] Tafsiri ya Kiingereza inachanganya sentensi hii; rejea ya asili kutoka Kijerumani, katika H. Meyer, H. J. Urban and L. Vischer (eds), *Dokumente wachsender Űbereinstimmung: Sämtliche Berichte und Konsenstexte interkonfessioneller Gespräche auf Weltebene* 1931–1982 (Paderborn: Bonifatius and Frankfurt: Lembeck, 1983), 287.

dhambi zetu na ambaye alifufuka tena kwa ajili ya kuhesabiwa haki, kafara iliyotolewa mara moja kwa dhambi za ulimwengu. Kafara hii haiwezi kuendelea kutolewa wala haiwezi kurudiwa, wala kuletwa mbadala wake, wala kukamilishwa na nyingine, ila yaweza na ni lazima iwe inafanya kazi kwa upya kila siku katikati ya kusanyiko la washarika. Zipo tafsri tofauti miongoni mwetu kuhusiana na asili na kiwango hiki cha uwezo wake wa kufanya kazi. (Eucharist 56).

158. Dhana ya *anamnesis* [kumbukumbu] imesaidia kujibu swali lenye mvutano kuhusu jinsi ya kuhusianisha kwa usahihi kafara ya Yesu Kristo iliyofanyika mara moja na Chakula cha Bwana: Kwa njia ya kukumbuka katika ibada ya tendo la ukombozi la Mungu, haya matendo yenyewe yanakuwepo katika uweza wa Roho Mtakatifu, na usharika unaosherehekea unaungana pamoja wanaume na wanawake ambao tayari wenyewe wameguswa na matendo ya ukombozi. Hivi ndivyo agizo la Kristo katika chakula cha Bwana lilivyokusudiwa: Katika kutangaza, katika maneno yake mwenyewe, katika kifo chake, na katika marudio ya tendo lake katika chakula cha Bwana, kukumbuka huwa halisi pale ambapo Neno la Yesu na kazi yake ya ukombozi vinakuwepo katika hali halisi. [23]

159. Mafanikio ya kimaamuzi yalikuwa kutatua mtengano wa *sacrificium* (kafara ya Yesu Kristo) kutoka *sacramentum* (Sakramenti). Ikiwa Yesu Kristo ni kweli yupo katika chakula cha Bwana, basi maisha yake, mateso, kifo na kufufuka kwake pia vipo hakika na mwili wake, kwa hiyo chakula cha Bwana kinafanya uwepo wa tukio la msalaba kuwa halisi.[24]. Si tu matokeo ya tukio la msalaba ila pia tukio lenyewe lipo katika hali halisi katika chakula cha Bwana bila chakula kurudia au kukamilisha tukio la msalaba. Tukio hili moja lipo katika hali/namna ya kisakramenti. Muundo wa liturgia wa chakula kitakatifu lazima, hata hivyo, kuondoa kila kitu ambacho chaweza kuleta hisia ya kurudia au kukamilisha kafara ya msalabani. Ikiwa

[23] Condemnations of the Reformation Era, 3.II.1.2, 86.

[24] Ibid., 3.II.1.4, 88.

ufahamu wa Chakula cha Bwana utachukuliwa kwa uzito wake, tofauti zilizopo katika kuelewa kafara ya Ekaristi zinavumilika kwa Walutheri na Wakatoliki.

**Ushirika Katika Hali Zote na Ofisi ya Huduma ya Ekaristi**

160. Tangu wakati wa matengenezo ya Kanisa, kupokea kikombe kwa walei kimekuwa tabia katika ibada za Kilutheri. Kwa hivyo, kwa muda mrefu hali hii imetofautisha kwa wazi ushiriki wa sakramenti kati ya Walutheri na Wakatoliki ambao walei hupokea mkate tu. Leo, kanuni hii inaweza kuelezewa kuwa Walutheri na Wakatoliki wapo katika ukiri mmoja kuwa mkate na mvinyo zinakamilisha umbile kamili la ekaristi (Eucharist 64). Hata hivyo tofauti zimebaki katika namna ya kushiriki.

161. Kwa vile suala la uongozi katika kusherehekea Ekaristi limepewa umuhimu mkubwa katika mambo ya kiekumeni, umuhimu wa watumishi waliochaguliwa na kanisa ni jambo la msingi la pamoja lililoainishwa katika majadiliano, ”Wakristo Wakatoliki na Walutheri wanasadiki kuwa ushirikishwaji wa Ekaristi unahusisha uongozi uliochaguliwa na Kanisa” (Eucharist 65). Hata hivyo, Wakatoliki na Walutheri bado wanaelewa ofisi za huduma katika mitizamo tofauti.

## Huduma [ya Kichungaji]

### *Ufahamu wa Luther Kuhusu Ukuhani wa Waliobatizwa na Ofisi ya Kiuchungaji*

162. Katika Agano jipya, neno “hiereus” (kuhani, Kilatini, sacerdos) halikumaanisha ofisi katika ushirika wa Kikristo, ingawa Mtume Paulo anaeleza huduma yake ya kimitume kama ya Kikuhani (Rum.15:16). Kristo ni kuhani mkuu. Luther alitambua uhusiano wa waumini na Kristo kama “mabadilishano ya furaha”, “ambapo waumini wanachukua sehemu ya sifa za Kristo, na kwa jinsi hiyo kuchukua pia Ukuhani wake.” Sasa kwa haki ya kuzaliwa ya Kristo anamiliki haki mbili. Kwa hiyo kwa kutegemea haki yake kuzaliwa

ana uwezo wa kuziweka na kuzishirikisha kwa yeyote anayeamini katika yeye kulingana na kanuni zilizotajwa hapo juu kuhusu ndoa, ambapo mwanamke anamiliki chochote ambacho ni mali ya mume wake. Kwa hiyo sisi sote tunaomwamini Yesu Kristo tu makuhani na wafalme katika Kristo, kama anavyosema 1 Petro 2:9 "ninyi ni mzao mteule, watu wa Mungu, ukuhani wa Kifalme." [25] "Sote tu Makuhani waliosimikwa kwa njia ya ubatizo." [26]

163. Ingawa katika ufahamu wa Luther Wakristo wote ni makuhani, hakuwahesabu wote kuwa wachungaji. "Ni kweli kuwa Wakristo wote ni makuhani, lakini sio wote ni Wachungaji. Ili kuwa Mchungaji mhusika si lazima tu kuwa Mkristo na kuhani lakini lazima awe na ofisi na eneo la huduma ambalo amekabidhiwa kulitunza. Wito na agizo hili vinazalisha wachungaji na wahubiri." [27]

164. Dhana ya kitheolojia ya Luther kuwa Wakristo wote ni makuhani lilipingana na mpangilio wa jamii ambao ulikuwa umezoeleka katika miaka ya kati. Kwa mujibu wa Gratian, kulikuwa na aina mbili za Wakristo, Wakristo walei na waliobarikiwa.[28] Kwa fundisho lake la Ukuhani wa wote, Luther alikusudia kuondoa msingi wa mgawanyiko huu. Alivyo Mkristo kama Kuhani asili yake ni katika kujihusisha katika ukuhani wa Kristo. Mkristo analeta mahitaji ya watu katika maombi mbele za Mungu na matakwa ya Mungu kwa wanadamu kwa njia ya kueneza Injili.

165. Luther alielewa ofisi ya kiuchungaji kuwa huduma ya umma kwa kanisa zima. Wachungaji ni *ministri* (wahudumu). Ofisi hii haipo

---

[25] Luther, "Freedom of a Christian," tr. W. A. Lambert, Rev. Harold J. Grimm, katika *LW* 31:354; *WA* 7; 56, 35 -57, 1

[26] Luther, "Christian Nobility," katika *LW* 44:127; *WA* 6; 407, 22f.

[27] Luther, "Psalm 82," tr. C. M. Jacobs, katika *LW* 13:65; *WA* 31/1; 211, 17–20.

[28] Gratian, *Decr.* 2.12.1.7.

katika hali ya kupingana ukuhani wa wote waliobatizwa, lakini badala yake inawahudumia wote ili watu ambao ni Wakristo waweze kuwa makuhani wao kwa wao.

## Agizo la Mungu Katika Huduma

166. Kwa zaidi ya miaka 150, mojawapo ya majadiliano katika theolojia ya Kilutheri umehusu kama huduma ya kiuchungaji inategemea agizo takatifu au mgawanyo wa kazi kibinadamu. Hata hivyo, Luther anasema juu ya "ofisi ya kichungaji, ambayo Mungu ameianzisha ambayo lazima itawale juu ya usharika kwa mahubiri na sakramenti"[29]. Luther anaona kuwa asili ya ofisi hii ni katika mateso na kifo cha Kristo. "Nina tumaini, kwa hakika, waumini, wote wale ambao wanatamani kuitwa Wakristo, wanajua vizuri kabisa kuwa mamlaka haya ya kiroho limeanzishwa na kusimikwa na Mungu, si kwa dhahabu wala fedha ila kwa damu ya thamani na kwa kifo kichungu cha Mwana mpendwa wa Mungu, Bwana wetu Yesu Kristo (1 Pet.1:18-19). Kutoka kwenye majeraha yake kulifurika Sakramenti. [...] Alilipa kwa upendo ili watu kila upande wawe na ofisi hii ya kuhubiri, kubatiza, kufunga, kufungua, kushirikisha sakramenti, kufariji, kuonya, kuhimiza kwa Neno, na lolote linalohusiana na ofisi ya kiuchungaji.[...]. Hali ninayofikiria juu yake ni hasa ofisi ya kuhubiri na huduma ya Neno na sakramenti na ambayo inaeneza Roho na wokovu."[30] Kwa wazi, kwa hiyo, kwa Luther, Mungu ndiye mwasisi wa ofisi ya huduma.

167. Luther aliamini, hakuna hata mmoja, anayeweza kujiweka mwenyewe katika ofisi: mtu anapaswa kuitwa katika ofisi hii. Tangu 1535, ubarikio wa Wachungaji ulikuwa ukifanywa Wittenberg. Ubarikio ulifanyika baada ya uchunguzi wa mafundisho ya kiimani na maisha ya mhusika na kama aliitwa na usharika. Hata hivyo ubarikio haukufanyika katika usharika alipotoka mhusika ila ulifanyika mahali

[29] Luther, "To the Christian Nobility," Tr. C. M. Jacobs, Rev. J. Atkinson, katika *LW* 44, *WA* 6; 441, 24f.

[30] Luther, "A Sermon on Keeping Children in School," tr. Charles M. Jacobs, Rev. Robert C. Schulz, katika *LW* 46:219–20; *WA* 30/2; 526, 34; 527, 14–21; 528, 18f., 25–27.

pamoja Wittenberg, kwa mantiki kuwa ubarikio ulikuwa ni ubarikio kwa ajili ya huduma kwa kanisa zima.

168. Ubarikio ulifanyika kwa maombi na kuwekewa mikono. Kama maombi ya utangulizi kwamba Mungu atume watenda kazi kuvuna mavuno, (Mt. 9:38) na maombi ya Roho Mtakatifu, alivyoweka wazi, Mungu ndiye katika uhalisia ni mtendaji katika ubarikio. Katika ubarikio, wito wa Mungu unamshika huyu anayebarikiwa kikamilifu. Katika tumaini hili kwamba maombi yatajibiwa na Mungu, wito wa kwenda katika kazi ulifanyiwa kupitia Neno toka 1 Petro 5:2-4.[31] Moja ya taratibu za ubarikio unasema: "Ofisi ya kanisa ni kwa makanisa yote jambo kubwa na muhimu na kwamba Ofisi hii inatolewa na kuongozwa na Mungu peke yake".[32]

169. Kwa kuwa tafsiri ya Luther ya sakramenti ilikuwa kali kulinganisha na kawaida ya nyakati za miaka ya katikati, na kwa sababu alihisi sakramenti ya Wakatoliki ya madaraja ilihusu zaidi utaratibu wa msingi wa kafara ya ibada ya misa, Luther alisita kuona ubarikio kama sakramenti. Hata hivyo, Melanchton, alieleza katika ukiri wa Augsburg: "Ikiwa ubarikio wa wachungaji utafahamika kwa kurejea huduma ya Neno, hatuna upinzani kuita ubarikio wa wachungaji sakramenti. Kwa kuwa huduma ya Neno ina agizo kutoka kwa Mungu na ina ahadi kuu kama Warumi 1(:16) Injili ni uweza wa Mungu wa wokovu kwa yeyote aminiye. Aidha, Isaya 55(:11), '… ndivyo litakavyokuwa Neno langu litokalo kutoka kinywa changu: halitanirudia bure, bali litatimiza kile nililokusudia…' Kama ubarikio wa wachungaji unafahamika katika mtazamo huu, hatutaweza kupinga kuwa kuwekewa mikono ni sakramenti. Kanisa lina mamlaka ya kuchagua watumishi, ambao wanatufaa kabisa kwa sababu tunajua kuwa Mungu amethibitisha huduma hii na yupo katikati yake." [33]

---

[31] Ona the Wittenberger Ordinationszeugnisse, katika *WABr*12, 447–85.

[32] *WA* 38 423, 21–25.

[33] Apology XIII, "On the Number and Use of the Sacraments" 7, katika *BC*, 220.

## Ofisi ya Askofu

170. Kwa kuwa Maaskofu walikataa kuwabariki wafuasi wa matengenezo ya Kanisa kuwa wachungaji, Wanamatengenezo waliwabariki wachungaji wao kupitia wazee (wachungaji). Kifungu 28, cha ungamo la Augsburg kinalalamika kuhusu maaskofu waliokataa kubariki wachungaji. Hali hii iliwalazimu wanamatengenezo kuchagua kati ya kushikilia kanuni ya maaskofu kubariki wachungaji au kuwa waaminifu kuhusu kile wanachoelewa kuwa ukweli wa Injili.

171. Wanamatengenezo waliweza kufuata ubarikio wa wachungaji wa Kipresbiteri kwa sababu walijifunza kutoka kauli za Peter Lombard kuwa kanuni ya kanisa ilitambua utaratibu wa aina mbili tu, za Sakramenti, miongoni mwa taratibu kuu, udiakonia na uzee, na kwamba, kulingana na mafundisho yaliyoenea ya karne za kati, kusimikwa kwa kuwa askofu yenyewe haikuwa na tabia ya kisakramenti.[34] Wanamatengenezo kwa wazi walirejea kwa barua ya Jerome, ambaye alishawishika kwamba, kulingana na Agano Jipya, ofisi za wazee na askofu zilikuwa sawa pamoja na tofauti kwamba askofu ana haki ya kubariki watumishi wawe wachungaji. Kama Wanamatengenezo walivyoelewa, barua hii kwa *Evangelus* ilipokelewa kwenye *Decretum Gratiani*.[35]

172. Luther na Wanamatengenezo walisisitiza kwamba kuna ofisi moja tu ya kutegemea Ubarikio, ofisi ya kutangaza kwa wazi Injili na kushirikisha chakula cha Bwana, ambayo kwa asili yake ni tukio la umma. Hata hivyo, kutoka mwanzo kulikuwa na kutofautisha ofisi. Tangu ziara za kwanza, ofisi ya msimamizi mkuu ilianzishwa, ambayo ilikuwa na jukumu la pekee la kusimamia wachungaji. Philipp Melanchton

[34] Peter Lombard, *Sent*. IV, dist. 24, cap.12.

[35] Philipp Melanchthon alinukuu barua ya Jerome katika “De potestate et primatu papae tractatus,” katika *BC*, 340. Ona pia *WA* 2; 230, 17–9; Jerome, “Letter 146 to Evangelus,” katika J.-P. Migne (ed.), *Patrologia Latina* XXII (Paris, 1845), 1192–95; “Decretum Gratiani,” pars 1, dist. 93, katika E. Friedberg (ed.), *Corpus Iuris Canonici* (Graz, 1955), 327–29.

aliandika mwaka wa 1535: "Kwa sababu katika kanisa tunahitaji watawala, ambao wanawapima na kuwabariki kuwa wachungaji hao ambao wameitwa kuwa watumishi wa kanisa, sheria ya kanisa inafuatilia na kusimamia mafundisho ya mapadri (wahudumu wa neno). Na kama tusingekuwa na maaskofu ingetubidi tuwaunde."[36]

### *Maelezo ya Wakatoliki Kuhusiana Ukuhani wa Watu Wote na Upadre*

173. Wajibu na nafasi ya wale waliobatizwa kwa maisha ya kanisa havikutiliwa mkazo vya kutosha mwishoni mwa karne za kati. Hadi Mtaguso wa Pili wa Vatikani ndipo *magisterium* ilipowasilisha theolojia ya kanisa kama watu wa Mungu, na kuthibitisha "usawa wa kweli wa wote kuhusiana na nafasi na wajibu wa pamoja kwa waumini wote katika kuujenga mwili wa Kristo" (LC 32).

174. Kwenye mfumo huu Mkutano uliibua dhana ya ukuhani kwa watu wote waliobatizwa na kujadili uhusiano wake na huduma ya kikuhani. Katika theolojia ya Kikatoliki, mtumishi aliyebarikiwa kuwa mchungaji ameimarishwa kisakramenti kutenda katika Jina la Kristo lakini pia katika jina la kanisa.

175. Theolojia ya Kikatoliki imeshikilia kuwa ofisi ya Askofu inatoa mchango mkubwa katika umoja wa Kanisa. Wakatoliki wanauliza swali kwa vipi bila ofisi ya Askofu, umoja wa kanisa unaweza kudumishwa wakati wa ugomvi. Wanadai pia kuwa fundisho la Luther kuhusu Ukuhani wa wote waliobatizwa halikujali itifaki ya mfumo wa kanisa, ambao wanaamini umeanzishwa na Mungu mwenyewe.

---

[36] Melanchthon, "Consilium de moderandis controversiis religionis," katika C. G. Bretschneider (ed.), *Corpus Reformatorum*, vol. II (Halle: C. A. Schwetschke, 1895), 745f.; 1535).

## Majadiliano Kati ya Walutheri na Wakatoliki kuhusu Huduma

176. Majadiliano kati ya Walutheri na Wakatoliki umeainisha maeneo ambayo wanafanana na kutofautiana katika Theolojia na muundo wa ubarikio wa wachungaji, hususan kuwabariki wanawake, ambayo inafanywa na makanisa mengi ya Kilutheri. Maswali yaliyobakia ni kama kanisa la Kikatoliki laweza kutambua huduma ya makanisa ya Kilutheri. Kwa pamoja Walutheri na Wakatoliki wanaweza kuhusianisha wajibu wa kutangaza habari njema na kushirikisha sakramenti na ofisi ya kiuchungaji katika kazi hii. Kwa pamoja wanaweza kutofautisha kati ya wajibu kama za kiaskofu (episkope) na huduma katika ngazi ya chini (mtaa) na ngazi za juu zaidi (kanda/ jimbo) (*regional offices).*

### *Ufahamu wa Pamoja Kuhusiana na Huduma*

#### Ukuhani kwa Waliobatizwa

177. Swali linajitokeza kuhusu ni kwa jinsi gani upekee wa ofisi ya ubarikio kuwa mchungaji inahusishwa pote ulimwenguni na ukuhani wa wote waaminio waliobatizwa. Andiko la *Kitume la Kanisa* linaeleza, "Wakatoliki na Walutheri wapo kwenye maafikiano kuwa wote waliobatizwa ambao wanaamini katika Kristo, wanashiriki katika ukuhani wa Kristo na kwa pamoja wametumwa 'kutangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru ya ajabu' (1Petro 2:9). Kwa hivyo hakuna kiungo kinachokosa nafasi ya kutenda katika misioni ya mwili mzima" (ApC 273).

#### Asili ya Kimungu ya Huduma

178. Katika uelewa wa ofisi ya kiuchungaji kuna makubaliano ya pamoja kuhusu asili ya kimungu ya huduma hii: "Wakatoliki na Walutheri wanakubaliana kwamba Mungu ndiye aliyeanzisha huduma ya Kiuchungaji na kwamba ni ya muhimu sana kwa uwepo wa Kanisa, kwani Neno la Mungu na kutangazwa kwake katika neno na sakramenti ni vya lazima ili imani katika Kristo ikue na kudumishwa

na kwa pamoja ili kanisa liwepo na kudumishwa katika waamini wajengao mwili wa Kristo katika umoja wa imani" (ApC 276).

### Huduma ya Neno na Sakramenti

179. *Ukimitume wa Kanisa* (*The Apostolicity of the Church)* unatambulisha wajibu wa msingi wa watumishi waliobarikiwa kuwa wachungaji kwa Walutheri na Wakatoliki kwa pamoja kuwa ni kuhubiri Injili: "Watumishi waliobarikiwa kuwa wachungaji wana wajibu wa pekee katika kanisa kwa ujumla wake" (ApC 274). Kwa Wakatoliki na Walutheri "wajibu wa msingi na lengo la ubarikio wa mchungaji ni huduma ya hadhara ya neno la Mungu, Injili ya Yesu Kristo, ambalo Mungu wa Utatu ameliagiza kanisa kuhubiri kwa ulimwengu wote. Kila huduma na kila mtoa huduma atapimwa kwa malengo haya." (ApC 274)

180. Mkazo huu wa wajibu wa kuhubiri Injili, ni kwa wote Wakatoliki hata Walutheri (ling. ApC 247, 255, 257, 274). Wakatoliki wanaelekeza chanzo cha huduma ya kikuhani kwenye kuihubiri Injili. Agizo kuhusu Makuhani (*Presbyterorum Ordinis)* linasema: "Awali ya yote, watu wa Mungu huundwa na Neno la Mungu lililo hai, ambalo linatazamiwa litolewe kwa usahihi kabisa kupitia vinywa vya makuhani. Kwa kuwa hakuna anayeweza kuokolewa kabla hajaamini, jukumu la kwanza kabisa la makuhani ambao ni wanafanya kazi pamoja na maaskofu ni kuihubiri Injili ya Mungu kwa watu wote" (PO4, imepatikana ApC 247). "Pia Wakatoliki wanakiri kuwa ni jukumu la wahudumu waliobarikiwa kuwa wachungaji kuwakusanya watu wa Mungu kwa kutumia Neno la Mungu na kulihubiri kwa watu wote ili waamini" (ApC 274). Vile vile uelewa wa Kilutheri ni kuwa: "Huduma ina misingi na vigezo katika kuhubiri Injili kwa kusanyiko **lote** kwa namna ambayo ya inaweka msukumo wa kuhakikisha kuwa watu wanaamshwa na kuimarishwa kiimani" (ApC 255).

181. Walutheri na Wakatoliki pia wanaafikiana kwamba wajibu wa kutoa Sakramenti upo kwa kiongozi aliyebarikiwa kuwa mchungaji. Walutheri wanasema kwamba: "Injili inawapa wajibu wale waliokabidhiwa uongozi wa Kanisa kuhubiri Injili, kutangaza msamaha wa dhambi

na kutoa Sakramenti" (ApC 274).[37] Wakatoliki nao wanakiri kwamba, makuhani wamewekwa wakfu kwa kazi ya kutoa Sakramenti ambayo wanaamini "imefungamanishwa na Ekaristi" ambayo imeelekezwa kuwa "chanzo na upeo wa Injili yote iliyohubiriwa" (PO 5, cited in ApC 274.)

182. Andiko kuhusu msingi wa K*imitume wa Kanisa* linasema, "Ni muhimu kutambua vizuri kufanana kwa kazi za wazee wa Kanisa na zile Maaskofu. Mfumo ule ule wa sura tatu za huduma (yaani Mahubiri, Liturgia, Uongozi) umetumika kwa Maaskofu na wazee wa Kanisa. Na katika utendaji wa kanisa wazee wanatoa huduma za siku kwa siku wakati Maaskofu ni waangalizi wa mafundisho na ushirika katika jamii. Hata hivyo wazee wa kanisa hufanya huduma yao kwa kuwasaidia maaskofu wakiwa katika ushirika nao." (ApC 248)

## Kanuni ya Ubarikio wa Wachungaji / Mapadre

183. Kwa mujibu wa kanuni za kuingizwa katika huduma hii maalum, mambo yafuatayo yanahusishwa: "Kuingizwa katika huduma kunafanya kwa kubarikiwa ambapo Mkristo anakuwa ametengwa rasmi kwa huduma takatifu kwa kufanyiwa maombi, na kuwekewa mikono kwa huduma kuhubiri Injili katika neno na sakramenti. Maombi hayo ni kwa ajili ya kujazwa Roho Mtakatifu na vipawa vya kiroho na yanafanywa kwa imani (uhakika) kuwa yanasikiwa." (ApC 277)

## Huduma za Ndani na za Nje

184. Walutheri na Wakatoliki wanaweza kwa pamoja kusema kuwa tofauti ya madaraka katika huduma "ki-mtaa na ki-kanda, ni jambo muhimu sana linalojitokeza katika nia na shabaha ya kutoa huduma katika umoja wa Imani." (ApC 279). Kwa Makanisa ya Kilutheri, kazi ya uaskofu inatambulika katika mifumo tofauti. Kwa wale wanaotumia

[37] Akimnukuu Melanchton, Treatise on the Power and Primacy of the Pope, *BC,* 340: *BSLK*, 489, 30-35

utaratibu unaojumuisha sharika kadhaa *(Supra-Congregational Ministry)* wana jinsi wanavyowaita viongozi wao badala ya 'Askofu'. Majina hayo ni kama vile: Mwangalizi *(Ephorus)*, Rais *(Church president)*, Mkurugenzi *(Superintendent)* au Mchungaji wa Sinodi *(Synodal Pastor)*. Walutheri wanatambua kwamba, huduma ya Uaskofu inafanya kazi si tu kwa mtu binafsi bali katika mifumo mingine pia kama vile sinodi ambapo wachungaji na Wakristo wasio wachungaji hushiriki pamoja.[38]

### Msingi wa Kimitume

185. Pamoja na kwamba Walutheri na Wakatoliki wanatambua kwa njia tofauti kuhusu muundo wa ukimitume katika kanisa, wanakubaliana, "Uaminifu katika mahubiri ya kimitume ya Injili una kipaumbele katika *uhusiano wa Mapokeo, kupokezana Uongozi na Ushirika (Traditio, Successio na Communio) (ApC 291).* Wote wanakubaliana kuwa, "Kanisa ni la Kimitume kwa misingi ya uaminifu katika Mafundisho ya *Injili* ya Kimitume." (ApC 292). Makubaliano haya yana athari (matokeo) kwa uelewa wa Wakatoliki kuwa "wale wenye madaraka ya usimamizi ambao kwa Kanisa katoliki ni maaskofu" pia "wanahusika kipekee na mafundisho ya kimitume katika makanisa yao". Hivyo hawawezi kutengwa na "Jumuiya ambayo ukubali wake kwa mtizamo wa Kikatoliki ni ishara ya mafundisho yenye msingi wa Kimitume" (ApC 291).

### Huduma kwa Kanisa la Ulimwenguni Mwote

186. Walutheri na Wakatoliki wanakubaliana kuwa huduma wanayotoa ni kwa Kanisa kwa ujumla wake. Walutheri "wanachukulia kwamba kusanyiko la ibada lina uhusiano muhimu na kanisa la ulimwenguni"

---

[38] Mnamo 2007, Baraza la LWF liliasili "Huduma ya Maaskofu ndani ya Utume wa Kanisa: Taarifa ya Lund ya Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani - Ushirika wa Makanisa." Ingawa "haikusudiwi kuwa hati ya kimahakama," kifungu kinatafuta kufafanua kwa Ushirika wa Kilutheri maswali kadhaa kuhusu *episkopé*, kwa kuzingatia mapokeo ya Kilutheri na kwa matunda ya shughuli za kiekumene. Tazama **www.lutheranworld.org/lwf/index.php/affirms-historic-statement-on-episcopal-ministry.html**.

mwote na kuwa uhusiano huu ni wa msingi, si kitu cha juu juu (ApC 285). Pamoja na kwamba Maaskofu wa Kikatoliki "Hutawala sehemu ya watu wa Mungu ambao wamekabidhiwa na si Makanisa mengine au kanisa kwa ujumla wake," Kila Askofu analazimika "Kulitunza kanisa zima kwa ujumla wake" (LG 23). Askofu wa Rumi kwa madaraka yake ni " mchungaji wa Kanisa kwa Ujumla." (LG 22)

## *Tofauti Katika Uelewa wa Huduma*

### Uaskofu

187. Zipo tofauti katika uelewa wa huduma ya kanisa. *Ukimitume wa Kanisa* hukiri kwamba kwa Wakatoliki uaskofu ni huduma kamilifu ya mtumishi aliyebarikiwa kuwa mchungaji na hivyo huwa chanzo cha tafsiri ya kitheolojia kuhusu huduma katika kanisa. Andiko linanukuu *Lumen Gentium 21: "*Mafundisho ya kusanyiko takatifu yanakiri kwamba ukamilifu wa sakramenti ya madaraka ya huduma unatolewa na wakfu wa kiaskofu.... ambao unatoa pamoja na huduma ya kutakasa, huduma ya kufundisha na huduma ya kutawala. Hata hivyo, hali hii inaweza kufanya kazi kwenye jumuiya zinazofuata utawala wa ngazi (msonge) kati ya viongozi wakuu na wajumbe katika jopo la uongozi" (imenukuliwa katika ApC 243)

188. Mtaguso wa Pili wa Vatikani ulikazia mafundisho yake kwamba, "Maaskofu wanayo mamlaka kutoka kwa Mungu waliyopokea kutoka mitume kuwa wachungaji wa kanisa kana kwamba atakayewasikia wao, amemsikia Kristo na atakayewakataa wao amemkataa Kristo na yule aliyemtuma Kristo." (LG 20). Hata hivyo, Ni mafundisho ya Kikatoliki kwamba, "Askofu binafsi hawezi kuwa katika mnyororo wa kimitume kwa kuwa tu sehemu ya mfuatano wa kihistoria wa kuwekewa mikono wenye chanzo chake kwenye mmoja wa mitume. Badala yake; "Ni ushirika wa mfumo mzima wa maaskofu ambao wanachukua nafasi ya mitume na utume wao" (ApC 291).

189. Mtazamo wa namna hii kuhusu huduma ambao huanzia kwa Uaskofu, ni tofauti na msisitizo wa ukuhani katika Mkutano wa Trent

na unaonesha umuhimu wa mnyororo wa utume ingawa andiko la *Lumen Gentium* lilikazia utumishi katika mnyororo bila kukataa mafundisho ya kiimani, kiutume na kuwepo kwa urithi wa kiutume (ApC 240). Kwa sababu hii, Wakatoliki wametambulisha kanisa la wenyeji na Dayosisi wakizingatia mambo muhimu ya kanisa kuwa ni Neno, Sakramenti, na huduma ya kimitume ambayo huwakilishwa na askofu (ApC 284).

**Ukuhani**

190. Wakatoliki hutofautiana na Walutheri katika kutafsiri sakramenti ya ukuhani na uhusiano kati ya sakramenti ya ukuhani na ukuhani wa Kristo. Wanathibitisha kuwa, makuhani ni: "washiriki kwa hali ya pekee wa ukuhani wa Kristo, na kwa kubeba huduma hii takatifu hufanya kama watumishi wake ambaye kwa kupitia Roho wake, huduma ya kikuhani hufanyika kwa faida yetu katika Liturgia" (PO 5).

**Ukamilifu wa Alama ya Sakramenti**

191. Kwa Wakatoliki, ubarikio wa wachungaji wa Kilutheri umepungua ukamilifu wa alama ya sakramenti. Kwa mafundisho ya Kikatoliki, "kitendo na fundisho la urithi wa kimitume kwa maaskofu ni, pamoja na huduma tatu, sehemu ya ukamilifu wa muundo wa kanisa. Urithi huu huthibitika pale ambapo kwa umoja wao, maaskofu hupatiwa mafundisho ya uaskofu wa Katoliki na kupitia hayo hupewa nguvu ya kubariki wachungaji. Kwa hiyo ni mafundisho ya Kikatoliki kwamba katika makanisa ya Kilutheri alama ya sakramenti ya kubariki wachungaji haijakamilika kwa sababu hao wanaobariki watumishi kuwa wachungaji hawafanyi hivyo katika ushirika wa mafundisho ya maaskofu wa Kikatoliki. Kwa hiyo, Mtaguso wa Pili wa Vatikani unaeleza habari za *defectus sacramenti ordinis* (UR 22) kwa makanisa haya" (ApC 283)[39]

[39] Ona Randall Lee and Jeffrey Gros, FSC (eds), *The Church as Koinonia of Salvation: Its Structures and Ministries* (Washington, D.C.: United States Conference of Catholic Bishops, 2005), 49–50, §§107–109.

## Huduma Ulimwenguni Mwote

192. Mwisho, Wakatoliki na Walutheri hutofautiana katika wajibu na mamlaka ya huduma na Utawala nje ya ukanda. Kwa Wakatoliki, Papa ana "Nguvu na mamlaka yote juu ya kanisa" (LG 22). Muungano wa maaskofu pia una mamlaka kuu juu ya kanisa la ulimwenguni mwote, "pamoja na uongozi wa Papa huko Roma na hakuna kitakachowezekana pasipo uongozi huo" (LG 22). Ukimitume wa kanisa (*The Apostolicity of the Church)* unatambua mitazamo tofauti miongoni mwa Walutheri kuhusiana na "Uwezo wa vyombo vya uongozi juu ya makanisa binafsi na nguvu ya maamuzi yao" (ApC 287).

## Mitazamo Tofauti

193. Katika majadiliano mbalimbali, imegundulika kwamba uhusiano kati ya maaskofu na wazee wa kanisa mwanzoni mwa karne ya kumi na Sita haukueleweka kama ilivyoelezwa katika Mtaguso wa Pili wa Vatikani. Ubarikio wa wazee wa kanisa wakati wa Matengenezo ya kanisa ni lazima utazamwe kwa maelezo ya kipindi kile. Pia ni muhimu kujua kuwa wajibu wa viongozi wa Kikatoliki na wale wa Kilutheri ulihusiana kwa ukaribu sana.

194. Kihistoria, huduma ya Kilutheri imeweza kutimiza wajibu wa kudumisha kanisa katika kweli na hivyo kwa karibia miaka mia tano baada ya matengenezo iliwezekana kukiri kukubaliana kati ya Wakatoliki na Walutheri kwa ukweli wa msingi kuhusu Fundisho la Kuhesabiwa haki. Kama kulingana na maamuzi ya Mtaguso wa Pili wa Vatikani, Roho Mtakatifu hutumia "Kusanyiko la Kanisa" kama njia ya wokovu, ingeweza kuonekana kuwa kazi hii ya Roho ingalikuwa na maana ileile inayokubaliwa na pande zote mbili kuhusu huduma ya kanisa. Kwa hiyo, kuwepo kwa huduma hii kunawakilisha kwa wakati ule ule kikwazo kikubwa katika uelewa wa pamoja na pia uwezekano wa makubaliano.[40]

[40] Maswali haya pia yamechunguzwa na Őkumenischer Arbeitskreis evangelischer und katholischer Theologen; Kazi zao zimekusanywa katika *Das kirchliche Amt in apostolischer Nachfolge,* 3 vols (Freiburg: Herder and Göttingen: Vandenhoeck & Ruprecht, 2004, 2006, 2008).

## Maandiko Matakatifu na Mapokeo

### *Ufahamu wa Luther Kuhusu Maandiko Matakatifu, Tafsiri yake na Mapokeo ya Kibinadamu*

195. Mabishano yaliyotokea yakiunganishwa na kusambazwa kwa Hoja Tisini na Tano ya Luther kuhusu vyeti vya msamaha, kuliibua kwa haraka sana swali kwamba, ni mamlaka gani yanayoweza kumsaidia mtu wakati wa mapambano. Katika mahakama ya Papa, Mtheolojia Sylvester alidai katika jibu lake la kwanza kuhusu maandiko ya Luther juu ya Vyeti vya msamaha kuwa, "Yeyote asiyeyashika na kufuata mafundisho ya Kanisa la Kirumi na Papa kama mamlaka ya kiimani isiokosea ambapo ndipo Maandiko matakatifu yanapata nguvu na mamlaka: Huyo ni mzushi."[41] Na John Eck akamjibu Luther: "Maandiko matakatifu si halali bila mamlaka ya kanisa".[42] Hali ilibadilika na mara moja mgogoro ulizuka kutoka mabishano kuhusu maswali ya mafundisho ya msingi (Ufahamu sahihi wa Vyeti vya msamaha, kitubio na ondoleo la dhambi) na kuwa swali kuhusu mamlaka katika kanisa. Kwa habari ya mgogoro kati ya mamlaka mbalimbali, Luther aliweka mkazo wake kuwa Maandiko Matakatifu pekee ndiyo yenye nguvu na yamejithibitisha yenyewe kuwa na mamlaka na mamlaka nyingine zote zinapata nguvu kutoka kwake.

196. Luther alitambua Maandiko Matakatifu kama Kanuni ya kwanza *(primum principium)*[43] ambayo inapaswa kuwa msingi wa hoja zote za kitheolojia. Akiwa Mwalimu, mhubiri, Mshauri, na mjumbe wa mazungumzo hayo, alitumia theolojia kama tafsiri sahihi na ngumo (complex) ya Maandiko Matakatifu. Alishawishika kuwa Wakristo

---

[41] Sylvester Prierias, "Dialogue de potestate papae," katika P. Fabischand E. Iserloh (eds), *Dokumente zur Causa Lutheri (1517-1521)*, vol. I, (Münster: Aschendorff, 1988), 55.

[42] John Eck, "Enchiridion locorum communium adversus Lutherum et alios hostes ecclesiae (1525–1543)," katika P. Fraenkel (ed.), *Corpus Catholicorum* 34 (Münster: Ascendorff, 1979), 27.

[43] Ona *WA* 7; 97, 16–98, 16.

na Watheolojia wanapaswa si tu kulisoma Neno ila kuliishi na kudumu ndani yake. Aliliita "Hali ya Mungu ambapo hututunga mimba, hutubeba pia hutuzaa"[44]

197. Kwa Luther, njia sahihi ya kujifunza theolojia ni katika hatua tatu: *Oratio* [Maombi], *Meditatio* (Tafakuri), na *Tentatio* (Kuhisi maumivu yake).[45] Kumwomba Roho Mtakatifu awe mwalimu, Kulisoma Neno katika uwepo wa Mungu, katika Maombi pamoja na kutafakari hayo maneno yaliyomo ndani ya Biblia na kuwa msikivu ukizingatia hali ya maisha ambayo yanaonekana yakipingana na yale unayoyapata humo. Kwa kufanya hivyo, Maandiko Matakatifu hutuhakikishia mamlaka yake kwa kushinda Maumivu yote. Kama Luther alivyosema: "Tambua kuwa nguvu ya Maandiko Matakatifu ni hii, kwamba haibadilishwi na yule anayeyasoma bali humbadilisha yule anayeyapenda awe kama yanavyotaka na humpa nguvu yake."[46] Kwa uzoefu huo, imekuwa mara zote, mtu hatafsiri tu Maandiko bali Maandiko humtafsiri mtu na hapa ndipo Maandiko yanapothibitisha nguvu na mamlaka yake.

198. Maandiko Matakatifu ni ushuhuda wa ufunuo wa Mungu; hivyo mtheolojia anapaswa kuwa makini na kufuata njia ambayo Mungu amejifunua kwayo katika vitabu vya Biblia (modus loquendi scripturae). Vinginevyo, ufunuo wa Mungu hautakuwa umetambuliwa kwa uzito wake. Sauti mbalimbali za Maandiko zimejumuishwa katika Yesu Kristo "Ukimtoa Kristo kwenye Maandiko ni nini kinachosalia?"[47] Kinachomhusisha Kristo ni ule uwezo wa kukabili matatizo ya kisheria na mipaka ya sheria. Ni kipimo kilichojengwa kutoka Maandiko

[44] *WA* 10/1, 1; 232, 13–14.

[45] Luther, "Preface to the Wittenberg edition of Luther's German writings (1539)," tr. Robert R. Heitner, katika *LW* 34:285; *WA* 50; 559, 5–660, 16.

[46] Luther, "First Lectures on the Psalms," tr. Herbert J. A. Bouman, katika *LW* 10:332; *WA* 3; 397, 9–11).

[47] Luther, "Bondage of the Will," tr. Philip S. Watson with Benjamin Drewery, katika *LW* 33:26; *WA* 18; 606, 29.

yenyewe na katika hali kadhaa kimetumika kuchunguza kitabu kimoja kimoja mfano, mfano Waraka wa Yakobo.

199. Luther mwenyewe alitumia mara chache tu maelezo ya *"Sola scriptura"* na mtazamo wake mkuu ulikuwa: hakuna mamlaka inayoweza kudai kuwa juu ya Maandiko Matakatifu, na alikuwa kinyume kabisa na yeyote au chochote ambacho kinabadili au kupunguza chochote katika Maandiko Matakatifu. Lakini pamoja na msisitizo wake wa neno pekee, hakusoma Biblia peke yake, bali alirejea pia kwenye mazingira mbalimbali akiyahusianisha na maungamo yanayohusu Kristo na Utatu yaliyofanywa na kanisa la Kwanza ambayo kwake yalikazia malengo na maana ya Maandiko Matakatifu. Aliendelea kujifunza Maandiko kwa kutumia Katekisimo Ndogo na Kubwa ambazo alizitumia kama mafafanuzi ya Maandiko kwa ufupi alifanya mafafanuzi yake akirejea mababa wa kanisa hasa Agustino. Alikazia pia matumizi ya mafafanuzi ya kale na yale ya kifalsafa za wanadamu. Alifanya mafafanuzi yake ya maandiko katika mdahalo wa moja kwa moja na mawazo ya kitheolojia ya wakati wake na yale ya vizazi vya mwanzo. Kwake kusoma Biblia pamoja na jamii ya waaminio ndio msingi bora zaidi.

200. Kutokana na Martin Luther, Neno la Mungu halipingi mapokeo yote isipokuwa yale yanayoitwa mapokeo ya wanadamu. Kuhusiana na mapokeo hayo ya wanadamu anasema" Hatukubaliani na mafundisho ya wanadamu sio kwa sababu yamesemwa na wanadamu, bali kwa sababu ni ya uongo na kufuru dhidi ya Neno la Mungu. Neno la Mungu japokuwa limeandikwa na wanadamu sio la binadamu wala halikutoka kwa wanadamu bali limetoka kwa Mungu.[48] Akipima mamlaka nyingine swali la kumsaidia kufanya uamuzi la Luther alijiuliza kama mamlaka hiyo inakubaliana na Neno la Mungu au inasaidia kuleta ujumbe wa neno na kuufanya ueleweke vizuri zaidi katika mazingira fulani. Kutokana na Neno la Mungu kuwa ni wazi kwa mtazamo wa nje, maana ya Neno la Mungu inaweza

---

[48] *WA* 10/2; 92, 4–7.

kutambulika: Kutokana na Nguvu ya Roho Mtakatifu Neno la Mungu linaweza kuushawishi moyo wa mwanadamu kuhusu ukweli wake, uwazi wa ndani wa Neno la Mungu. Kwa msingi huo Neno la Mungu linajitafsiri lenyewe.

### *Mashaka ya Kikatoliki Kuhusu Neno la Mungu, Mapokeo na Mamlaka*

201. Wakati swali kuhusu kubainisha mapokeo na mamlaka ya Biblia lilipotokea, mkutano wa Trent pamoja na wanatheolojia wa wakati ule walijaribu kutoa majibu yanayoweka mapokeo na mamlaka ya kutafsiri Biblia katika mizani sawa. Uzoefu wa Wakatoliki ulibainisha kuwa maisha ya kanisa yaliendelezwa na kubainishwa na mambo mbalimbali hayarejei katika Biblia pekee. Mkutano wa Trent ulibainisha kuwa Biblia na mapokeo ya mitume ambayo hayakuandikwa ni vyombo vilivyobeba Injili. Hili linahitaji kutofautisha kati ya mapokeo ya mitume na mapokeo ya kanisa ambayo yana thamani lakini ambayo ni ya nafasi ya pili na ambayo yanaweza kubadilika. Wakatoliki walijali pia kuhusu hatari inayoweza kujitokeza kwa watu binafsi kufikia hitimisho la mafundisho makuu ya imani kwa kutafsiri Biblia wao wenyewe (bila mwongozo wa kanisa). Kutokana na tahadhari hiyo, mkutano wa Trent uliamua kuwa utafsiri wa Neno la Mungu ulipaswa uongozwe na mamlaka ya kufundisha ya kanisa.

202. Waalimu wa Kikatoliki, kwa mfano Melchior Cano alitoa hoja kuwa kutathmini mamlaka ya kufundisha ya kanisa ni kitu kigumu. Cano alianzisha mfumo wa vyanzo kumi, au vyanzo kumi vya theolojia ambapo aliweza kueleza kwa mfuatano kuhusu mamlaka ya Neno la Mungu, Mapokeo Simulizi, Kanisa la Kikatoliki, Mitaguso, Mababa wa Kanisa, Wasomi wa theolojia, Thamani ya Uumbaji, Uwezo wa fikra kama unavyofunuliwa na Sayansi, mamlaka ya wanafalsafa, na Mamlaka ya Historia. Mwisho alitathmini matumizi na manufaa ya vyanzo hivyo katika mijadala ya wasomi na wanatheolojia.[49]

---

[49] Melchior Cano, *De locis theologis,* Book 1, chap. 3 (Migne, *Theologiae cursus computus*1 [Paris, 1837]), col. 62.

203. Hata hivyo katika karne zilizofuata ulitokea utaratibu wa kutenga mamlaka ya kufundisha ya kanisa na vyanzo vingine vya theolojia ambapo mamlaka ya kufundisha ya kanisa ilikuwa ndiyo mamlaka pekee yenye neno la mwisho kuhusiana na tafsiri ya Biblia. Ilifika wakati mapokeo ya kanisa yakachanganywa na mapokeo ya mitume kiasi kwamba ilikuwa vigumu kutofautisha kati ya Mapokeo ya kanisa na mapokeo ya mitume kitu kilichosababisha mapokeo ya kanisa na mapokeo ya mitume yachukuliwe kama yana thamani sawa kwa imani ya Kikristo. Kulitokea pia ugumu wa uwezekano wa kukosoa mapokeo ya kanisa. Theolojia ya Mtaguso wa Pili wa Vatikani, kwa ujumla wake ina mtazamo wenye ulinganifu bora kuhusu mamlaka tofauti katika kanisa na uhusiano wa Biblia na mapokeo. Katika andiko la Mtaguso wa Pili wa Vatikani 'Dei Verbum' (DV. 10) Papa na Maaskofu walibainisha wazi kwa mara ya kwanza kuwa mamlaka ya mafundisho ya kanisa "hayako juu ya Neno la Mungu bali inasimama katika kulihudumia Neno."

204. Nafasi ya Neno la Mungu katika maisha ya kanisa ilikazwa wakati wa Mtaguso wa Pili wa Vatikani uliposema "msukumo na nguvu ya Neno la Mungu ni mkubwa sana kiasi kwamba linasimama kama nguzo na nguvu ya kanisa, kama nguvu ya imani kwa watoto wake, kama chakula cha roho, kama chanzo kikamilifu na kinachodumu cha maisha ya kiroho" (DV 21).[50] Kwa hiyo waamini wanaaswa kujizoeza kusoma Biblia, ambayo Mungu huzungumza nao, pamoja na kuomba (DV 25).

205. Majadiliano ya kiekumeni yamesaidia Walutheri na Wakatoliki kufikia kwenye mitazamo tofauti ya hoja maalumu za rejea na mamlaka ambazo zimesaidia katika mchakato wa utambuzi wa Imani ya Kikristo maana ya jinsi ambavyo imani hiyo inapaswa iumbe maisha ya kanisa.

[50] **www.vatican.va/archive/hist_councils/ii_vatican_council/documents/vat-ii_const_19651118_dei-verbum_en.html**.

### ***Majadiliano ya Wakatoliki – Walutheri Kuhusu Neno la Mungu na Mapokeo***

206. Matokeo ya kurejea kwenye Biblia yaliyosababisha kuandikwa kwa andiko Imani la *Dei Verbum* la Mtaguso wa Pili wa Vatikani, yamewezesha uelewa mpya wa kiekumeni wa nafasi na umuhimu wa Neno la Mungu. Andiko la kiekumeni la *Utume wa Kanisa* linasema "Mafundisho ya Kikatoliki hayana tena kile ambacho theolojia ya matengenezo ilikiogopa na kutaka kwa gharama yoyote kukikwepa ambacho ni asili ya mamlaka yasiobadilika ya maandiko matakatifu ya kikanoni yaliyotoka kwenye mfumo msonge wa kanisa uliotambulisha Kanoni. (ApC 400)

207. Katika majadiliano, Wakatoliki wamesisitiza uelewa ambao Wanamatengenezo pamoja na Wakatoliki wanakubaliana kwa pamoja kwa mfano upekee wa uvuvio wa maandiko yaliyo katika Biblia "katika kueneza ukweli uliofunuliwa unaounda, akili na moyo kama inavyothibitishwa katika 2Timotheo 3:17 na kusemwa katika Mtaguso wa Pili wa Vatikani (Dv 21-25)" (ApC 409). Wakatoliki wanaendelea kusema kwamba, "ukweli huu umekuwa ukifanya kazi katika kanisa kwa muda mrefu sio tu kwa mwamini mmoja mmoja bali hata katika mapokeo ya kanisa. Na hili linadhihirika kwa pamoja katika mafundisho makuu ya imani kwa mfano sheria ya imani, kiri za imani na mafundisho mengine ya msingi ya kanisa, na pia katikamfumo mzima wa kuabudu… Neno la Mungu limeingia lenyewe kwenye mapokeo ambayo yameweza kuchukua nafasi muhimu katika utafsiri wake. Mtaguso wa Pili wa Vatikani hausemi kuwa mapokeo yameleta kweli fulani nje ya Biblia bali mapokeo yanaonesha ukweli kuhusu ufunuo unaosemwa na Biblia. (*ApC 410)*

208. Tunda la majadiliano ya kiekumeni kwa theolojia ya Kilutheri utayari wa kupokea msimamo wa Wakatoliki kuwa Neno la Mungu liko kazini sio tu kwa mtu mmoja mmoja, bali kwa kanisa zima pia. Ushahidi wa hili uko wazi katika kiri za Kilutheri katika makanisa ya Kilutheri.

## Neno la Mungu na Mapokeo

209. Leo nafasi na umuhimu wa Neno la Mungu na mapokeo yanaeleweka kwa tofauti sana katika kanisa la Katoliki kuliko ilivyokuwa inaeleweka na wapinzani wa theolojia ya Luther. Kuhusiana na usahihi wa tafsiri ya Neno la Mungu, Wakatoliki wameeleza kuwa, "Wakati mafundisho ya kanisa katoliki yanaposema kwamba maamuzi ya kanisa yana umuhimu katika usahihi wa tafsiri ya Neno la Mungu, haimaanishi Papa na Maaskofu peke yao wameshikilia mamlaka ya kutafsiri Neno la Mungu jambo ambalo Wanamatengenezo ya kanisa waliliogopa na kulikataa. Hata kabla ya matengenezo ya kanisa, watu mashuhuri walikuwa wameonesha kuwa ndani ya kanisa kulikuwepo watafsiri mbalimbali... wakati wa Mtaguso wa Pili wa Vatikani wa II ulipoongea kuhusu kanisa kuwa na maamuzi ya mwisho (DV 12) ni wazi kuwa mtaguso huo ulikwepa mtazamo kuwa Papa na Maaskofu ndio chombo pekee cha kutoa tafsiri sahihi ya Neno la Mungu na hoja hii imethibitishwa na idara kongwe ya uenezi wa kusoma Biblia na utambuzi wa DV 12 kuhusu nafasi ya tafsiri ya Biblia kwa kutumia mbinu za kisasa katika kuboresha tafsiri zinazotolewa na mamlaka ya mafundisho ya kanisa. (*ApC* 407).

210. Kwa hiyo Walutheri na Wakatoliki kwa pamoja wanaweza kuhitimisha, "kwa hiyo kuhusu Neno la Mungu na mapokeo, Walutheri na Wakatoliki wanakubaliana kwa sehemu kubwa sana kwamba mikazo yao tofauti yenyewe haipaswi kuendelea kuleta mpasuko wa makanisa. Katika eneo hili kuna umoja katika maridhiano ya kutofautiana." (*ApC* 448)[51]

---

[51] Masuala haya pia yamechunguzwa nchini Ujerumani na Ökumenischer Arbeitskreis evangelischer und katholischer Theologen; kazi yao inapatikana katika W. Pannenberg and Th. Schneider (eds), *Verbindliches Zeugnis*, 3 vols (Freiburg: Herder and Göttingen: Vandenhoeck & Ruprecht, 1992, 1995, 1998).

### *Kuangalia Mbele: Injili na Kanisa*

211. Pamoja na kuwapa Wakatoliki uelewa wa theolojia ya Martin Luther, majadiliano ya kiekumeni, pamoja na historia na tafiti za kitheolojia, vinawapa wote pamoja Walutheri na Wakatoliki uelewa wa pamoja kuhusu mafundisho ya kila mmoja, hoja wanazokubaliana na hoja zinazohitaji majadiliano zaidi. Hoja kuhusu kanisa ni miongoni mwa hoja muhimu katika majadiliano haya.

212. Asili ya kanisa ni miongoni mwa hoja zilibishaniwa wakati wa Matengenezo ya kanisa. Hoja ya msingi ilikuwa uhusiano kati ya wokovu na kanisa, ambavyo vyote hupokea na kueneza Neema ya Mungu kwa Neno na sakramenti. Uhusiano kati ya Injili na kanisa ilikuwa hoja ya kwanza kujadiliwa katika majadiliano ya kimataifa kati ya Walutheri na Kanisa la Kikatoliki Kirumi. Kutokana na majadiliano hayo taarifa ya Malta, pamoja na machapisho kadhaa ya kiekumeni yaliyochapishwa baadaye yamewezesha leo kuwa na uelewa bora kuhusu misimamo ya Walutheri na Wakatoliki na kuweza kubainisha hoja wanazokubaliana na hoja zinazohitaji kufanyiwa kazi zaidi.

### Kanisa kulingana na Mapokeo ya Kilutheri

213. Kwa mapokeo ya Kilutheri, kanisa linaeleweka kama, “kusanyiko la watakatifu ambapo Injili inahubiriwa kwa usafi na sakramenti zinatolewa kwa usahihi” (CA VII). Hii inamaanisha kwamba maisha ya kiroho ya mtaa/usharika yanategemea mimbara na madhabahu. Hii inajumuisha mtazamo wa kanisa la kiulimwengu wote kwa kuwa kila kusanyiko limeunganishwa na makusanyiko mengine kwa mahubiri safi na kusherehekewa kwa usahihi sakrament kwani mahubiri na sakrament ndizo zinaanzisha huduma katika kanisa. Ni vizuri kukumbuka kuwa Luther katika Katekisimo yake kubwa aliita kanisa “mama anayebeba mimba na kumzaa kila Mkristo kwa Neno la Mungu ambalo Roho Mtakatifu analifunua na kulitangaza. . . Roho Mtakatifu atabaki na jumuiya takatifu au Wakristo mpaka mwisho

wa dahari. Kupitia yeye hutuvuta kwenda kwa Kristo akimtumia (Roho) kufundisha na kuhubiri Neno.“[52]

### Kanisa Kulingana na Mapokeo ya Kikatoliki

214. Mafundisho ya Mtaguso wa Pili wa Vatikani katika *Lumen Gentium* ni wa muhimu katika uelewa wa Wakatoliki kuhusu kanisa. Mababa wa mtaguso walieleza nafasi ya kanisa katika historia ya wokovu kwa msingi wa Sakramenti: “ Kanisa liko ndani ya Kristo kama sakrament au kama alama na chombo vyote vikiwa karibu kuungana na Mungu na umoja wa wanadamu wote” (LG1).

215. Dhana ya msingi ya kueleza uelewa wa kanisa kama sakramenti inajirudia katika uelewa siri na inathibitisha dhana ya uhusiano usiogawanyika wa kanisa linaloonekana na lisiloonekana. Mababa wa mtaguso huu walifundisha: “Kristo, mpatanishi pekee, alianzisha na anaendelea kulitunza kanisa lake takatifu hapa duniani, ushirika wa waaminio, tumaini na upendo, kama kitu kinachoonekana ambacho kwacho huwasilisha kweli na neema kwa wote. Lakini jamii iliyoundwa katika mifumo ya taasisi msonge na mwili wa utukufu wa Kristo, hazipaswi kuonwa kama vitu viwili, wala kusanyiko linaloonekana na jumuiya ya kiroho, wala kanisa la duniani na kanisa lililopewa zawadi za mbingu, bali zinaunda kitu kimoja cha kweli kilichoungana chenye vipashio vya kiungu na kibinadamu.“ *(LG 8)*

### Kuelekea Maridhiano

216. Katika majadiliano kati ya Walutheri na Wakatoliki maridhiano ya wazi yamefikiwa kuwa fundisho la kuhesabiwa haki na fundisho la kanisa yanakwenda pamoja. Uelewa huu wa pamoja umeelezwa katika chapisho la *Kanisa na Kuhesabiwa Haki*: “ Wakatoliki na Walutheri kwa pamoja wanakiri kuhusu wokovu unaopatikana kwa Yesu tu kwa Neema tu na unapokelewa kwa imani. Wanakiri Ukiri

---

[52] Luther, “Large Catechism,” katika *BC*, 436–38 (tafsri imebadilishwa); *BSLK* 665, 3–6; 667, 42–46.

mmoja, wakisema ‘Kanisa moja takatifu la ulimwengu wote na la kimitume’. Vyote kwa pamoja, kuhesabiwa haki kwa mwenye dhambi na kanisa ni mafundisho makuu ya imani (*Church and Justification,4*).

217. Andiko la *Church and Justification (Kanisa na Kuhesabiwa Haki)* linaeleza pia kwamba: “Kwa hakika na kwa usahihi kabisa tunasema hatuamini katika kuhesabiwa haki na hatuamini katika kanisa bali tunaamini katika Baba mwenye rehema kwetu na ambaye anatukusanya katika kanisa tukiwa watu wake, na tunaamini katika Kristo anayetuhesabia haki na ambaye kanisa ni mwili wake, na tunaamini katika Roho Mtakatifu anayetutakasa na kukaa ndani ya Kanisa. Imani yetu inajumuisha kuhesabiwa haki na kanisa kama kazi ya Mungu wa Utatu ambayo inapokelewa kwa usahihi tu kwa kuwa na imani kwa Mungu wa Utatu“ (*Church and Justification*, 5).

218. Pamoja na kuwa chapisho la *Kanisa na Kuhesabiwa Haki* na chapisho la *Utume wa Kanisa* yametoa mchango mkubwa kwenye hoja kadhaa ambazo hazijapata ufumbuzi kati ya Wakatoliki na Walutheri, bado majadiliano ya kiekumeni yanahitajika kwenye: uhusiano wa kanisa linaloonekana na lisilooneka na uhusiano uliopo kati ya kanisa la wenyeji (mahali fulani) na kanisa la ulimwenguni kote, kanisa kama sakramenti, umuhimu wa uwekaji wakfu wa sakramenti kwa maisha ya kanisa, na dhana ya kisakramenti katika kuweka wakfu watumishi. Majadiliano ya baadaye yanapaswa yazingatie kazi muhimu ambazo zimeshafanyika katika machapisho haya na mengine muhimu. Kazi hii ni ya muhimu sana kwani Wakatoliki na Walutheri hawakuwahi kuacha kukiri pamoja imani katika “kanisa moja takatifu la ulimwengu wote na la kimitume.”

# Mlango wa V

## Wito wa Maadhimisho ya Pamoja

### Ubatizo: Msingi wa Umoja na Maadhimisho ya Pamoja

219. Kanisa ni mwili wa Kristo. Kama ambavyo Kristo ni mmoja tu, vivyo hivyo Kristo ana mwili mmoja tu. Kwa njia ya ubatizo, wanadamu wanafanywa viungo vya mwili wa Kristo.

220. Mtaguso wa Pili wa Vatikani unafundisha kwamba, watu waliobatizwa na kumwamini Kristo, lakini sio wa Kanisa la Katoliki – wamehesabiwa haki kwa njia ya Imani katika ubatizo na ni viungo vya mwili wa Kristo na wana haki ya kuitwa Wakristo, na wanakubalika kama ndugu na watoto wa Kanisa la Katoliki. (*UR 1.3*) [1] Walutheri wanakiri vivyo hivyo kwa Wakristo wenzao.

221. Kwa kuwa Wakatoliki na Walutheri wanaunganishwa pamoja katika mwili wa Kristo, kama viungo vyake, inakuwa kweli kwao asemayo Paulo katika barua I Kor. 12 :26 "Na kiungo kimoja kikiumia, viungo vyote huumia nacho, na kiungo kimoja kikitukuzwa, viungo vyote hufurahi pamoja nacho." Kinachoweza kudhuru sehemu moja ya mwili, mwili wote huumia pamoja. Kwa mtizamo huu, wakati Wakristo wa Kilutheri wanakumbuka tukio fulani lililosababisha kuwepo kwao, hawapendi kufanya hivyo bila Wakristo wenzao wa Kanisa la Katoliki. Wanapokumbuka kwa pamoja mwanzo wa matengenezo, wanaujali ubatizo wao vema.

[1] **www.vatican.va/archive/hist_councils/ii_vatican_council/documents/vat-ii_decree_19641121_unitatis-redintegratio_en.html**.

222. Kwa kuamini kuwa ni sehemu ya mwili mmoja wa Kristo, Walutheri wanasisitiza kuwa Kanisa lao halitokani na matengenezo au limekuwepo miaka 500 iliyopita tu bali wanasisitiza kuwa Kanisa la Kilutheri linaasilika katika tukio la Pentekoste na toka mahubiri ya Mitume. Kanisa hili limepata muundo wake, kupitia mafundisho na nguvu za wanamatengenezo. Wanamatengenezo hawakuwa na matumaini ya kuanzisha Kanisa jipya na kulingana na ufahamu wao wenyewe hawakufanya hivyo, walihitaji kuleta matengenezo ya Kanisa, na walifaulu kufanya hivyo ndani ya ushawishi wao, japo katika hali ya makosa na mapungufu.

### *Maandalizi ya Maadhimisho*

223. Kama mwili mmoja, Wakatoliki na Walutheri wanakumbuka kwa pamoja - matukio ya matengenezo yaliyoleta hali ya maisha ya utengano kwa jamii hizi hata kama bado ni mwili mmoja. Hali halisi hii haikubaliki na ni chanzo cha maumivu makubwa. Kwa kuwa wao ni sehemu ya mwili mmoja, Wakatoliki na Walutheri wanapambana katika mafarakano yao kuufuatilia umoja wa Kanisa moja duniani. Mapambano haya yana sura mbili. Kwanza, kutambua kile wanachoshiriki na kuwaunganisha, na pili kutambua ni nini kinachowatenganisha. Hili kwanza ni la kishukrani na furaha na hilo la pili ni la maumivu na masikitiko.

224. Mwaka 2017, wakati Walutheri wanasherekea maadhimisho ya mwanzo wa matengenezo, hawasherehekei mgawanyo wa Kanisa la Magharibi. Hakuna mwanatheolojia mwajibikaji anayeweza kusherekea utengano wa Wakristo.

### Kushiriki Furaha ya Injili

225. Walutheri wanashukuru kwa moyo kwa lile alilolifanya Luther na Wanamatengenezo wengine. Ufahamu wa Injili ya Yesu Kristo na imani katika Yesu Kristo, ufahamu wa fumbo la Mungu wa utatu kujitoa mwenyewe kwetu wanadamu kwa neema yake, ambapo tunaweza kumpokea tu kwa kumwamini katika ahadi yake; Uhuru

na uhakika vinavyoletwa na Injili; katika upendo upatikanao na kuhusishwa kwa imani, na katika matumaini la maisha na kifo; na katika kuishi maisha ya neno, Katekisimo na nyimbo zinazohuisha imani. Kumbukumbu na maadhimisho haya yataongeza sababu za shukrani. Shukrani hii ndiyo inayowafanya Walutheri kufanya maadhimisho Mwaka 2017.

226. Walutheri wanatambua pia kwamba kumshukuru Mungu sio kitu wanachoweza kumiliki wenyewe, wangependa kushirikiana na Wakristo wengine wote kumshukuru Mungu. Hivyo wanawakaribisha Wakristo wote kusherehekea pamoja. Kama tulivyoona nyuma, Wakatoliki na Walutheri wana mambo mengi ya pamoja na hivyo wanaweza kumshukuru Mungu pamoja hasa siku ya matengenezo ya Kanisa.

227. Hili linaleta msukumo ambao Mtaguso wa Pili wa Vatikani unaeleza; "Wakatoliki, ni lazima kuwakubali kwa furaha na kwa heshima karama za kikristo toka urithi wetu ambazo zinapatikana kati ya ndugu zetu waliojitenga. Ni sahihi na inafaa kutambua utajiri wa Kristo na kazi mbalimbali katika maisha ya wengine wenye ushuhuda wa Kristo wakati mwingine hata kwa kumwaga damu yao. Kwa kuwa Mungu ni wa ajabu wakati wote katika kazi zake na anastahili sifa zote.

## Sababu za Kujuta na Kuomboleza

228. Kama vile maadhimisho ya 2017 yanavyodhihirisha furaha na shukrani, vivyo hivyo ni lazima yatoe mwanya kwa Wakatoliki na Walutheri kuhisi maumivu ya kushindwa na hatia, makosa na dhambi za watu na matukio yanayokumbukwa.

229. Katika tukio hili Walutheri pia watakumbuka maazimio matata na ya udhalilishaji yaliyotamkwa na Martin Luther dhidi ya Wayahudi. Wanatambua ni maazimio ya aibu na watayajutia, Walutheri kwa moyo wa toba wanatambua mateso ya Waanabaptisti (wapinga ubatizo wa mtoto) waliyofanyiwa na mamlaka ya Walutheri na Martin Luther na Philip Melancthon walihimiza mateso haya katika theolojia zao. Walutheri wanajutia vurugu kwa wakulima wadogo yaliyofanywa na

Luther wakati wa vita vya wakulima. Ufahamu wa upande mbaya wa Martin Luther na matengenezo. Vimehamasisha Watheolojia wa Kilutheri kujikosoa na kumkosoa Martin Luther na matengenezo ya Wittenberg. Pamoja na kuwa wanakubali kwa sehemu upinzani wa Luther juu ya papa, hata hivyo Walutheri wa leo wanakanusha kumhusisha Papa na mpinga Kristo.

**Sala ya Umoja**

230. Kwa kuwa Yesu Kristo kabla ya kifo chake alimwomba Baba ''wawe na umoja'', ni dhahiri kuwa mgawanyo wa mwili wa Kristo ni kinyume na mapenzi ya Bwana. Ni mgawanyo kinyume pia cha maelekezo ya Kitume katika Efeso 4: 3 – 6 muwe na "kujitahidi kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani. Mwili mmoja, na roho mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu. Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja. Mungu mmoja, naye ni Baba wa wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote." Mgawanyiko wa mwili wa Kristo ni kinyume na mapenzi ya Mungu.

**Tathmini ya Mambo yaliyopita**

231. Wakati Wakatoliki na Walutheri wanakumbuka migongano ya Kitheolojia na matukio ya karne ya 16 kwa mtizamo huu, lazima wajali mazingira ya Karne ya 16. Walutheri na Wakatoliki hawawezi kulaumiwa kwa kila kitu ambacho kilitokea kwa wakati ule, kwa kuwa matukio mengine ya Karne ya 16 yalikuwa juu ya uwezo wao. Katika Karne hii, ushawishi wa Kitheolojia na siasa ya kiutawala ziliingiliana mara kwa mara. Wanasiasa wengi walitumia mawazo ya Kitheolojia kufikia malengo yao, wakati wanatheolojia wengi walisukuma mitazamo yao kwa njia ya kisiasa. Katika mazingira haya tata, sio rahisi kumlaumu mtu fulani kwa jambo moja fulani na kumwita mkosaji au kumweka upande wa wakosaji.

232. Mgawanyo wa karne ya 16 uliasilika kwenye tofauti za uelewa wa kweli ya imani ya Kikristo na ulileta ubishi kwa kuwa wokovu ulionekana kuwa hatarini. Pande zote mbili zilishikilia msimamo wa kitheolojia

ambao hawakuweza kuuacha. Mmoja hawezi kumlaumu mwingine kwa kufuata dhamiri yake, wakati Neno la Mungu na mijadala ya wengine imezingatiwa.

233. Jinsi Watheolojia walivyowasilisha ushawishi wao wa Kitheolojia katika vita kwa mawazo ya wengi ni jambo jingine kabisa. Katika karne ya 16, Wakatoliki na Walutheri mara kwa mara si tu hawakuelewana, lakini pia walitia chumvi na kuwafanyia mzaha wapinzani wao ili kuwafanya waonekane kama hawafai. Mara kwa mara walivunja amri ya nane inayokataza kumshuhudia jirani uongo. Hata kama wapinzani walikuwa na busara wao kwa wao wakati mwingine, utayari wao kumsikiliza mwingine na kujali jambo lake haukuwa toshelevu. Wapinzani walitaka kupuuza na kushinda adui zao, mara nyingi kwa makusudi wakizidisha malumbano badala ya kutafuta suluhisho kwa kuangalia mambo yaliyowaunganisha. Chuki na tofauti zilichukua nafasi katika kutangaza upande mmoja fulani. Upinzani ulijengwa na kurithishwa kwa vizazi vilivyofuata. Hapa pande zote zina sababu ya kujuta na kuomboleza namna walivyoendesha majadiliano yao. Wakatoliki na Walutheri pamoja wanachukua dhambi ambayo itahitaji kutubiwa waziwazi katika kumbukumbu ya matukio ya miaka 500 iliyopita.

## Toba ya Wakatoliki dhidi ya Umoja

234. Katika ujumbe wake kwa mkutano wa Nürnberg 25/11/1522, Papa Handriani VI tayari alilalamika dhidi ya ukatili na makosa ya mamlaka ya Kanisa. Baadaye sana wakati wa karne iliyopita, Papa Paulo VI katika hotuba ya ufunguzi katika kipindi cha pili cha Mtaguso wa Pili wa Vatikani, aliomba radhi kwa Mungu na ndugu wa mashariki, waliotengwa. Tendo hili la Papa linaelezwa katika mkutano wenyewe, zaidi ya yote katika kanuni ya Uekumeni[2] na katika viapo juu ya uhusiano wa Kanisa na dini zingine. (*Nostra Acetate)* [3]

---

[2] «Kwa hiyo kwa unyenyekevu tunaomba msamaha kwa Mungu na kwa ndugu zetu waliotengwa, kama sisi tunavyowasamehe wanaotukosea» (*UR* 7)

[3] "Zaidi ya hayo, katika kukataa kwake kila aina ya mateso dhidi ya mtu ye yote, Kanisa, likikumbuka

235. Katika mahubiri ya Kwaresima, siku ya msamaha, Papa John Paulo II vile vile alikubali dhambi na alifanya maombi ya toba kama sehemu ya utekelezaji wa mwaka mtakatifu 2000. [4] Alikuwa wa kwanza sio tu kurudia majuto ya mtangulizi wake Paulo VI na mababa wa mkutano kuhusu kumbukumbu ya maumivu hayo, lakini pia kuchukua hatua kuhusu kumbukumbu hizi. Aliuhusisha pia maombi ya msamaha na ofisi ya Askofu wa Rumi. Katika maandiko yake *Ut unum sint (ili wawe na umoja)* anaeleza ziara yake kwenye mkutano wa Makanisa duniani Geneva 12 Juni 1984. Hapa anakiri kuwa msimamo wa Kikatoliki kutunza umoja wa Kanisa katika huduma ya Askofu wa Rumi (*ni Papa)* kwenye uaminifu kuhusu mapokeo ya kimitume na imani ya mababa, ushawishi huu wa umoja umesababisha ugumu kwa Wakristo wengine wengi, ambao kumbukumbu zao kuhusu mambo haya zina maumivu. Hivyo aliongeza kusema "Kiasi tulichokosea hapa, najiunga na watangulizi wangu Paulo VI kuomba msamaha."[5]

## Toba ya Walutheri Dhidi ya Umoja

236. Kwenye Mkutano wake wa 1970 Evian, Fungamano la Makanisa ya KilutheriDuniani lilitamkwa kwa mujibu wa uwasilishaji, wa Johannes Cardinal Willebrand. "Kuwa sisi kama Wakristo wa Kilutheri na washarika tumejiandaa kukubali kuwa hukumu ya Wanamatengenezo dhidi ya kanisa la Kirumi na theolojia haikuwa tu bila malumbano yenye uharibifu, ambapo kwa sehemu umefanywa hata leo. Tunaomba radhi kwa kweli kwa kosa na kutofahamiana ambapo alama za malumbano haya ziliwagusa ndugu zetu wa Katoliki. Tunakumbuka kwa shukrani maelezo ya Papa Paulo VI

---

urithi linaoushiriki na Wayahudi na kuchochewa si kwa sababu za kisiasa bali na upendo wa kiroho wa Injili, linashutumu chuki, mateso, maonyesho ya chuki dhidi ya Usemitiki, unaolekezwa dhidi ya Wayahudi wakati wowote na mtu yeyote" (*NA* 4).

[4] John Paul II, "Day of Pardon," 12 March 2000, katika **www.vatican.va/holy_father/john_paul_ii/homilies/2000/documents/hf_jp-ii_hom_20000312_pardon_en.html**.

[5] John Paul II, *Ut Unum Sint,* 25 May 1995, 88.

kwenye Mtaguso wa Pili wa Vatikani ambapo aliwasilisha ombi lake la msamaha kwa kosa lolote lililosababishwa na Kanisa Katoliki. Kama ilivyo kwenye sala ya Bwana Wetu Yesu Kristo, tujitahidi kuwa wazi, waaminifu na wahisani katika majadiliano yetu yote."[6]

237. Walutheri pia walikiri makosa yao dhidi ya Wakristo wa tamaduni zingine. Katika mkutano wake wa kumi na moja wa 2010 huko Stuttgart Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani walitangaza "wamejawa na hali ya toba na maumivu juu ya mateso kwa Waanabaptisti (wapinga ubatizo) yaliyofanywa na mamlaka ya Kilutheri na haswa juu ya ukweli kuwa Theolojia ya Wanamatengenezo ya Kilutheri walihimiza mateso hayo. Hivyo Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani... lingependa kutangaza hadharani majuto na masikitiko yao. Tukimwamini Mungu ambaye katika Yesu Kristo aliupatanisha ulimwengu na yeye mwenyewe, tunaomba msamaha - toka kwa Mungu na toka kwa kaka na dada wa Wamennonites - kwa maumivu ambayo watangulizi wetu katika Karne 16 waliyafanya kwa Waanabaptisti (wapinga ubatizo), kwa kusahau au kupuuza mateso haya katika karne hizi, na kwa namna isiosahihi, inayopotosha na kuumiza ya kuwaelezea (hurtful portraits) Waanabaptisti (wapinga ubatizo wa watoto na kubatiza tena) na Wamennonites iliofanywa na Walutheri, kwa wazi na kitaaluma, hadi siku hii."[7]

---

[6] Jan Willebrands, "Lecture to the 5th Assembly of the Lutheran World Federation, on 15 July 1970," katika *La Documentation Catholique* (6 September 1970), 766.

[7] "Action on the Legacy of Lutheran Persecution of 'Anabaptists,'" katika **www.lwf-assembly.org/uploads/media/Mennonite_Statement-EN_04.pdf**.

# Mlango wa VI

## Maazimio Matano ya Pamoja

238. Wakatoliki na Walutheri wanatambua kuwa wao ni mwili mmoja wa Kristo katika imani kwenye jamii wanamoishi. Uelewa umechomoza miongoni mwa Wakatoliki na Walutheri kuwa malumbano ya karne ya 16 yamefika mwisho. Sababu za kila mmoja kuhukumu imani ya mwingine haipo tena kwa hiyo, Walutheri na Wakatoliki wameafikiana mambo matano ya kufanyika kwenye maadhimisho ya pamoja ya 2017.

239. Walutheri na Wakatoliki wanaalikwa kuzingatia umoja wa mwili wa Kristo na kuondoa vizuizi vya kuufutilia umoja huu ili kuitumikia jamii ya Kikristo. Kwa njia ya ubatizo wanatambuana kuwa wote ni Wakristo. Jambo hili linahitaji mabadiliko endelevu ya moyo.

| |
|---|
| AZIMIO LA KWANZA: Wakatoliki na Walutheri waanze kushiriki kutokana na Umoja uliopo na sio kutokana na tofauti zilizopo ili wawe pamoja japo tofauti zinaonekana wazi katika maisha halisi. |

240. Katika Historia maungamo ya Kikatoliki na Kilutheri yametambulisha upande mmoja dhidi ya mwingine na kuzalisha ubinafsi unaoathiri utatuzi wa maswala kama yahusuyo mamlaka. Hivyo, utatuzi unawezekana kwa njia ya kuimarisha ushirikiano. Kila upande unahitaji uzoefu, kutiwa moyo na ukosoaji wa mwenzake.

| |
|---|
| AZIMIO LA PILI: Walutheri na Wakatoliki lazima waruhusu mabadiliko ya mara kwa mara kila wanapokutana na kushirikiana kushuhudia imani. |

241. Wakatoliki na Walutheri wamejifunza katika mazungumzo na kuona kuwa ushirikiano unawezekana katika namna na viwango mbalimbali. Kwa ajili ya 2017, bidii iongezwe kwa shukrani ya yale ambayo

yameshafikiwa kwenye ushirikiano, kwa ustahimilivu na uvumilivu kwa kuwa bado safari ni ndefu kuliko inavyoweza fikiriwa kwa hamu isiotosheka na hali ilivyo sasa, kwa upendo hata katika nyakati za kutokubaliana kwa imani katika Roho Mtakatifu, kwa imani kuwa Roho Mtakatifu atatimiza maombi ya Yesu Kristo kwa Baba kuruhusu wawe na umoja, na maombi ya dhati kuwa hayo yatatimia.

AZIMIO LA TATU: Wakatoliki na Walutheri wajitahidi kutafuta umoja unaoonekana, kueleza kwa pamoja maana ya umoja wa namna hii, na kujitahidi wakati wote kuufikia.

242. Wakatoliki na Walutheri wanalo jukumu la kudhihirisha kwa upya uelewa wa Injili, imani ya Kristo na mapokezi ya Kanisa. Changamoto ya kuepukwa ni kurejea kwenye upinzani wa zama katika mafundisho hayo.

AZIMIO LA NNE: Walutheri na Wakatoliki wanapaswa kuitambua nguvu ya Injili ya Yesu Kristo kwa wakati huu.

243. Lengo la kujidhihirisha na mambo ya pamoja ni kwa Kanisa na kwa ulimwengu uweze kuamini. Kazi ya Utume itakuwa ngumu zaidi katika mwingiliano wa jamii na dini mbalimbali. Hivyo kufikiri tena na toba vinahitajika.

AZIMIO LA TANO: Wakatoliki na Walutheri wanapaswa kushuhudia pamoja huruma ya Mungu katika kutangaza na kuhudumia ulimwengu.

244. Safari ya pamoja imewezesha Wakatoliki na Walutheri kukubali mafundisho ya Martin Luther kuhusu haki ya Mungu, ambapo pia ni huruma ya Mungu. Katika dibaji ya kazi ya lugha ya Kilatini (1545), alisema kuwa “Kwa huruma ya Mungu kutafakari usiku na mchana” amepata uelewa mpya wa Warumi 1:17: “hapa nilijisikia nimezaliwa upya kuingia Paradiso milango ili wazi. Na kutokea hapo maandiko

mengine yalikuwa dhahiri kwangu. Baadaye nilisoma waraka wa Agustino kuhusu Roho na barua, niligundua tofauti kuwa, yeye pia, alitafsiri haki ya Mungu vivyo hivyo kuwa Mungu ametuvika haki hiyo anapotuhesabia haki."[1]

245. Mwanzo wa Matengenezo utakumbukwa kwa usahihi pale Walutheri na Wakatoliki watakaposikiliza kwa pamoja Injili ya Yesu Kristo na kuitikia wito wa kuwa jamii moja ya Kristo. Ndipo watakapoungana katika utume ambao fundisho la kuhesabiwa haki linaelezea "Walutheri na Wakatoliki wana lengo moja la kumkiri Kristo kwa kila kiumbe, yeye pekee ni wa kuaminiwa kuliko vitu vyote kuwa mpatanishi (1Tim. 2: 5) ambaye Mungu kwa njia ya Roho Mtakatifu amejitoa na kumimina vipawa vyake vya kutufanya wapya." (JDDJ 18).

[1] Luther, "Preface to the Complete Edition of Luther's Latin Writings," tr. Lewis W. Spitz, Sr., katika *LW* 34:337; *WA* 54; 186, 3.8–10.16–18.

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| AAS | Acta Apostolicae Sedis |
| *ApC* | *The Apostolicity of the Church: Study Document of the Lutheran-Roman Catholic Commission on Unity* (2006) |
| Apol. | Apology of the Augsburg Confession (1530) |
| AS | Smalcald Articles (1537) |
| *BC* | *The Book of Concord: The Confessions of the Evangelical Lutheran Church,* (Minneapolis, MN: Fortress, 2000) |
| *BSLK* | *Die Bekenntnisschriften der evangelisch-lutherischen Kirche* (Göttingen, 1930; 10th ed. 1986) |
| CA | Augsburg Confession |
| can. | Canon |
| *CD* | Vatican II: Decree on the Pastoral Office of Bishops in the Church, *Christus Dominus* |
| *DH* | H. Denzinger and P. Hünermann (eds), *Enchiridion symbolorum definitionum et declarationum de rebus fidei et morum* (Freiburg, 2001) |
| *DV* | Vatican II: Dogmatic Constitution *Dei Verbum* |
| Epit. | Epitome (Formula of Concord) |
| *Eucharist* | *The Eucharist: Final Report of the Joint Roman Catholic-Lutheran Commission* (1978) |

| | |
|---|---|
| FC | Formula of Concord (1577) |
| *JDDJ* | *Joint Declaration on the Doctrine of Justification* (1999) |
| LC | M. Luther, Large Catechism (1529) |
| *LG* | Vatican II: Dogmatic Constitution on the Church, *Lumen Gentium* |
| *LW* | *Luther's Works,* American Edition, ed. J. Pelikan and H. T. Lehmann, 54 vols (Philadelphia and St. Louis, 1955–1986) |
| LWF | The Lutheran World Federation |
| *Ministry* | *Ministry in the Church,* Lutheran-Roman Catholic Conversation, 1981. |
| *PO* | Vatican II: Decree on the Ministry and Life of Priests, *PresbyterorumOrdinis* |
| *SC* | Vatican II: Constitution on the Sacred Liturgy, *Sacrosanctum Concilium* |
| SmC | M. Luther, Small Catechism (1529) |
| *STh* | Thomas Aquinas, *Summa Theolojiae,* Latin/Engl., Blackfriars (London and New York, 1963) |
| *UR* | Vatican II: Decree on Ecumenism, *Unitatis Redintegratio* |
| *WA* | M. Luther, Werke (Weimar, 1883ff.) (Weimarer Ausgabe) |
| *WAB* | D. Martin Luthers Werke-Briefwechsel (Weimar, 1930ff) |

# Maazimio ya Pamoja

## Awamu ya Kwanza (1967–1972)

*Injili na Kanisa (The Gospel and the Church)* (Malta Report – 1972)

## Awamu ya Pili (1973–1984)

*Ekaristi (The Eucharist)* (1978)

*Wote Chini ya Kristo Mmoja (All Under One Christ)* (1980)

*Kuelekea Jumuiya (Ways to Community)* (1980)

*Huduma ndani ya Kanisa (The Ministry in the Church)* (1981)

*Martin Luther – Ushuhuda wa Kristo (Martin Luther – Witness to Christ)* (1983)

*Kukabiliana na umoja – Vielelezo, Miundo na Awamu za Ushirika wa Kanisa Katoliki-Kilutheri* (*Facing Unity – Models, Forms and Phases of Catholic-Lutheran Church Fellowship)* (1984)

## Awamu ya Tatu (1986–1993)

*Kanisa na Kuhesabiwa Haki (Church and Justification)* (1993)

## Awamu ya Nne (1995–2006)

*Utume wa Kanisa (The Apostolicity of the Church)* (2006)

*Azimio la pamoja kuhusu Fundisho la kuhesabiwa haki* – lililosainiwa na wawakilishi wa Kanisa Katolic na wa Shrikisho la Walutheri Duniani *(oint Declaration on the Doctrine of Justification* signed by representatives of the Catholic Church and the Lutheran World Federation), 31 October 1999.

# Tume ya Walutheri – Wakatoliki Kuhusu Umoja

## Walutheri

### Wajumbe

Askofu Mstaafu Dk Eero Huovinen (Mwenyekiti Mwenza), Finland
Mch. Prof. Dk Wanda Deifelt, Brazil
Dk Sandra Gintere, Latvia
Prof. Dk Turid Karlsen Seim, Norway
Mch. Dk. Fidon R. Mwombeki, Tanzania
Prof. Dk Friederike Nüssel, Germany
Prof. Dk Michael Root, USA (2009)
Mch. Prof. Dk Hiroshi Augustine Suzuki, Japan
Mch. Prof. Dk Ronald F. Thiemann, USA (2010–)

### Mshauri

Mch. Prof. Dk Theodor Dieter, Taasisi ya Utafiti ya Ekumene, Strasbourg

### Mtendakazi

***(Fungamano la Makanisa Kilutheri Duniani)***

Prof. Dk Kathryn L. Johnson, Katibu Mwenza

# Wakatoliki

## Wajumbe

Askofu Prof. Dk Gerhard Ludwig Müller (Mwenyekiti Mwenza), Germany (2009–2012)
Askofu Prof. Dk Kurt Koch, Switzerland (2009)
Askofu Mwenza Prof. Dk Karlheinz Diez, Germany (2012–)
Padri Prof. Dk Michel Fédou, S.J., France
Padri Prof. Dk Angelo Maffeis, Italy
Prof. Dk Thomas Söding, Germany
Prof. Dk Christian D. Washburn, USA
Prof. Dk Susan K. Wood, SCL, USA

## Washauri

Prof. Dk Eva-Maria Faber, Switzerland
Prof. Dk Wolfgang Thönissen, Johann-Adam-Möhler-Institut für Ökumenik, Germany

## Watumishi

(***Baraza la Kipapa Linalohimiza Umoja wa Kikristo)***

Mons. Dr Matthias Türk, Katibu Mwenza

Mnamo mwaka wa 2017, Wakatoliki na Walutheri kwa pamoja walitazama nyuma kuhusu matukio ya Matengenezo ya Kanisa kwa miaka 500 iliyopita.

Wakati huo huo, walitafakari miaka 50 ya mazungumzo rasmi ya kiekumene katika ngazi ya dunia nzima.

Wakati huu, ushirika wanaoshiriki upya umeendelea kukua. Hii inawatia moyo Walutheri na Wakatoliki kuadhimisha kwa pamoja ushuhuda wa pamoja wa Injili ya Yesu Kristo, ambaye ndiye kitovu cha imani yao ya pamoja. Hata hivyo, katikati ya adhimisho hili, pia wanayo sababu ya kushiriki machungu yaliyosababishwa na mgawanyiko wa Kanisa, na kujitathimini kwa kina wenyewe, si tu katika historia yote, bali hata katika hali halisi ya leo.

Andiko "Kutoka Ugomvi hadi Ushirikiano" linakuza msingi wa ukumbusho wa kiekumene ambao ni tofauti na karne zilizotangulia. Tume ya Umoja wa Kilutheri-Kirumi inawaalika Wakristo wote kusoma ripoti yake kwa uwazi na kwa makini, na kutembea katika njia kuelekea umoja kamili unaoonekana wa Kanisa.

ISBN 978-9976-5629-3-4

9 789976 562934